Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki

WIZARA WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

# HOTUBA YA MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.)

## AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025



# VIONGOZI WAKUU
## Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



**Mheshimiwa January Makamba (Mb.)**
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano
wa Afrika Mashariki



**Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb.)**
Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano
wa Afrika Mashariki



**Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.)**
Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
Anayeshughulikia Masuala ya Afrika Mashariki



**Balozi Dkt. Samweli Shelukindo**
Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Afrika Mashariki



**Balozi Stephen P. Mbundi**
Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano
wa Afrika Mashariki Anayeshughulikia Masuala
ya Afrika Mashariki



**Balozi Said Shaib Mussa**
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano
wa Afrika Mashariki

# Jedwali la Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| **1.0** | **UTANGULIZI** | **02** |
| **2.0** | **MISINGI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UHUSIANO WA KIMATAIFA** | **12** |
| **3.0** | **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** | **19** |
| 3.1 | MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | **20** |
| 3.2 | UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE | **23** |
| 3.2.1 | Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje | **23** |
| 3.2.2 | Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi | **24** |
| 3.2.3 | Kusimamia na Kuratibu masuala ya uhusiano baina ya Jamhuri ya Muungano waTanzania na nchi nyingine | **35** |
| 3.2.4 | Ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa | **57** |
| 3.2.5 | Ushirikiano wa Kimataifa | **70** |
| 3.2.6 | Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (OACPS) | **76** |
| 3.2.7 | Uratibu wa Watanzania wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora) | **76** |
| 3.2.8 | Kuratibu Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli | **78** |
| 3.2.9 | Diplomasia ya Umma | **79** |
| 3.2.10 | Kujengea Uwezo wa Watumishi na Kuimarisha Mazingira ya Kazi | **81** |
| 3.2.11 | Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara | **82** |
| 3.2.12 | Kusimamia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara | **86** |
| **4.** | **CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO** | **91** |
| **5.** | **SHUKRANI** | **92** |
| **6.** | **VIPAUMBELE, MALENGO NA MAJUKUMU YA KUZINGATIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** | **94** |

| | | |
|---|---|---|
| 6.1 | Vipaumbele | **95** |
| 6.2 | Malengo na Majukumu ya Kuzingatiwa | **96** |
| **7.** | **MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** | **99** |
| 7.1 | KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA ARUSHA (AICC) | **99** |
| 7.2 | KITUO CHA UHUSIANO WA KIMATAIFA CHA DKT. SALIM AHMED SALIM (SAS – CFR) | **100** |
| 7.3 | MPANGO WA HIARI WA AFRIKA WA KUJITATHMINI KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA NA DEMOKRASIA | **101** |
| 8. | **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025** | **102** |
| 8.1 | MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA MAKAO MAKUU | **102** |
| 8.2 | MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025 | **103** |
| **9.** | **HITIMISHO** | **104** |

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area |
| AfDB | African Development Bank |
| AICC | Arusha International Convention Centre |
| APRM | African Peer Review Mechanism |
| AU | African Union |
| AWCCSP | African Women Clean Cooking Support Programme |
| BRICS | Brazil, Russia, India, China and South Africa |
| EAC | East African Community |
| EALA | East African Legislative Assembly |
| EU | European Union |
| FAO | United Nations Food and Agriculture Organisation |
| GPAP | Global Plastic Action Partnership |
| IEA | International Energy Agency |
| IGAD | Intergovernmental Authority on Development |
| IPU | Inter-Parliamentary Union |
| IDD | International Direct Dialling |
| IORA | Indian Ocean Rim Association |
| MINUSCA | Misheni ya Umoja wa Mataifa ya kulinda amani nchini Afrika ya Kati |
| MCC | Millenium Challenge Corporation |
| NAM | Non-Aligned Movement |
| NSSF | National Social Security Fund |
| OACPS | Organisation of African, Caribbean and Pacific States |
| OCHA | United Nations Office for Coordination of Humanitarian Affairs |
| OSBP | One Stop Border Post |
| SADC | Southern African Development Community |
| SAMIM | SADC Mission in Mozambique |
| SAMIDRC | SADC Mission in  the Democratic Republic of Congo |
| SAS-CFR | Dr. Salim Ahmed Salim Centre for Foreign Relation |
| UNIFIL | United Nations Interim Force in Lebanon |
| UNICEF | United Nations Children's Fund |
| WB | World Bank |
| WFP | World Food Programme |
| WEF | World Economic Forum |



**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# 01 Utangulizi

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, na lijadili na kupitisha mpango na bajeti ya Wizara na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na makadirio ya mapato na matumizi.

3. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa heshima na unyenyekevu, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mimi pamoja na viongozi wenzangu katika Wizara hii, tunaahidi kuendelea kutimiza majukumu yetu kwa weledi, ari, ubunifu, kujituma, na kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sera na sheria za ndani pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa kuimarisha uhusiano wa kimataifa na kulinda maslahi ya taifa letu duniani.



Mheshimiwa January Y. Makamba (Mb.), akiapishwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 01 Septemba 2023

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

5. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu (3) ya uongozi mahiri na wa vitendo wenye mafanikio makubwa yanayoonekana katika sekta mbalimbali. Aidha, akiwa mwanadiplomasia namba moja hapa nchini, ameendelea kuimarisha uhusiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi mbalimbali, taasisi za kikanda na kimataifa na kuliletea heshima kubwa taifa letu. Katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wake, Mheshimiwa Rais ametumia diplomasia kwa umahiri wa hali ya juu kulinda na kutimiza malengo ya kiuchumi ya taifa letu kama inavyojidhihirisha katika maeneo mengi kwenye hotuba hii.




Miaka Mitatu ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muunganowa Tanzania

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa utendaji wao mahiri na wakizalendo ambapo ushauri wao umemwezesha Mheshimiwa Rais kutekeleza azma yake ya kuharakisha maendeleo ya taifa letu.



Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi



Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.)
Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa upekee kabisa naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Aidha, naungana na waheshimiwa mawaziri, wabunge na watanzania wenzangu kuendelea kuwaombea viongozi wetu wakuu kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema, hekima, busara na mafanikio katika kutekeleza majukumu ya kuiongoza nchiyetu.

8. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote na viongozi mbalimbali walioteuliwa na walioendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi na nyadhifa mbalimbali katika wizara, taasisi, wakala na vyombo vya Serikali. Kwa dhati kabisa, nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao. Nitaendelea kutoa ushirikiano kwao katika kutimiza azma na malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. **Kazi iendelee!**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) kuwa Naibu Waziri Mkuu (Uratibu wa Shughuli za Serikali) na Waziri wa Nishati katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu ndogo Tunguu Zanzibar Mwezi Septemba, 2023.

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake iliyoeleza kwa ufasaha kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2023/2024 na mwelekeo wa mwaka 2024/2025. Vilevile, nawapongeza mawaziri wenzangu walionitangulia kwa kuwasilisha vyema hotuba zao mbele ya Bunge lako Tukufu, ambazo zimeainisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

10. **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Baraza la Uongozi la IPU ambalo ni chombo kikuu cha maamuzi kinachojumuisha Mabunge kutoka duniani kote. Umekuwa mwanamke wa kwanza shupavu kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu historia ya kuanzishwa kwa chombo hicho. Hivyo, siyo tu umeipa sifa njema nchi yetu ya Tanzania kimataifa, bali pia umeendelea kuwa kioo kwa wanawake na vijana wa kitanzania hususani wa kike, na kuwadhihirishia kuwa inawezekana kwao kushindana na kupigania nafasi za uongozi katika taasisi za kikanda na kimataifa. **Hongera Sana!!**

11. **Mheshimiwa Spika,** aidha, nakupongeza kwa dhati, wewe pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb,), Naibu Spika wa Bunge mkishirikiana na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deogratius Philip




Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani akiongoza moja ya Kikao cha Bunge hilo kilichofanyika hivi karibuni. Dkt. Tulia alichaguliwa kushika wadhifa huo mwezi Oktoba 2023.

Mwanyika Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge hili Tukufu. Juhudi na maarifa yenu vimeendelea kukipa heshima chombo hiki muhimu mbele ya umma wa watanzania, jumuiya ya kimataifa na kukiwezesha kuisimamia na kuishauri ipasavyo Serikali.



Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

12. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia, na kwa kazi kubwa ya kuishauri Wizara, na Serikali kwa ujumla. Miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali imekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, kwa muktadha huo, nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati nyingine za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu ya kuisimamia na kuishauri Serikali.



Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumwamini Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo kuwa Katibu Mkuu.



Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb.)
Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

14. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuwateua Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Balozi Stephen Patrick Mbundi kuwa Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki na Balozi Said Shaibu Mussa kuwa Naibu Katibu Mkuu. Napenda kuwashukuru viongozi hao kwa ushirikiano wa dhati wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nipende kutumia fursa hii kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudi zao katika kufanikisha malengo ya Wizara.



Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), akiapa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki



**Mheshiwa January Makamba (Mb.)**
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



**Balozi Dkt. Samweli Shelukindo**
Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki



**Balozi Stephen P. Mbundi**
Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki



**Balozi Said Shaib Mussa**
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

15. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru mtangulizi wangu Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb.), kwa kazi nzuri aliyoifanya na kuweka misingi inayoniwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

16. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo, uvumilivu na kuniombea kuendelea kutekeleza majukumu yangu kwa juhudi na weledi.

17. **Mheshimiwa Spika,** nchi yetu kwa nyakati tofauti imekumbwa na maafa na matukio mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, na uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao katika maafa. Aidha, ninamuomba Mwenyezi Mungu awajalie majeruhi wote uponyaji wa haraka na aendelee kuwapumzisha kwa amani wale waliopoteza maisha.

18. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uthubutu wake wa kuruhusu mageuzi ya mfumo wa kisiasa na kiuchumi wa taifa letu utakumbukwa daima. Vilevile, tutamkumbuka kwa hulka ya ustahamilivu, unyenyekevu na uwajibikaji. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Dkt. Husein Ali Mwinyi wakitoa heshima za mwisho kwenye jeneza la hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungaano wa Tanzania aliyefariki dunia Februari 2024

19. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, hivi karibuni tumeondokewa na mwanasiasa nguli na mahiri, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo ambaye atakumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi mkubwa wa kisiasa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe marehemu pumziko la milele. Amina.

20. **Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, waheshimiwa wabunge na wananchi wote kwa msiba uliolipata Bunge lako Tukufu kufuatia kufariki kwa Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi; Amina. Aidha, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara na taasisi zilizo chini yake kutoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko yaliyotokea katika msimu huu wa mvua kwenye maeneo mengi nchini.

21. **Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuishukuru jumuiya ya kidiplomasia hapa nchini kwa kushiriki pamoja nasi katika misiba hii mizito ya kitaifa na kuratibu misaada ya fedha na vifaa iliyoelekezwa kwa waathirika wa maafa. Kadhalika, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kutoa salamu za pole kwa viongozi wakuu wa nchi na Serikali na wananchi wa mataifa ya Jamhuri ya Watu wa China, Urusi, Malawi, Madagascar na Msumbiji kufuatia maafa yaliyosababishwa na ajali na majanga ya asili ikiwemo vimbunga, maporomoko ya udongo na mafuriko.

22. **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa pole kwa mataifa ya Namibia, Kuwait na Iran kwa misiba mizito ya kitaifa kufuatia vifo vya viongozi wakuu wa nchi hizo. Mheshimiwa Dkt. Hage Geingob aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Namibia, Mtukufu Sheikh Nawaf Al Ahmad Al Jaber Al Sabah, aliyekuwa Amiri wa Kuwait na Mheshimiwa Dkt. Sayyed Ebrahim Raisi aliyekuwa Rais wa Iran ambaye amefariki katika ajali ya Helikopta.

23. **Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na mataifa hayo katika kipindi hiki kigumu, na tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema roho za marehemu. Aidha, tunawaombea majeruhi wote wapone kwa haraka na kurejea katika utekelezaji wa shughuli za kujenga mataifa yao.

24. **Mheshimiwa Spika,** aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, nchi za Senegal, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zimbabwe, Misri, Comoro, Pakistan, Malaysia, Maldives, Indonesia, Iran, New Zealand, Finland, Shirikisho la Urusi, Uholanzi, Uturuki, Malta, Croatia, Bulgaria, Czech Republic, Hungary, Greece, Portugal, Azerbeijan, Belarus, Slovakia na Poland zilifanya chaguzi za kuwachagua Viongozi wa nchi zao katika hali ya amani na utulivu. Nawapongeza wananchi wa nchi hizo kwa kukamilisha zoezi hilo kwa amani na kwa njia za kidemokrasia. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kushirikiana na viongozi waliochaguliwa na Serikali zao ili kuimarisha uhusiano uliopo baina yetu. Aidha, natumia nafasi hii kuzitakia kheri nchi zinazotarajia kufanya uchaguzi katika kipindi kilichosalia kwa mwaka huu na mwaka ujao wa fedha wa 2024/2025 ambazo ni Afrika Kusini, India, Algeria, Msumbiji, Namibia, Mauritania, Rwanda, Ghana, Sudani Kusini, Uingereza, Marekani, Croatia, Austria, Georgia, Lithuania, Venezuela, Ireland, Mexico, Belgium na Umoja wa Ulaya.

# 02 Misingi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Katika Uhusiano wa Kimataifa

25. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imeendelea kuwa na ushawishi katika Jumuiya ya Kimataifa na kusimamia misingi madhubuti iliyowekwa na Waasisi wa Taifa letu katika uhusiano wa kimataifa ambayo inapinga na kulaani vitendo vya uonevu na ukandamizaji popote duniani, kulinda uhuru na kujiamulia mambo yetu wenyewe; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza sera ya kutofungamana na upande wowote kama dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa. Kwa muktadha huo, Tanzania imeendelea kushiriki katika kulinda amani, kudumisha umoja na mshikamano, kuhimiza maendeleo na kupinga dhuluma.

26. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya siasa, ulinzi na usalama wa dunia kama ifuatavyo:

## AFRIKA

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, hali ya siasa, ulinzi na usalama Barani Afrika ni ya kuridhisha licha ya kuendelea kwa migogoro na matukio ya kigaidi, hususan nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Somalia, Libya, Msumbiji na Sudan. Vilevile, katika miaka ya hivi karibuni, Bara la Afrika limeshuhudia ongezeko la matukio ya kigaidi, hususan katika eneo la Sahel na Pembe ya Afrika na pia mapinduzi ya Serikali hasa katika eneo la Magharibi mwa Afrika. Mpaka sasa takriban nchi sita zimesimamishwa kushiriki shughuli za Umoja wa Afrika kutokana na mapinduzi ya Serikali. Nchi hizo ni Burkina Faso, Gabon, Guinea, Mali, Niger na Sudan. Miongoni mwa masuala yanayochochea kuzorota kwa amani na usalama Barani Afrika ni ukosefu wa utawala bora, mgawanyo usio sawa wa rasilimali, umasikini, ukosefu wa ajira, ukiukwaji wa haki za binadamu na ushawishi kutoka mataifa ya nje.

### JAMHURI YA SUDAN

28. **Mheshimiwa Spika,** hali ya usalama katika Jamhuri ya Sudan haijaimarika kutokana na mapigano yanayoendelea kati ya Jeshi la Sudan (Sudan Armed Forces - SAF) na kikosi cha Msaada wa Haraka (Rapid Support Forces - RSF) yaliyoanza mwezi Aprili 2023. Mapigano hayo yamesababisha vifo vya zaidi ya watu 10,000; wakimbizi milioni 1.2 na wengine milioni 8 kulazimika kuyahama makazi yao. Tanzania inaendelea kuzisihi pande hizo mbili za mgogoro kusitisha mapigano na kurejea kwenye meza ya mazungumzo chini ya Umoja wa Afrika na Intergovernmental Authority on Development (IGAD).

## JAMHURI YA AFRIKA YA KATI (CAR)

**29. Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) imekuwa na changamoto za kiusalama kutokana na matishio kutoka kwa makundi ya waasi yanayoipinga Serikali iliyopo madarakani na kugombania umiliki wa maeneo yenye rasilimali za madini. Tanzania inashiriki katika juhudi za kurejesha amani kwa kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa ya kulinda amani nchini Afrika ya Kati (MINUSCA).

## LIBYA

**30. Mheshimiwa Spika,** hali ya ulinzi na usalama nchini Libya bado sio shwari kutokana na kuendelea kwa mgogoro kati ya pande mbili; Serikali inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa yenye Makao yake Makuu Tripoli na Serikali inayoungwa mkono na Bunge la nchi hiyo yenye Makao Makuu kwenye mji wa Tobruk. Pande hizo mpaka sasa hazijafikia makubaliano kuhusu kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi.

## ULAYA NA AMERIKA

**31. Mheshimiwa Spika,** kiujumla hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Ulaya na Amerika imeendelea kuwa ya amani isipokuwa mgogoro unaondelea kati ya Shirikisho la Urusi na Jamhuri ya Ukraine. Hali hiyo imechangia kuzorota kwa hali ya usalama katika eneo la mashariki ya Ulaya. Aidha, mgogoro huo umesababisha kudorora kwa uchumi wa dunia, ambapo nchi nyingi, ikiwemo Tanzania zimeendelea kushuhudia kuongezeka kwa mfumuko wa bei za bidhaa na huduma hasa vyakula, nishati ya gesi na mafuta na mbolea. Tanzania inaendelea kuzisihi pande zote mbili kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano ili kurejesha amani na usalama.

**32. Mheshimiwa Spika,** vilevile Taifa la Haiti limekuwa likikabiliwa na ukosefu wa utulivu kwa muda mrefu, udikteta na majanga ya asili yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu na uchumi. Katika tukio la hivi karibuni lililotokea mwezi Machi 2024, dunia ilishuhudia Kaimu Rais na Waziri Mkuu Mheshimiwa Ariel Henry akijiuzulu kutokana na ongezeko la ghasia na shinikizo la magenge ya wahalifu. Itakumbukwa kuwa mnamo 2021, Rais Jovenel Moïse aliuawa na watu wenye silaha huko Port-au Prince.

**33. Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo Haiti imeendelea kukabiliwa na machafuko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kuongezeka kwa vita baina ya magenge ya wahalifu ambayo yameifanya nchi hiyo kuendelea kuwa maskini zaidi katika Bara la Amerika. Tanzania inaendelea kuunga mkono jitihada za Jumuiya za Kimataifa katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano ili kurejesha amani na usalama.

## ASIA NA AUSTRALASIA

**34. Mheshimiwa Spika,** hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Asia na Australasia imeendelea kuimarika isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:

## INDIA NA PAKISTAN

**35. Mheshimiwa Spika,** Mgogoro wa India na Pakistan wa kugombea eneo la Jammu na Kashmir ni wa muda mrefu na unachochewa na uwepo wa makundi yenye itikadi kali zinazokinzana. Hali hii inachangia kudorora kwa uchumi na kuwepo kwa machafuko ya mara kwa mara. Aidha, uwepo wa hali hii unakwamisha juhudi za kimataifa katika kutafuta Amani na kufikia suluhu ya kudumu katika eneo hilo. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa katika kudumisha Amani na usalama katika eneo hilo.

## RASI YA KOREA

**36. Mheshimiwa Spika,** hali ya usalama katika Rasi ya Korea imeendelea kuwa ya mashaka

kutokana na mvutano uliopo baina ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea na Jamhuri ya Korea na washirika wao. Pande zote mbili zinakubaliana na dhamira ya kushikilia maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kufikia azimio endelevu na la amani. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa za usuluhishi wa mgogoro huo kwa njia ya amani.

## MASHARIKI YA KATI

37. **Mheshimiwa Spika,** hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Mashariki ya Kati imeendelea kuimarika isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:

### ISRAEL NA PALESTINA

38. **Mheshimiwa Spika,** mgogoro kati ya Israel na Palestina ni wa muda mrefu, na umeendelea kuleta changamoto za kiusalama katika eneo la ukanda huo kutokana na mapigano yanayoendelea hivi sasa kati ya Jeshi la Serikali ya Israel (IDF) na Kundi la Hamas. Mgogoro huu umesababisha athari kubwa kama vile, vifo na majeruhi, uharibifu wa makazi na miundombinu pamoja na kuzorotesha upatikanaji wa huduma muhimu za kibinadamu. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoratibu masuala ya kibinadamu (United Nations Office for Coordination of Humanitarian Affairs - OCHA) mwezi Aprili, 2024 inakadiriwa kuwa zaidi ya watu elfu thelathini wamepoteza maisha na kusababisha majeruhi zaidi ya watu elfu sabini kwa pande zote mbili.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika mgogoro huu unaoendelea hivi sasa Tanzania tulipoteza vijana wetu wawili ambao walikuwa nchini Israel kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kuhusu kilimo cha kisasa. Tunatuma pole za dhati kwa familia na wapendwa wa vijana hao wawili waliopoteza maisha yao. Ni pigo kubwa kwa Nchi yetu kupoteza vijana waliojitolea kujifunza ili kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo. Tunawaombea faraja na nguvu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia umuhimu wa kupatikana amani ya kudumu katika mgogoro huu, msimamo wa Tanzania ni kuendelea kuunga mkono juhudi za Umoja wa Mataifa na msimamo wa Umoja wa Afrika unaozitaka pande husika kuheshimu makubaliano ya kuwepo kwa mataifa mawili huru ya Palestina na Israel na yanayoishi kwa amani.

### IRAN NA ISRAEL

41. **Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na kuongezeka kwa uhasama baina ya mataifa ya Iran na Israel, hivi karibuni Ubalozi wa Iran nchini Syria ulishambuliwa kwa ndege za kivita na kusababisha vifo vya watu kadhaa wakiwemo makamanda waandamizi wa Jeshi la Mapinduzi la Iran, shambulio linalohisiwa kufanywa na Israel, kufuatia shambulio hilo Iran iliishambulia Israel kwa makombora zaidi ya 300. Siku chache baadae Israel nayo iliishambulia Iran kwa makombora huku kila mmoja akidai kulipiza kisasi kwa kushambuliwa na mwenzake. Tanzania inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kutoa wito kwa mataifa haya kuepuka kufanya vitendo vyovyote vitakavyo sababisha kuzidisha kuzorota kwa hali ya Amani na usalama ili kuepuka kusambaa kwa athari za mgogoro huu na kuleta athari za kiuchumi kwa mataifa mbalimbali duniani.

### JAMHURI YA LEBANON

42. **Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Lebanon imeendelea kukabiliwa na changamoto ya uwepo wa makundi yenye itikadi kali yanayokinzana na hivyo kusababisha kukosekana kwa Serikali imara ya kitaifa. Makundi hayo pamoja na mapigano ya mara kwa mara kati ya Kundi la Hizbullah na jeshi la Israel

kutokana na mzozo wa muda mrefu kuhusu maeneo yanakaliwa na Israel kinyume cha sheria Kusini mwa Lebanon. Aidha, msimamo wa Hizbullah kutetea haki za Wapalestina, imechangia kuendelea kudorora kwa amani katika eneo hilo la Kusini mwa Lebanon na kuleta taharuki katika ukanda mzima wa Mashariki ya Kati. Tanzania inaendelea kushiriki katika juhudi za kulinda amani nchini Lebanon kwa kuchangia walinda amani kupitia Misheni ya Umoja wa Mataifa (UNIFIL).

## JAMHURI YA YEMEN

43. **Mheshimiwa Spika,** hali ya usalama nchini Yemen sio ya kuridhisha kutokana na uwepo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea baina ya majeshi ya serikali na kundi la wanamgambo wa Houthi. Pamoja na vita hivyo, hivi karibuni kundi hili limeanza kushambulia na kuteka meli za mizigo katika eneo la Bahari ya Shamu hali inayodhoofisha biashara ya kimataifa, amani na usalama wa eneo la Mashariki ya kati. Kwa kuzingatia umuhimu wa kupatikana amani ya kudumu katika mgogoro huu, Tanzania imeendelea kuunga mkono juhudi za Jumuiya za Kimataifa za kutafuta amani ya kudumu katika Nchi hiyo.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassa akiwa na mwenyeji wake Rais wa Uturuki Mheshimiwa Recep Tayyip Erdogan wakikagua Gwaride la Heshima mara baada ya kuwasili katika viwanja vya Ikulu ya Kulliye Ankara nchini Uturuki tarehe 18 Aprili 2024.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhemiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza mkutano wa Mifumo ya Chakula Afrika uliojumuisha Marais na Wakuu wa Nchi na Wadau wa Kilimo na Chakula kutoka nchi mbalimbali za Afrika na kwingineko duniani uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Septemba 7, 2023



Mheshimiwa Rais Dkt. Samia akiwa na baadhi ya Marais walioshiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Rasilimali Watu. Kutoka kushoto ni Mhe. Rais William Ruto, Mhe. Rais Lazarus Chakwera, Mhe. Rais Andry Rajoelina wa Madagascar, Mhe. Rais Carlos Vila Nova wa Sao Tome na Principe




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Rais wa Burundi Mhe. Évariste Ndayishimiye pamoja na Rais wa Kenya Mhe. William Ruto wakati wa Wimbo wa Taifa wa Tanzania ukiimbwa kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliojadili kuhusu masuala ya Tabianchi na Usalama wa Chakula uliofanyika Mkoani Arusha tarehe 23 Novemba, 2023




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika picha ya pamoja na Rais wa Afrika Kusini Mhe. Cyril Ramaphosa, Rais wa Zambia Mhe. Hakainde Hichilema, Rais wa Angola Mhe. João Lourenço, Rais wa Zimbabwe Mhe. Emmerson Mnangagwa pamoja na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Félix Tshisekedi pamoja na Viongozi mbalimbali kwenye Mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) jijini Luanda, Angola




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. January Makamba akimkaribisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwahutubia Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania sehemu mbalimbali duniani waliokusanyika mjini Kibaha kwa warsha ya kutathimini utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa January Makamba akichangia mada kwenye Mkutano wa Raisina 2024 uliofanyika jijini New Delhi, nchini India.

# 03 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

44. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024, maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni:-

   a. Kuratibu ziara za kikazi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi, na ziara za Viongozi Wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini kwa lengo la kudumisha uhusiano wa kidiplomasia na kutumia fursa za kiuchumi;

   b. Kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama, hususan Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

   c. Kukamilisha maboresho ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001;

   d. Kuendelea kuratibu na kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

   e. Kutekeleza Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya Balozi za Tanzania;

   f. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;

   g. Kuimarisha ushiriki wa diaspora katika kuchangia maendeleo ya taifa ikiwa ni pamoja na kukamilisha mfumo na taratibu za kutoa Hadhi Maalum kwa diaspora;

   h. Kugharamia mahitaji ya msingi na ya kimkataba ya uendeshaji wa Balozi za Tanzania nje ya nchi ikiwemo pango la ofisi na makazi ya watumishi;

   i. Kuimarisha utendaji kazi wa Balozi na Konseli Kuu kwa kuzipatia rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi stahiki;



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. January Makamba (Mb.) akisalimiana na Waziri wa Mambo ya Nje wa China Mhe. WANG Yi walipokutana Ofini kwa Mhe. Yi jijini Beijing kwa mazungumzo mwezi Mei 2024

j. Kufanikisha uendeshaji wa Makao Makuu ya Wizara kwa kulipa pango, kugharamia huduma za maji, umeme, simu; mafuta ya magari; na kulipa mikataba ya wazabuni;

k. Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

l. Kuimarisha ukaguzi wa ndani na mifumo ya udhibiti Makao Makuu na Balozi za Tanzania; na utunzaji wa mali za Serikali;

m. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, makubaliano ya kikanda na kimataifa;

n. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM);

o. Kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi na kuzingatia maslahi ya mahali pa kazi; na

p. Kutoa elimu kwa umma kuhusu ushirikiano wa kimataifa na fursa zinazopatikana kutokana na nchi yetu kuwa mwanachama wa jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na mikataba/makubaliano kati ya Tanzania na nchi nyingine.

## 3.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

### 3.1.1 Mapato

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kukusanya shilingi 1,559,879,000. Kati ya kiasi hicho, shilingi 150,000,000 ni makusanyo ya makao makuu ya Wizara na shilingi 1,409,879,000 ni makusanyo kutoka balozi za Tanzania nje. Vyanzo vikuu vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka na pango la majengo ya Serikali nje ya nchi.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 988,088,883.10, sawa na asilimia 76.01 ya lengo lililopangwa la shilingi 1,300,116,951.45 kufikia mwezi Aprili 2024. Fedha zote za maduhuli zilizokusanywa na Wizara ziliingizwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama taratibu zinavyoelekeza.

### 3.1.2 Fedha zilizoidhinishwa na kupokelewa

47. **Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 247,971,524,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 230,083,916,000, sawa na asilimia 92.79 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 17,887,608,000, sawa na asilimia 7.21 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida, shilingi 213,304,516,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 16,779,400,000 ni kwa ajili ya mishahara.

48. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Wizara imepokea kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha shilingi 218,365,714,841.09 sawa na asilimia 88.06 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, shilingi 188,255,230,101.48 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 88.26 ya fedha zote za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024; shilingi 13,347,757,781.00 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 79.55 ya fedha zote zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2023/2024; na shilingi 16,762,726,958.61 ni kwa ajili ya maendeleo sawa na asilimia 93.71 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, na fedha zilizopokelewa na kutumika ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na 1 hapo chini.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. January Makamba (Mb.), akifungua Kongamano la kukusanya maoni ya wadau kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 tarehe 9 Januari, 2024 Jijini Dar es Salaam

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa
Julai 2023 – Aprili 2024

| Na. | Matumizi | Fedha Zilizoidhinishwa (Sh.) | Fedha Zilizopokelewa (Sh.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| A | B | C | D | D/C |
| 1 | Matumizi Mengineyo | 213,304,516,000.00 | 188,255,230,101.48 | 88.26 |
| 2 | Mishahara | 16,779,400,000.00 | 13,347,757,781.00 | 79.55 |
| 3 | Maendeleo | 17,887,608,000.00 | 16,762,726,958.61 | 93.71 |
| JUMLA | | 247,971,524,000.00 | 218,365,714,841.09 | 88.06 |

*Chanzo: W-NJ&UAM*

## 3.1.3 Matumizi

**49. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Wizara ilitumia kiasi cha shilingi 217,706,821,535.74 sawa na asilimia 99.70 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 187,596,336,796.13 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 99.65 ya fedha zilizopokelewa; shilingi 13,347,757,781.00 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa; na shilingi 16,762,726,958.61 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, na fedha zilizopokelewa na kutumika ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2 hapo chini.

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa na Kutumika
Julai 2023 – Aprili 2024

| Na. | Matumizi | Fedha Zilizopokelewa (Sh.) | Fedha Zilizotumika (Sh.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| A | B | D | E | E/D |
| 1 | Matumizi Mengineyo | 188,255,230,101.48 | 187,596,336,796.13 | 99.65 |
| 2 | Mishahara | 13,347,757,781.00 | 13,347,757,781.00 | 100.00 |
| 3 | Maendeleo | 16,762,726,958.61 | 16,762,726,958.61 | 100.00 |
| **JUMLA** | | **218,365,714,841.09** | **217,706,821,535.74** | **99.70** |

*Chanzo: W-NJ&UAM*

## 3.2 Utekelezaji Wa Majukumu Ya Wizara Kwa Kuzingatia Vipaumbele

### 3.2.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje

**50. Mheshimiwa Spika,** mwezi Agosti, 2023, Wizara iliwasilisha rasimu ya marekebisho ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 na rasimu ya Waraka kwa ajili ya kujadiliwa na Baraza la Mawaziri ambalo lilijadili rasimu hiyo na kuielekeza Wizara kukusanya maoni zaidi ya wadau kuhusu mapendekezo yaliyomo kwenye Sera inayorekebishwa.

**51. Mheshimiwa Spika,** napenda kuifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza maelekezo hayo Wizara imeratibu makongamano matano ya wadau ambapo kongamano la kwanza lilifanyika mwezi Novemba, 2023 Jijini Arusha; kongamano la pili lilifanyika mwezi Januari, 2024 Jijini Dar es Salaam; kongamano la tatu lilifanyika mwezi Februari, 2024 Unguja; kongamano la nne lilifanyika mwezi Februari, 2024 Pemba; na kongamano la tano lilifanyika mwezi Aprili, 2024 katika Mkoa wa Mwanza.




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. January Makamba (Mb) akifungua Kongamano la Wadau kukusanya maoni ya marekebisho ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 lililofanyika mjini Zanzibar Mwezi Februari 2024

52. **Mheshimiwa Spika,** Makongamano hayo yalihudhuriwa na wadau kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii ikiwemo viongozi wa serikali kuu, tawala za mikoa na serikali za mitaa, mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi, viongozi wa vyama vya siasa, wasomi, wawakilishi wa taasisi za kidini; wawakilishi wa asasi za kiraia, sekta binafsi, taasisi za elimu, diaspora, makundi maalum, vijana na wananchi kwa ujumla.

53. **Mheshimiwa Spika,** nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, maoni yote yaliyokusanywa kupitia makongamano hayo yanaendelea kufanyiwa uchambuzi na wataalam wa Wizara na tayari yamejumuishwa kwenye rasimu ya sera na mkakati wake wa utekelezaji. Aidha, Wizara imepanga kupokea maoni ya wadau mbalimbali kupitia makongamano katika mikoa ya Mbeya, Mtwara na Dodoma.

### 3.2.2 Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi

54. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Wizara iliendelea kuratibu na kufanikisha jitihada mbalimbali zinazolenga kunufaisha Taifa kiuchumi kupitia uhusiano wa kidiplomasia. Jitihada hizo zinajumuisha utafutaji wa masoko ya bidhaa na huduma nje ya nchi; kuwezesha uagizaji bidhaa na huduma muhimu kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya ndani; na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Jitihada nyingine ni pamoja na kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo; kuvutia watalii kutoka nje ya nchi; na kutafuta fursa za ajira na ufadhili wa masomo nje ya nchi.

55. **Mheshimiwa Spika,** ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako kuwa, Wizara imekamilisha rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Maandalizi ya mkakati huo yamehusisha ushiriki wa wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi na mchakato wa kukusanya maoni unaendelea. Mkakati huu umeianisha maeneo saba ya kipaumbele ambayo Wizara itayatilia mkazo katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Maeneo hayo ni pamoja na (i)Kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (ii) Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi (iii) Kuvutia watalii kuja Tanzania (iv) Kutafuta misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje (v) Kutafuta fursa za ajira na masomo kwa Watanzania nje ya nchi (vi) Kujenga taswira nzuri ya nchi yetu kimataifa (vii) Kujenga uwezo wa kitaasisi wa Wizara, na Wizara na Taasisi nyingine kusimamia vizuri utekelezaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Kukamilika kwa mkakati huo kutaiwezesha Serikali na wadau wote kutambua majukumu yao katika mnyororo wa hatua za kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuzingatia vipaumbele vya taifa.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Wizara imesimamia shughuli mbalimbali katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Umma na Sekta Binafsi. Shughuli hizi ni pamoja na kuratibu makongamano mbalimbali ya biashara na uwekezaji yanayofanyika pamoja na ziara za Mheshimiwa Rais nchi za nje, kuratibu ziara za watendaji wa serikali mbalimbali katika nchi yetu kuzungumzia masuala ya kiuchumi, biashara na uwekezaji, kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu, na shughuli nyingine nyingi.

57. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Mei 2024, Wizara iliratibu na kufanikisha kuanza kwa k majadiliano ya kibiashara baina ya Tanzania na Marekani. Uzinduzi wa majadiliano hayo unafuatia kutiwa saini kwa Hati ya Makubaliano (MOU) kati ya nchi zetu mbili kupitia mawaziri wa biashara kulikofanyika mwezi Oktoba mwaka 2023 Kukamilika kwa makubaliano hayo kutafungua fursa zaidi kwa nchi zetu mbili kufanya biashara zaidi, na hivyo wafanyabiashara kutoka Tanzania watanufaika na fursa hizo.

58. **Mheshimwa Spika,** Vilevile, mwezi Mei 2024, Wizara imeshirikiana na wadau wengine ikiwemo sekta binafsi kufanikisha Kongamano la Biashara baina ya Uganda na Tanzania ambalo linachangia katika kuleta ushirikiano mkubwa zaidi kwenye biashara na uwekezaji baina ya nchi zetu mbili. Wizara pia imeratibu na kushiriki katika ziara ya makampuni makubwa ya biashara kutoka Ufaransa ambayo yamefanya ziara nchini Tanzania mwezi Mei 2024. Pia, Wizara inaratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Namibia ambalo litafanyika mwishoni mwa mwezi Mei 2024.

59. **Mheshimiwa Spika,** pia mwezi Mei 2024, Wizara kupitia Ubalozi wetu nchini Ubeligiji iliandaa Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Ubeligiji ikiwa pia ni sehemu ya kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Kupitia kongamano hili, wafanyabiashara wa nchi zetu mbili na wawekezaji kutoka Ubeligiji wameweza kubaini fursa mpya za ushirikiano na uwekezaji zilizopo nchini, hususan katika maeneo ya Madini, Utalii, Viwanda, Bandari, Nishati Jadidifu, Uvuvi, Kilimo na Mifugo.

60. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Aprili 2024, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Uturuki. Miongoni mwa mafanikio ya ziara hiyo ni pamoja na upatikanaji wa fursa za masomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Tanzania kuweza kusoma katika vyuo vikuu vya Uturuki kwa ufadhili wa nchi hiyo. Vilevile wahadhiri wa vyuo vikuu kutoka Tanzania watapata fursa za kujiendeleza kupitia tafiti za pamoja, programu za kubadilishana ujuzi (exchange programmes), na mafunzo ya muda mfupi katika vyuo vikuu vya Uturuki; na kubadilishana utaalamu katika masuala ya hifadhi za nyaraka; na kuanzisha ushirikiano wa Sera za Diaspora. Pia, katika ziara hiyo, Tanzania na Uturuki zilisaini hati ya makubaliano ya kubadilishana taarifa na uzoefu baina ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) pamoja na na Mamlaka ya Uwekezaji ya Uturuki, ili kuongeza tija na uzoefu katika kituo chetu cha Uwekezaji katika kuvutia wawekezaji.

61. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na ziara hiyo, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Uturuki lililofanyika mjini Istanbul, Uturuki, likiwa sehemu ya ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Uturuki. Kongamano hilo lililofunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais akiwa pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Uturuki, limeamsha ari ya ushirikiano kati ya nchi zetu katika sekta mbalimbali hususan sekta za miundombinu, utalii, elimu, afya biashara, uzalishaji na sekta nyingine za kiuchumi. Kupitia ziara na kongamano hilo,



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Mwenyeji wake Rais wa Uturuki, Mheshimiwa Recep Tayyip Erdogan mara baada ya kukagua Gwaride la Heshima katika viwanja vya Ikulu ya Kulliye Ankara nchini Uturuki Mwezi Aprili, 2024.

tumeazimia kwa pamoja kukuza biashara kati ya nchi zetu mbili kutoka Dola za Marekani milioni 345 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 1 katika kipindi kifupi kijacho. Kupitia ziara hiyo Wawekezaji kadhaa kutoka Nchi ya Uturuki wamekuja Tanzania kuangalia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali kama vile viwanda vya miundombinu, nguo, kilimo, na nishati jadidifu.

62. **Mheshimiwa Spika,** mwezi April 2024, Wizara kupitia Ubalozi wetu nchini Brazil uliandaa Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Brazil lililofanyika nchini humo na kuhusisha washiriki kutoka sekta ya umma na binafsi kutoka Tanzania na Brazil. Kongamano hilo limechangia kuleta fursa za ushirikiano na kupata wawekezaji kutoka nchini Brazil katika sekta za kilimo, mifugo, utalii, usafirishaji na viwanda.

63. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Februari 2024, Wizara kupitia Ubalozi wetu nchini Uingereza uliendesha semina kwa njia ya mtandao kujenga uelewa wa mfuko wa dhamana wa Uingereza wa uwezeshaji wa mauzo nje (UK Export Finance), ambapo washiriki zaidi ya 80 kutoka kampuni mbalimbali nchini Tanzania walihudhuria, na baadhi wameanza mazungumzo na mfuko huo kwa ajili ya kukuza biashara.


64. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, mwezi Machi 2024, Wizara iliandaa semina kwa ajili ya kukuza uelewa wa wafanyabiashara kutoka Tanzania wanaotaka kuuza bidhaa zao nchini Uingereza juu ya vivutio vya kiushuru vilivyowekwa na nchi ya Uingereza kupitia utaratibu wao mpya wa kufanya biashara na nchi zinazoendelea unaojulikana kama Developing Countries Trading Scheme (DCTS). Zaidi ya washiriki 150 walihudhuria semina hii Jijini Dar es Salaam na wengi wao wameonesha nia ya kuitumia fursa hii kuingia katika soko la Uingereza.

65. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Mei, 2024, Wizara kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani pia uliendesha semina ya kwenye mtandao kwa ajili ya wafanyabiashara wenye nia ya kupeleka bidhaa za kahawa na chai nchini humo. Vilevile Ubalozi huo umefanikisha kufunguliwa kwa Chemba ya Biashara ya Tanzania iliyopo Dallas nchini Marekani ili kuchagiza ongezeko la biashara baina ya Tanzania na Marekani.

66. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Februari 2024, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe wa watendaji wa Serikali ya Iran na wawakilishi wa kampuni saba (7) kutoka nchi ya Iran. Kufuatia ziara hiyo, kampuni ya Tanchoice inayojishughulisha na usindikaji wa nyama imeonekana kukidhi vigezo vya kuuza nyama na bidhaa za nyama katika nchi ya Iran. Aidha, Serikali inakamilisha taratibu zitakazoiwezesha kampuni hiyo kuuza nyama nchini Iran kwa kuzingatia masharti yaliyopo.

67. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Februari, 2024, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Norway. Wakati wa ziara hiyo, nchi hizo zilikubaliana kuendelea kuboresha uhusiano na ushirikiano kwenye sekta za nishati mbadala, kilimo na usalama wa chakula, Uchumi wa buluu, biashara na uwekezaji, utalii, uboreshaji wa mfumo wa ukusanyaji mapato, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, na masuala ya usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

68. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Februari 2024, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe wa watendaji wa Serikali ya Iran na wawakilishi wa kampuni saba (7) kutoka nchi ya Iran. Kufuatia ziara hiyo, kampuni ya Tanchoice inayojishughulisha na usindikaji wa nyama imeonekana kukidhi vigezo vya kuuza nyama na bidhaa za nyama katika nchi ya Iran. Aidha, Serikali inakamilisha taratibu zitakazoiwezesha kampuni hiyo kuuza nyama nchini Iran kwa kuzingatia masharti yaliyopo.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha na Mfalme Harald V wa Norway pamoja na Malkia Sonja alipowsili katika Kasri la Kifalme Jijini Oslo kwa ajili ya ziara ya Kitaifa, mwezi Februari, 2024

69. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, wakati wa ziara hiyo Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliandaa Kongamano la Biashara na Uwekezaji lililotoa fursa ya kunadi na kuchochea ushirikiano baina ya nchi zetu kwenye sekta ya nishati, kilimo, afya na utalii endelevu. Katika Kongamano hilo, Serikali ya Norway iliahidi kuendelea kuhamasisha Kampuni za Norway kuja kuwekeza nchini kwenye sekta za nishati mbadala, teknolojia rafiki kwa mazingira, uvumbuzi, utunzaji mazingira na afya kwa ajili ya maendeleo endelevu. Vilevile, Serikali ya Norway iliarifu kuwa itatenga kiasi cha Dola za Marekani milioni 193 kwa ajili ya Tanzania na kuwezesha Kampuni za Norway kufanya kuwekeza nchini.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais pia alishiriki kwenye ufunguzi wa Jukwaa la Nishati la Oslo (Oslo Energy Forum). Jukwaa hilo liliwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya nishati wakiwemo viongozi wa serikali, sekta binafsi, wanazuoni na asasi za kiraia chini ya kaulimbiu "Action for Transformational Change". Kupitia jukwaa hilo, Mheshimiwa Rais alinadi fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya nishati nchini na kukaribisha wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali kuwekeza nchini. Vilevile, alitoa rai kwa nchi zilizoendelea kushirikiana na nchi zinazoendela kukuza matumizi ya teknolojia ya kijani kwa kuzingatia uwepo wa malighafi ya kutosha ya kuzalisha nishati jadidifu zenye uwezo wa kufikia azma hiyo.

71. **Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alishiriki katika Semina yenye mada ya mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula iliyolenga kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na Norway kwenye maeneno hayo. Katika semina hiyo, Mheshimiwa Rais alipata fursa ya kuanisha masuala mbalimbali ya kipaumbele kwa Tanzania ikiwemo umuhimu wa nchi zilizoendelea kuunga mkono juhudi za Tanzania na nchi nyingine za Afrika kwa kufadhili programu kukabiliana na kujenga ustahimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula.

72. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Nne wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Italia uliofanyika mwezi Januari, 2024 Roma, Italia. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kutambukisha Mpango Mpya wa Maendeleo wa Italia kwa nchi za Afrika unaojulikana kama Mattei Plan wenye thamani ya Euro bilioni 5.5 utakaotekelezwa kuanzia mwaka 2024 hadi 2028. Mpango huo unalenga kuifanya nchi ya Italia kuwa kitovu cha usambazaji wa nishati ya gesi kutoka barani Afrika kwenda nchi za Ulaya. Tanzania ni miongoni mwa nchi nane (8) zilizopewa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango huo.

73. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua za utekelezaji wa Mpango huo, mwezi Machi 2024 Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano baina ya Tanzania na Italia kuhusu mapendekezo ya miradi ya kujumuishwa kwenye Mpango huo. Kufuatia majadiliano hayo, Serikali imewasilisha mapendekezo ya miradi yenye thamani ya dola za marekani 1,991,720,560 takribani na shilingi Trilioni 4.6. Miradi iliyowasilishwa inahusisha sekta za afya; mifugo na uvuvi; utalii; utamaduni; nishati; tafiti na teknolojia; kilimo; usalama wa chakula; na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, utekelezaji wa mpango huo utaleta matokeo chanya katika sekta nyingine zikiwemo elimu, teknolojia ya kisasa na maendeleo ya rasilimali watu.

74. **Mheshimiwa Spika,** Mwezi Januari 2024, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya Mheshimiwa



Mhe. Rais akiwa na mwenyeji wake aliyekuwa Rais wa Indonesia Mhe. Joko Widodo akikagua gwaride alipowasili katika Ikulu ya Bogor jijini Jakarta Indonesia mwezi Januari, 2024

Rais katika nchi ya Indonesia. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alikutana na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Joko Widodo. Pia, wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alihudhuria na kufungua Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Indonesia. Kongamano hilo lilijadili masuala mbalimbali yatakayowezesha kukuza biashara baina ya Tanzania na Indonesia. Mafanikio yaliyopatikana wakati wa kongamano hili ni pamoja na kuwepo kwa dhamira ya dhati ya mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, kusainiwa kwa Hati za Makubaliano (MOUs) zinazolenga kuongeza ama kukuza biashara.

75. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara iliratibu majadiliano ya kiserikali baina ya Tanzania na Marekani yaliyofanikisha kuchaguliwa kuingia katika programu ya uangalizi (threshold program) ya Shirika la Changamoto za Milenia (Millenium Challenge Corporation - MCC). Majadiliano hayo yaliyofanyika mwezi Desemba 2023 yalipelekea mazungumzo kati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bi. Alice Albright, Mkurugenzi Mtendaji wa MCC, ambao walithibitisha uamuzi wa Tanzania kurejeshwa kwenye mpango huo baada ya kipindi cha miaka miwili ya uangalizi.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Millenium Challenge Corporation (MCC) Bibi Alice Albright wakati wa Mkutano wa Viongozi wa Afrika na Marekani uliofanyika Jijini Washington DC nchini Marekani mwezi Desemba 2022

76. **Mheshimiwa Spika,** ushiriki wa Tanzania kwenye programu ya MCC, katika kipindi cha uangalizi, umejikita katika eneo la vizuizi vya biashara na mazingira yanayosababisha vizuizi hivyo. Aidha, itakapofuzu kuingia kwenye mpango kamili (MCC-II) itanufaika zaidi kama ilivyokuwa katika awamu ya kwanza ya ufadhili wa MCC (2008 hadi 2013), ambapo nchi ilinufaika na fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 698, sawa na shilingi trilioni 1.46 zilizotumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, huduma ya maji na nishati.

77. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Desemba 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) katika masuala ya ajira. Kusainiwa kwa makubaliano hayo kutawezesha watanzania kupata ajira zenye staha katika taasisi za umma na binafsi nchini UAE, na hivyo kuongeza vipato vyao na kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

78. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa makubaliano hayo umeanza kwa mafanikio ambapo mwezi Februari 2024, kampuni ya Emirates Group inayomilikiwa na Serikali ya UAE ilitoa nafasi 100 za ajira ya udereva kwa watanzania wenye sifa za kufanya kazi katika kampuni yake tanzu ya Amani Taxi-Sole Proprietorship LLC iliyopo Abu Dhabi. Taratibu zinaendelea kuhakikisha kuwa nafasi hizo zinajazwa mapema iwezekanavyo, ambapo Kitengo cha Huduma za Ajira (TaESA) kwa kushirikiana na Kamishna wa Kazi Zanzibar na kampuni ya uwakala wa ajira binafsi ya A&F Company wameanza kufanya mchujo wa watanzania wenye sifa na kukamilisha taratibu nyinginezo za ajira. Ni matarajio yangu kuwa, watanzania wenye sifa na vigezo stahiki watapatikana kwa wakati ili kuepuka fursa hizo kuelekezwa katika nchi nyingine na hatimaye nchi yetu kuzikosa.

79. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba 2023 Wizara iliratibu na kushiriki kwenye kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Uholanzi lililofanyika The Hague, Uholazi. Miongoni mwa mafanikio ya kongamano hilo ni kusainiwa kwa mkataba kati ya Wizara ya Fedha kwa niaba ya Serikali na shirika la Invest International la Uholanzi wa msaada wa kiasi cha Euro milioni 30 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kudhibiti mafuriko kwenye bonde la Mto Msimbazi. Utekelezaji wa mradi huo siyo tu



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa January Makamba akihutubia wakati wa Kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Uholanzi lililofanyika The Hague, Uholanzi mwezi Novemba 2023



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masahariki Mhe.January Makamba akishuhudia zoezi la kubadilishana Hati za Makubaliano ya Ushirikiano (MoUs) kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzani (TIC), Bw. Gilead Teri na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Biashara kati ya Uholanzi na Afrika, Bi. Rosmarijn Fens kongamano la biashara lililofanyika jijini The Hague, Uholanzi Mwezi Novemba, 2023

utasaidia kudhibiti mafuriko katika bonde hilo, bali pia utaongeza hali ya usalama wa mali na maisha ya wakazi wanaoishi kando ya bonde. Vilevile, utachagiza ongezeko la shughuli za kiuchumi katika bonde hilo na maeneo ya pembezoni.

80. **Mheshimiwa Spika**, pia mwezi Novemba 2023 Wizara ilifanya ziara ya kikazi nchini Ufaransa ambapo pamoja na kukutana na viongozi wa kiserikali, Wizara ilitumia nafasi hiyo kukutana na shirikisho la makampuni makubwa nchini Ufaransa lijulikanalo kama MEDEF, ambapo Wizara ilitumia nafasi hii kuwavutia kufanya ziara nchini Tanzania ili kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi zetu mbili. Kwa hivi sasa, kundi la makampuni kutoka shirikisho hilo wako nchini Tanzania kwa ziara ya siku tano ambapo wanatembelea Tanzania Bara na Zanzibar ili kujionea fursa za biashara na uwekezaji.

81. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba 2023, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 20 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika na Nordic uliofanyika Algiers, Algeria. Mkutano huo ulijadili masuala kuhusu kuimarisha ushirikiano kati ya nchi za Afrika na Nordic ndani ya taasisi za kimataifa; kukuza ujasiriamali na uwekezaji; na kuhamasisha mazungumzo na maridhiano katika utatuzi wa migogoro. Mkutano uliazimia kuendeleza ushirikiano katika masuala ya amani, usalama, biashara na uwekezaji, mageuzi katika Umoja wa Mataifa hususani Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili kuharakisha utatuzi wa changamoto za ulinzi na usalama duniani. Vilevile, uliazimia kuundwa kwa chombo kitakachofuatilia utekelezaji wa maazimio ya mikutano ya mawaziri wa mambo ya nje wa nchi za Afrika na Nordic na kutoa taarifa.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa January Makamba ambaye ni mwenyekiti wa mjadala uliohusu ushirikiano wa biashara na uwekezaji kati ya nchi za Afrika na Nordic akiongoza kikao wakati wa Mkutano wa 20 wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika na Nordic uliofanyika Jijini Algiers, Algeria mwezi Oktoba 2023. Kushoto ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Finland, Mheshimiwa Lauri Tierala.

82. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mkataba wa kuanzisha majadiliano ya kibiashara kati ya Tanzania na Marekani. Mkataba huo unalenga kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Marekani hususani kukuza ushirikiano kibiashara na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kampuni kutoka nchi zote mbili. Utekelezaji wa mkataba huo utahusisha kufanyika kwa majadiliano ya mara kwa mara baina ya wawakilishi wa pande mbili kutoka sekta za umma na binafsi kuhusu masuala ya biashara na uwekezaji, hatua ambayo inatarajiwa kutoa fursa kwa nchi yetu kuongeza kiwango cha bidhaa inazouza Marekani na kuvutia kampuni za Marekani kuwekeza hapa nchini.

83. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mpango kazi wa utekelezaji wa hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Makumbusho ya Taifa la Tanzania na Mamlaka ya Makumbusho ya Oman. Kusainiwa kwa mpango kazi huo ni kiashiria cha kuanza utekelezaji wa hati hiyo ya makubaliano iliyosainiwa mwaka 2022, ambapo utekelezaji wake utahusisha:

i. Ujenzi wa jengo jipya la makumbusho pamoja na ukarabati wa jengo la sasa la makumbusho jijini Dar es Salaam;

ii. Kuandaa maonesho ndani ya makumbusho ya Beit al Amini iliyopo Mnazi Mmoja pamoja na ukarabati wa jengo la Makumbusho ya Kijibweni Zanzibar;

iii. Mamlaka zote mbili kushirikiana katika kutafsiri nyaraka zilizohifadhiwa kwenye makumbusho ya Taifa; na

iv. Mamlaka zote mbili kushirikiana katika kuandaa maonesho ya malikale na makumbusho.

**84. Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tayari timu ya wataalamu kutoka Oman imewasili nchini kwa ajili ya kuchukua sampuli ya udongo katika eneo litakapojengwa jengo jipya la makumbusho jijini Dar es Salaam. Aidha, taratibu za kuipatia timu hiyo ya wataalamu ramani ya jengo husika zinaendelea.

**85. Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Zambia ambapo pamoja na mambo mengine, ziara hiyo ilifanikisha kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi baina ya nchi zetu mbili. Kupitia ziara hiyo, viongozi wetu wawili walikubaliana kuondoa vikwazo vya kibiashara vilivyopo baina ya nchi zetu mbili, ikiwemo changamoto wanazopata madereva wa magari ya mizigo yanayotoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitia Zambia. Katika ziara hiyo, viongozi wa nchi zetu mbili walikubaliana kuhusu mpango mkakati wa kuimarisha uendeshaji wa reli wa TAZARA, na upanuzi wa bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA). Pia, katika ziara hiyo, kulifanyika kongamano ya biashara na uwekezaji la Tanzania na Zambia ambapo wafanyabiashara wa nchi zetu mbili walipata fursa ya kujadiliana mikakati ya pamoja ya kukuza ushirikiano kwa manufaa ya nchi zetu mbili.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya India, Mhe. Narendra Modi alipowasili katika Jengo Maalum la kupokelea Wageni wa Kitaifa Hyderabad House lililopo New Delhi wakati wa ziara ya Kitaifa nchini India Mwezi Oktoba 2023

86. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Rais nchini India ambapo pamoja na mambo mengine, ziara hiyo ilifanikisha upanikanaji wa fursa za masoko ya bidhaa za kilimo hasa mbaazi na choroko za wakulima wa Tanzania kwenye soko la India. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alikutana na Waziri Mkuu wa India, Mheshimiwa Nahendra Modi, na kumuomba aridhie kutoa fursa kwenye soko la India kupokea hadi tani 200,000 za mbaazi kutoka Tanzania ili kumuinua mkulima wa Tanzania.

87. **Mheshimwa Spika,** sambamba na ziara hiyo, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Kongamano la Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na India lililofanyika mjini New Delhi, India, likiwa sehemu ya ziara ya Mheshimiwa Rais nchini India. Kongamano hilo lililofunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais limeongeza nguvu ya ushirikiano kati ya nchi zetu katika sekta mbali mbali hasa sekta za viwanda, elimu, afya, biashara, na sekta nyingine za kiuchumi. Kufuatia Kongamano hili na mikutano aliyofanya Mheshimiwa Rais na baadhi ya wawekezaji nchini India, kampuni ya Mahindra & Mahindra imeamua kufanya tathmini ili iweze kufungua kiwanda cha kuunganisha matreka (assembly plant) hapa Tanzania. Vile vile, hospitali ya Apollo pia imeamua kurejea mazungumzo na mifuko ya hifadhi ya jamii ili waweza kufungua tawi lao hapa Tanzania.

88. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Agosti 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 30 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi wa Serikali ya UAE. Fedha hizo zitagharamia mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu kilometa 167 kutoka Benaco, Ngara hadi Kyaka, Bukoba pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Kyaka Mkoani Kagera. Kukamilika kwa mradi huo kutaimarisha hali ya upatikanaji umeme katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuunganisha Mkoa wa Kagera na gridi ya Taifa, ambapo kwa sasa unategemea umeme kutoka nchi ya Uganda.

89. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Julai 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha Mkutano wa Kumi wa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na India uliofanyika Dar es Salaam. Kupitia mkutano huo, pande mbili ziliazimia kuendeleza ushirikiano katika sekta za maji, elimu, afya, biashara uchukuzi, TEHAMA, kilimo, nishati, uchumi wa buluu, madini na uwekezaji.

90. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania na India zina uhusiano mzuri wa kibiashara, hivyo mkutano huu ulitoa fursa kwa nchi hizi mbili kuweka mikakati ya kuongeza ujazo wa biashara kati yao. Mikakati hiyo inajumuisha kuratibu ziara za wafanyabiashara kutoka pande zote; kuandaa maonesho ya biashara na ushiriki wa pamoja katika maonesho hayo; kuimarisha uwezo wa bandari kuhudumia mizigo; kuharakisha uwekaji saini mkataba wa uwili wa uwekezaji; na uendelezaji wa wajasiliamali wadogo na wakati, matumizi ya kanda maalumu za mauzo ya nje na kanda maalum za kiuchumi kwa ajili ya kuongeza thamani bidhaa.

91. **Mheshimiwa Spika,** mikakati mingine ni kukuza ushirikiano wa kibiashara baina ya sekta binafsi za Tanzania na India; kubadilishana taarifa na uzoefu kuhusu sera za viwanda, tafiti na uzalishaji; na kuendelea kuruhusu bidhaa za kilimo za Tanzania kuingia katika soko la India ikiwemo mbaazi na jamii ya kunde yenye mahitaji makubwa nchini humo. Wizara inaendelea kushirikiana na taasisi za umma na binafsi kuhakikisha kunakuwepo na utekelezaji wa maeneo yaliyokubaliwa yenye tija ili kunufaika na fursa za kiuchumi kwa maendeleo ya taifa.

92. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Julai 2023, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa fedha za msaada wa kibajeti kiasi cha Euro milioni 46.11 kutoka Umoja wa Ulaya. Fedha hizo

zitatumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele nchini katika sekta ya fedha, uchumi wa buluu, nishati, kilimo, maendeleo ya kidigitali na mipango miji. Aidha, fedha hizo ni sehemu ya programu ya ushirikiano ijulikanayo kama Multi Annual Indicative Program inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2021 hadi 2027 chini ya Makubaliano ya Ushirikiano wa Maendeleo kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya.

93. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha kuanzishwa kwa huduma ya safari za moja kwa moja za ndege za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kutoka Dar es Salaam kwenda Dubai, UAE. Napenda kulijulisha Bunge lako kuwa safari hizo zimeanza terehe 31 Machi 2024. Kuanza kwa safari hizo kumeongeza mtandao wa safari za ATCL kimataifa na kuchochea ukuaji wa biashara na utalii kati ya Tanzania na UAE.

94. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha mikutano ya tume za pamoja za kudumu za ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine kwa dhumuni la kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika kipindi hiki ilifanyika mikutano miwili (2) ya tume za kudumu za pamoja za ushirikiano kati ya Tanzania na Algeria Agosti 2023. Nchi yetu imepewa nafasi soko la maziwa ya unga nchini Algeria (powdered milk) na kuanzisha makubaliano ya biashara ya nishati.

## 3.2.3 Kusimamia na Kuratibu masuala ya uhusiano baina ya Jamhuri ya Muungano waTanzania na nchi nyingine

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ushirikiano na uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii kama ifuatavyo:

### 3.2.3.1 Uratibu na Ushiriki katika Ziara za Kitaifa na Kikazi za Viongozi wa Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi

96. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, Wizara iliratibu ziara za kitaifa za viongozi wakuu wa kitaifa nje ya nchi kufuatia mialiko ya wakuu wa mataifa mengine pamoja na ziara za kikazi, kushiriki mikutano ya kikanda na kimataifa kama ifuatavyo:

i. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa kushiriki Mkutano Mkuu wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika uliofanyika Paris, Ufaransa mwezi Mei 2024.

ii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uturuki mwezi Aprili, 2024;

iii. Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda kushiriki Maadhimisho ya Miaka 30 ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda ya Mwaka 1994 mwezi Aprili 2024;

iv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ethiopia kushiriki Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mwezi Februari 2024;

v. Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Namibia kushiriki mazishi ya Mheshimiwa Dkt. Hage Geingob aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Namibia mwezi Februari, 2024;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na mwenyeji wake Rais wa Ufaransa, Mheshimiwa Emmanuel Macron mara baada ya kuwasili Ikulu ya Paris mwezi Mei 2024. Mheshimiwa Rais Samia alikuwa nchini humo kwa ajili ya kushiriki Mkutano Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika ambapo pia alikuwa Mwenyetiki Mwenza katika Mkutano huo.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwasili katika ukumbi wa Mikutano jijini Addis Ababa, Ethiopia kuhudhuria Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali Afrika, uliofanyika Mwezi Feburuari, 2024



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Mtendaji Mkuu wa Clean Cooking Alliance Bi. Dymphna Van der Lans Jijini Paris Ufaransa. Mheshimiwa Rais Samia alikuwa nchini Ufaransa kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika uliofanyika mwezi Mei 2024 ambapo pia alikuwa Mwenyetiki Mwenza katika Mkutano huo.

vi. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Norway mwezi Februari, 2024;

vii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Holy See (Vatican) mwezi Februari, 2024;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Rais wa Namibia Hayati Dkt. Hage Geingob katika uwanja wa Michezo wa Uhuru Jijini Windhoek mwezi Februari, 2024



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa katika ziara ya Kitaifa nchini Norway Mwezi Februari 2024

viii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Indonesia mwezi Januari, 2024;

ix. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kushiriki Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi mwezi Januari, 2024;

x. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Saudi Arabia kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Saudi Arabia mwezi Novemba, 2023;

xi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Morocco kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Uwekezaji barani Afrika mwezi Novemba, 2023;

xii. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Angola kushiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC, mwezi Novemba, 2023;

xiii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda kushiriki Mkutano wa Baraza la Wasafiri na Utalii Duniani mwezi Novemba, 2023;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, akiangalia kitu katika kitabu na Baba Mtakatifu Francis alipokuwa katika ziara ya Kitaifa nchini Vatican mwezi Februari, 2024




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akizungumza kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai katika Falme za Kiarabu mwezi Desemba, 2023



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali waliohudhuria Mkutano wa Saudi




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu wa Barbados Mhe. Mia Mottley wa pili (kushoto), Rais wa Comoros Azali Assoumani wa tatu kutoka (kulia), Rais wa Sierra Leone Mhe. Julius Maada wa tatu kutoka (kushoto) pamoja na Waziri Mkuu wa Rwanda Mhe. Dkt. Edouard Ngirente wa kwanza (kulia) kwenye moja ya mijadala kuhusu fursa mbalimbali za Uwekezaji Barani Afrika wakati wa mkutano wa Jukwaa la

xiv. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini India mwezi Oktoba, 2023;

xv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia kushiriki Sherehe za Maadhimisho ya miaka 57 ya uhuru wa Jamhuri ya Zambia mwezi Oktoba, 2023;

xvi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Wanachama wa Umoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na kushiriki Mkutano Maalum kwa ajili ya kujadili hali ya usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) mwezi Septemba, 2023;

xvii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Afrika Kusini kushiriki Mkutano wa 15 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za BRICS mwezi Agosti, 2023;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akizungumza kwenye Mkutano wa Kimataifa wa 23 wa Baraza la Utalii Duniani (WTTC) uliofanyika jijini Kigali, Rwanda Mwezi Novemba, 2023



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Jamhuri ya India Mheshimiwa Droupadi Murmu (kushoto) pamoja na Waziri Mkuu wa India Mheshimiwa Narendra Modi (kulia) alipowasili Ikulu ya Rashtrapati Bhawan jijini New Delhi, India Mwezi Oktoba, 2023



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Zambia Mheshimiwa Hakainde Hichilema alipowasili nchini humo kwa Ziara ya Kitaifa na kushiriki Sherehe za Maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Jamhuri ya Zambia, Mwezi Oktoba, 2023

xviii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Malawi kushiriki Sherehe za Maadhimisho ya miaka 59 ya uhuru wa Jamhuri ya Malawi mwezi Julai, 2023;

xix. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Zambia kushiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Utatu wa Asasi mbili za SADC, mwezi Machi 2024;




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa China Mheshimiwa Xi Jinping wakati wa Mkutano wa BRICS uliofanyika Jijini Johannesburg, Afrika Kusini Mwezi Agosti, 2023

xx. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Hungary kushiriki Jukwaa la 5 la Idadi ya Watu mwezi Septemba, 2023;

xxi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Marekani kushiriki Kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Septemba, 2023;

xxii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Angola kushiriki Mkutano wa 43 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika mwezi Agosti, 2023;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akihutubia Viongozi pamoja na Wananchi wa Malawi wakati wa maadhimisho ya miaka 59 ya Uhuru wa Nchi hiyo kwenye Sherehe zilizofanyika katika uwanja wa Taifa wa Bingu uliopo jijini Lilongwe, mwezi Julai, 2023



Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia Kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kikao hicho kilifanyika jijini New York mwezi Septemba, 2023.

xxiii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kushiriki Sherehe za uapisho wa Mheshimiwa Rais Felix Tshisekedi Januari, 2024;

xxiv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Qatar kushiriki Jukwaa la 21 la Doha mwezi Desemba 2023;

xxv. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Kenya kushiriki Sherehe za Maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Jamhuri ya Kenya mwezi Desemba, 2023;

xxvi. Ziara ya kikazi ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Cuba kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Kundi la Nchi 77 na China (G77 + China) mwezi Septemba 2023;




Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar akizungumza na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa Qatar Mheshimiwa Mohammed bin Ali Al Manai pembezoni mwa Jukwaa la Doha mwezi Desemba, 2023.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kundi la G77+ China jijini Havana Cuba tarehe 15 Septemba 2023

xxvii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda kushiriki Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali zisizofungamana na Upande Wowote mwezi Januari 2024;

xxviii. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Madagascar kushiriki Sherehe za Uapisho wa Rais wa Jamhuri ya Madagascar, Mheshimiwa Andry Rajoelina mwezi Disemba 2023;

xxix. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Italia kushiriki Mkutano wa Jukwaa la Kimataifa la Chakula Duniani mwezi Oktoba, 2023;

xxx. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Urusi kushiriki Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Shirikisho la Urusi na Afrika mwezi Julai, 2023;



Waziri Mkuu wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa akimpongeza Rais wa Madagascar Mheshimiwa Andry Rajoelina baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Nchi hiyo kwenye hafla iliyofanyika Mwezi Desemba, 2023

xxxi. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya kushiriki mazishi ya aliyekuwa Mkuu wa Majeshi wa Kenya, Jenerali Francis Ogalla mwezi Aprili, 2024;

xxxii. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Botswana kushiriki Mjadala wa Viongozi kuhusu Utekelezaji wa Ajenda ya Maendeleo ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2063 (Presidential Dialogue on the Implementation of AU Agenda 2063) na Tamasha la Kusi mwezi Disemba 2023; na

xxxiii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda kushiriki Sherehe za Maadhimisho ya miaka 61 ya uhuru wa Jamhuri ya Uganda mwezi Oktoba, 2023.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akimpa zawadi Rais wa Jamhuri ya Uganda Mheshimiwa Yoweri Museveni alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Uganda mwezi Oktoba 2023

### 3.2.3.2 Mafanikio ya kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa.

97. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa, ziara hizo zilikuwa na mafanikio kwa Taifa letu kiuchumi, kisiasa na kijamii kama ambavyo imeainishwa kwa uchache hapo chini.

i. Tanzania na Ufaransa zilikubaliana kuimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo na kusaini Tamko la Paris linalobainisha dhimira ya nchi zetu kuimarisha ushirikiano katika nyanja za nishati na hatua za

kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; maji, uchumi wa buluu, uendelezaji wa miundombinu ya usafiri; kilimo; usawa wa kijinsia na uendelezaji wa wanawake kiuchumi;

ii. Tanzania na Uturuki zilikubaliana kuimarisha ushirikiano uliopo katika sekta za Elimu, Afya, Uchukuzi, Ulinzi na Usalama, Utalii na Biashara na Uwekezaji na kuongeza maeneo mapya ya ushirikiano ambayo ni Kilimo, Uchumi wa Buluu na Sanaa na utamaduni. Katika hatua ya kusimamia ushirikiano huo ilikubalika kuanzishwa kwa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kama jukwaa maalumu la kujadili maeneo ya ushirikano baina ya pande mbili. Aidha, kupitia ziara hiyo hati sita (6) za Makubaliano zilisainiwa zinazohusu ushirikiano katika Nyanja za elimu ya juu, diaspora, uwekezaji na utunzaji wa kumbukumbu Serikalini;

iii. Tanzania na Norway zilisaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ya kilimo na usalama wa chakula na Utafiti. Kupitia makubaliano hayo Serikali itanufaika katika kujenga uwezo wa kufanya tafiti za kilimo, kuongeza thamani katika mnyororo wa bidhaa za kilimo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Norway (Norwegian University of Life Sciences) vitanufaika na programu za kubadilishana na mafunzo na wakufunzi. Vilevile, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) itanufaika na ufadhili wa kiasi cha Krona za Norway milioni 9.9, ambazo ni takribani shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kuendeleza elimu na utafiti kuhusu afya ya udongo na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

iv. Tanzania na Vatican na zilikubaliana kuimarisha na kupanua wigo katika maeneo mahsusi ya ushirikiano kwenye sekta za afya, elimu na kilimo. Aidha, ilikubaliwa uwepo wa Hati ya Makubaliano (Memorandum of Understanding) baina ya pande mbili itakayoongoza utekelezaji wa miradi na programu katika maeneo mahsusi ya ushirikiano kupitia ufadhili wa Vatican hapa nchini;

v. Taasisi ya Utafiti wa Uchumi wa Kibaiolojia ya Norway na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania zilisaini Mkataba wa Ruzuku ya Kroner za Norway milioni 9.9, sawa na shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya kuendeleza elimu na utafiti kuhusu masuala ya afya ya udongo na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

vi. Tanzania na Indonesia zilisaini Hati saba (7) za Makubaliano na Barua moja (1) ya kusudio vinavyogusa ushirikiano katika sekta za kilimo, madini, elimu na uchumi wa buluu, Uwekezaji, Diplomasia na Biashara. Vilevile, Tanzania na Indonesia zilikubaliana kuwa na mkutano wa kwanza wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ambapo Tanzania itakuwa mwenyeji wa kikao hicho kwa tarehe zitakazokubaliwa na pande mbili;

vii. Tanzania na Indonesia zilikubaliana kuanza majadiliano kuhusu kuanzisha eneo huru la biashara kati ya nchi hizi mbili ambapo baadhi ya bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine zitapewa upendeleo na kupunguziwa ushuru wa forodha zinapoingia katika soko;

viii. Tanzania itakuwa mwenyeji wa mkutano wa Tume ya Pamoja na Ushirikiano katika sekta ya kilimo (Indonesia-Tanzania Joint Agriculture Cooperation Committee - JACC) iliyoanzishwa mwaka 2011 kwa lengo la kukuza ushirikiano kati ya nchi ya Tanzania na Indonesia katika sekta ya kilimo. Maeneo ya ushirikiano yanayoratibiwa chini ya Tume hiyo ni pamoja na kujenga uwezo, kufanya tafiti za pamoja za kilimo na kupanua soko

la bidhaa za kilimo;

ix. Tanzania na Indonesia zilikubaliana kuanzisha Baraza la Biashara kati ya nchi hizi mbili litakalokuwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kuhamasisha ukuaji wa biashara;

x. Tanzania na Indonesia zilikubaliana kuangalia uwezekano wa kuanzisha safari za moja kwa moja za ndege kati ya nchi hizi mbili kwa lengo la kukuza biashara, utalii, uwekezaji na uhusiano mwingine wa kiuchumi;

xi. Mwezi Septemba 2023, Tanzania ilipokea ujumbe wa wafanyabishara na wawekezaji kutoka kampuni tatu (3) za Urusi waliofanya ziara nchini kwa lengo la kukutana na kampuni binafsi na taasisi zinazosimamia sekta za nishati na kilimo. Kampuni hizo ni Agrovent LLC, Unigreen Energy LLC na Seises. Kipaumbele cha wafanyabiashara na wawekezaji hao ilikuwa ni kuangalia fursa za biashara na uwekezaji katika nishati jadidifu, usindikaji wa mazao ya kilimo na kilimo cha mbogamboga na matunda (horticulture);

xii. Tanzania na India zilisaini Hati 18 za Makubaliano ya ushirikiano, ambapo Mkataba mmoja (1) na Hati za Makubaliano Tisa (9) zilisainiwa na Taasisi za Serikali na Hati za Makubaliano nane (8) baina ya Sekta Binafsi. Hati hizo zinagusa sekta za ulinzi, utamaduni, michezo, uchukuzi, mawasiliano na afya. Aidha, ushirikiano kati ya nchi hizi umepandishwa hadhi na kuwa ushirikiano wa kimkakati;

xiii. Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) zilisaini Hati tatu (3) za Makubaliano ya Ushirikiano katika Elimu, Sayansi, Teknolojia na masuala ya Ajira;

xiv. Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Wakala wa Maendeleo Zambia zilisaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika kukuza uwekezaji;

xv. Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania na Wakala wa Maendeleo Zambia zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika kukuza biashara. Kupitia makubaliano hayo, taasisi hizo zitabadilishana uzoefu na taarifa zenye lengo la kupunguza kero za kibiashara, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara, na hivyo kukuza ushirikiano wa kiuchumi;

xvi. Tanzania na Zambia zilisaini Mikataba miwili (2) ya ushirikiano katika masuala ya ulinzi na nishati na kukubaliana kuhamasisha wafanyabiashara wa Zambia kuendelea kutumia Bandari ya Dar es Salaam kupitishia mizigo yao sanjari na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha;

xvii. Tanzania na Saudi Arabia zilisaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya Ajira. Kupitia makubaliano hayo, watanzania watapata fursa za ajira katika taasisi za umma na binafsi nchini Saudi Arabia. Vilevile, Serikali ya Saudi Arabia imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa maafisa uhamiaji kutoka Idara ya Uhamiaji;

xviii. Tanzania na Malawi zilisaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika masuala ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Vilevile, zilikubaliana kuimarisha uhusiano wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha; na

xix. Tanzania na Hungary zilikubaliana kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano itakayokuwa na jukumu la kuibua maeneo mapya ya ushirikiano na kufanya ufuatiliaji wa maeneo yaliyokubaliwa.

### 3.2.3.3 Ziara za Kitaifa na Kikazi za Viongozi Wakuu kutoka Mataifa ya Nje

98. **Mheshimiwa Spika,** pia katika kipindi hiki, Wizara iliratibu ziara za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine na wawakilishi wa mashirika ya kikanda na kimataifa kutembelea Tanzania kama ifuatavyo:

i. Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Hassan Sheikh Mohamud, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia mwezi Aprili 2024;

ii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Museven, Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, Rigathi Gachagua, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mheshimiwa Gervais Ndirakobuca, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Burundi kushiriki katika Sherehe za Maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, mwezi Januari, 2024;

iii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Andrzej Duda, Rais wa Jamhuri ya Poland mwezi Februari, 2024;




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mgeni wake Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia, Mheshimiwa Dkt. Hassan Sheikh Mohamud alipowasili katika viwanja vya Ikulu wakati wa ziara yake nchini mwezi Aprili 2024



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Jamhuri ya Poland Mheshimiwa Andrzej Duda wakizungumza na Waandishi wa habari Ikulu kuelezea waliyokubaliana wakati wa mazungumzo yao yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam Mwezi Februari, 2024

iv. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Klaus Iohannes, Rais wa Jamhuri ya Romania mwezi Novemba, 2023;

v. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Frank-Walter Steinmeier, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani mwezi Oktoba, 2023;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Romania Mheshimiwa Klaus Iohannis alipowasili Ikulu Jijini Dar es Salaam Mwezi Novemba 2023



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akifurahia jambo na mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani Mhe. Dkt. Frank-Walter Steinmeier wakati wa Mkutano wa Wafanyabiashara wa Tanzania na Ujerumani uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2023

vi. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, Mheshimiwa Dkt. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mheshimiwa Macky Salli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Senegal kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Mfumo wa Chakula Afrika, mwezi Septemba, 2023;

vii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Joko Widodo, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Indonesia mwezi Agosti, 2023;

viii. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Katalin Novák, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Hungary mwezi Julai, 2023;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa na Mgeni wake aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Indonesia Mheshimiwa Joko Widodo wakati Wimbo wa Taifa wa Tanzania na Indonesia ulipopigwa katika Viwanja vya Ikulu Jijini Dar es Salaam katika mapokezi rasmi ya Mheshimiwa Widodo yaliyofanyika Mwezi Agosti, 2023

ix. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Filipe Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Dkt. Lazarus Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi, Mheshimiwa Andry Rajoelina, Rais wa Madagascar, Mheshimiwa Carlos Vila Nova, Rais wa Visiwa vya Sao Tome na Principe, Mheshimiwa Julius Maada Bio, Rais wa Jamhuri ya Sierra Leone na Mheshimiwa Mariam Chadi Talata, Makamu wa Rais wa Benin kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Rasilimaliwatu, Julai, 2023;

x. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Salvador Valdés Mesa, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Cuba mwezi Januari, 2024;



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan (wan ne kushoto) akiwa na Marais walioshiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Rasilimali Watu. Kutoka kushoto ni Rais wa Kenya, Mheshimiwa William Ruto, Rais wa Malawi, Mheshimiwa Lazarous Chakwera, Rais wa Msumbiji Mheshimiwa Filipe  Nyusi, Rais wa Madagascar, Mheshimiwa  Andry Rajoelina, Rais wa Sao Tome na Principe, Mheshimiwa Carlos Vila Nova na Rais wa Sierra Leone, Mheshimiwa Julius Maada Bio



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Cuba, Mheshimiwa Salvador Valdés Mesa akisalimiana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam Mwezi Januari,2024

xi. Ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Dkt. Abiy Ahmed Ali, Waziri Mkuu wa Shirikisho la Kidemokrasia la Jamhuri ya Ethiopia mwezi Machi, 2024;

xii. Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Liu Guozhong, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China mwezi Januari, 2024; na

xiii. Ziara ya kikazi ya bwana Bo Li, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Julai, 2023.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. January Makamba (Mb.) akisalimiana na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Mhe. Dkt. Abiy Ahmed Ali alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa ziara ya Kitaifa nchini Mwezi February 2024



Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China, Mhe. Liu Guozhong akisalimia wadau mbalimbali waliofika kumpokea alipowasili nchini kwa ziara ya kikazi ya siku tatu Mwezi Januari, 2024

### 3.2.3.4 Mafanikio yaliyopatikana katika ziara hizo

**99. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kupitia ziara hizo ni pamoja na

i. Tanzania na Ethiopia zilikubaliana kuimarisha uhusiano wa kiuchumi hususan katika sekta za kilimo, mifugo, viwanda, biashara, uwekezaji, utalii, TEHAMA, madini, ulinzi na usalama. Aidha, nchi hizi mbili zilisaini Hati tatu (3) za Makubaliano ya ushirikiano kwenye kilimo, nishati, sanaa na utamaduni. Utekelezaji wa hati hizo utahusisha kubadilishana maarifa, ujuzi, uzoefu na taarifa katika sekta husika kwa manufaa ya mataifa yote;

ii. Tanzania na Romania zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika kukabiliana na maafa na majanga ya kibinadamu; na Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika tafiti za kilimo. Makubaliano hayo yataiwezesha nchi yetu kunufaika na fursa za kubadilishana uzoefu, ujuzi na maarifa katika sekta husika. Serikali ya Romania pia ilitangaza kurejesha mpango wa ufadhili wa masomo 'scholarship' kwa wanafunzi kutoka Tanzania kusoma katika vyuo na taasisi za elimu ya juu vya nchi hiyo ambapo kwa mwaka 2024/25 itatoa ufadhili kwa wanafunzi kumi (10). Vilevile, Tanzania na Romania zilikubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano katika sekta za elimu, biashara na uwekezaji, utalii, afya, madini, nishati safi, kilimo na usalama wa chakula;

iii. Tanzania na Ujerumani ziliazimia kuendeleza ushirikiano katika masuala ya afya; maji; matumizi endelevu ya maliasili na uhifadhi mazingira; usawa wa kijinsia, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora; uchumi, biashara na uwekezaji. Vilevile, pande mbili zilikubaliana kuanzisha majadiliano kuhusu urejeshwaji wa masalia ya utamaduni, malikale na mabaki ya miili ya binadamu yaliyohifadhiwa kwenye makumbusho nchini Ujerumani;

iv. Tanzania na Poland ziliazimia kuendelea kudumisha uhusiano na ushirikiano uliopo katika sekta za elimu, nishati na gesi, madini ya kimkakati, usalama wa mtandao, ulinzi na usalama, uchumi wa buluu, utalii na usafirishaji. Vilevile, nchi hizi zimekubaliana kuanzisha majadiliano yatakayowezesha kusainiwa kwa Mikataba na hati za Makubaliano katika masuala ya anga; kodi; elimu ya juu. Sambamba na hayo, Tanzania na Poland zimekubaliana kuanzisha mashauriano ya kisiasa (Political consulations) yatakayotoa fursa ya kujadili maeneo ya ushirikiano na kuhuisha mikakati ya kutelekeza agenda za ushirikiano wa maendeleo ili kufikia malengo tarajiwa kwa muda muafaka;

v. Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Artimesa cha Cuba vilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika masuala ya ufundishaji na utafiti wa kilimo. Vilevile, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ya Tanzania (TMDA) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ya Cuba zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika masuala ya usimamizi na udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Kusainiwa kwa hati hizo kutasaidia taasisi zetu kunufaika na fursa za kubadilishana uzoefu na maarifa katika sekta za kilimo na afya;

vi. Tanzania na Cuba ziliazimia kuongeza wigo na maeneo ya ushirikiano katika uendelezaji wa vivutio vya utalii hususan Mji Mkongwe Zanzibar na Bagamoyo na kutafuta masoko mapya ya bidhaa zinazozalishwa na kiwanda cha Tanzania Biotech Product Limited kinachozalisha viuwadudu vya Malaria na viuwatilifu kwa ajili ya kilimo;

vii. Tanzania na Hungary zilisaini Hati ya Makubaliano ya ufadhili wa masomo itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia 2023 hadi 2026 na tayari utekelezaji wake umeanza kwa kutangaza nafasi hizo za masomo. Hati hiyo inatoa nafasi kwa wanafunzi 30 kutoka Tanzania kusoma katika Vyuo na Taasisi za elimu ya juu nchini Hungary. Aidha, Tanzania na Hungary zilikubaliana kuanzisha Tume

ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kwa ajili ya kuimarisha uhusiano uliopo na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano;

viii. Tanzania na Indonesia zilisaini Hati saba (7) za Makubaliano ya Ushirikiano katika sekta za afya, uhamiaji, nishati, na madini;


ix. Serikali ya China iliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kufufua reli ya TAZARA kupitia ushirikiano wa utatu baina ya Tanzania, Zambia na China. Vilevile, Serikali ya China itahamasisha kampuni na sekta binafsi kutoka nchini humo kuwekeza Tanzania na kurahisisha bidhaa za Tanzania kuingia katika soko la nchi hiyo kupitia utaratibu wa msamaha wa ushuru wa forodha wa hadi asilimia 98; na

x. Serikali ya China imeridhia kutekeleza mradi wa ujenzi na upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na vilevile ipo katika hatua za mwisho za kutoa mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 pamoja na mtandao wa mawasiliano vijijini.

100. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyoainishwa hapo juu, Serikali ya Tanzania ilisaini Jumla ya Mikataba na Hati za Makubaliano 78 baina ya Tanzania na nchi zifuatazo; Algeria, Indonesia, Falme za Kiarabu, Zambia, India, Noway, Urusi, Uganda, Cuba, Hungary, Malawi, Korea ya Kusini, Italia, Saudi Arabia, Japan, Angola, Rwanda, Marekani, Romania, Uturuki, Ivory Coast Ethiopia na Ufaransa. Hati za Makubaliano na mikataba iliyoingiwa ipo katika nyanja na sekta mbalimbali zikiwemo Nishati (11), Ulinzi (6), Mazingira na Hali ya Hewa (1), Usafirishaji (3), Uhamiaji (2), Afya (5), Mifugo (2), Uchumi wa Buluu (1), Elimu (11), Utamaduni, Sanaa na Michezo (5), Kilimo (4), Mawasiliano na Teknologia ya Habari (3), Madini (2), Biashara (3), Uwekezaji (5), Diplomasia (5), Kazi na Ajira (3), Maendeleo ya Jamii (1), Usanifu na Mipango Miji (2) na Madawa ya Kulevya (1) na Uhifadhi wa Nyaraka (1) na Ushirikiano wa Jumla (1). Orodha ya Mikataba na Hati hizo ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.1

101. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na jukumu la kuratibu utiaji saini na Ufuatiliaji wa karibu utekelezaji wa Mikataba na Hati

**Chati Na.1: Mchanganuo wa Hati za Mikataba na Makubaliano yaliyoingiwa na Serikali**



za Makubaliano zilizosainiwa kwa dhumuni la kuhakikisha kuwa nchi yetu inanufaika ipasavyo na fursa zilizoibuliwa katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano yaliyoainishwa katika Mikataba husika. Ili kufanikisha hilo, Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa mfumo maalum wa kielektroniki utakaorahisisha uratibu na upatikanaji wa haraka wa taarifa za utekelezaji wa mikataba zinazosainiwa ili kuepusha kasumba ya kusaini Mikataba na Hati za Makubaliano na kutotimiza utekelezaji wake hadi zinafikia ukomo.

## 3.2.4 Ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa

102. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika majadiliano ya kikanda na kimataifa kwenye jumuiya na mashirika ambayo nchi yetu ni mwanachama, hususan Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.Vilevile, imeratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa itifaki, maazimio na programu za maendeleo za jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa kama inavyobainishwa hapa chini.

### 3.2.4.1 Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

103. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Wizara iliendelea kusimamia na kuongoza ushiriki wa Tanzania katika hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kulinda na kutetea maslahi ya nchi yetu.

104. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba 2023, Wizara ilisimamia na kuratibu kwa mafanikio ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 23 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo uliridhia ombi la Jamhuri ya Shirikisho la Somalia kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya nchi hiyo kukidhi vigezo vya kuwa mwanachama. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, mwezi Desemba 2023 Somalia ilisaini Mkataba wa kujiunga na Jumuiya na kuwasilisha Hati ya Kuridhia kujiunga na uanachama kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya mwezi Machi 2024.

105. **Mheshimiwa Spika,** kujiunga kwa Somalia kunaifanya Jumuiya kuwa na nchi wanachama nane (8) ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Shirikisho la Jamhuri ya Somalia. Kukua kwa Jumuiya hiyo ambayo ina watu takriban milioni 450 kunaongeza wigo wa soko na fursa za kiuchumi na uwekezaji, sanjari na kuchangia katika kuimarisha hali ya ulinzi na usalama miongoni mwa nchi wanachama. Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nawahimiza Watanzania wenzangu kuchangamkia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano huu.

106. **Mheshimiwa Spika,** sanjari na hayo, Mkutano, uliridhia mabadiliko katika uchangiaji wa bajeti ya Jumuiya ambapo nchi wanachama zitachangia kwa usawa asilimia 65 ya bajeti ya Jumuiya na asilimia 35 itachangiwa kwa uwiano kulingana na tathmini ya Pato la Taifa la kila nchi mwanachama. Mabadiliko hayo yanalenga kupunguza changamoto za kifedha katika Jumuiya ambazo zimekuwa zikikwamisha utekelezaji wa majukumu ya vyombo na taasisi zake.

107. **Mheshimiwa Spika,** Wakuu wa Nchi walilielekeza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuharakisha marekebisho ya Ibara ya 137 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 inayohusu lugha rasmi katika Jumuiya, sambamba na kuharakisha taratibu za kuanza matumizi ya

lugha ya Kiswahili na Kifaransa kama lugha rasmi za Jumuiya.

108. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, wakati wa Mkutano huo, Mheshimiwa Salva Kiir Mayardit Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini alikabidhiwa Uenyekiti wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) itakuwa mnukuu (rapporteur) wa vikao na mikutano ya Jumuiya kwa kipindi hicho.

109. **Mheshimiwa Spika,** katika mkutano huo washindi wa shindano la insha kwa wanafunzi wa shule za Sekondari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2022/2023 walipokea tuzo zao. Wanafunzi hao walishindanishwa kuandika Insha kuhusu "Maendeleo ya miundombinu ya barabara na reli yanavyoweza kuchangia maendeleo ya mahusiano ya kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki". Ninayofuraha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, katika tuzo za mwaka 2023 mwanafunzi Idrisa Mussa wa Shule ya Sekondari Azania alikuwa mshindi wa pili kikanda.

110. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu na kufanikisha kufanyika kwa Mikutano mbalimbali ya Mabaraza ya Kisekta ya Mawaziri wa Ushirikiano katika Ulinzi, Baraza la Kisekta la Uratibu wa Sera za Nje, Baraza la Kisekta la Amani na Usalama na Mabaraza ya Pamoja ya Kisekta ya Ushirikiano katika Ulinzi, Amani na Uslama na Uratibu wa Sera za Nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mikutano hii ilijadili na kutoa mapendekezo ya namna ya kuimarisha masuala ya ulinzi na amani. Aidha, Mabaraza hayo yalipokea na kujadili taarifa za utekelezaji kuhusu jitihada za kukabiliana na mapambano dhidi ya ugaidi, uharamia, usafirishaji haramu wa binadamu, na biashara haramu ya dawa za kulevya. Kupitia mikutano hii, imewezesha kuanza kwa mchakato wa kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Jumuiya cha Kuratibu Mapambano dhidi ya ugaidi.

111. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Mazoezi ya Pamoja ya Kijeshi ya Medani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Field Training Exercise - Ushirikiano Imara). Mazoezi haya hulenga kujenga utayari kwa watalaam kukabiliana na changamoto zozote zitakazojitokeza katika Operesheni ya Kulinda Amani, Kupambana na Ugaidi, Uharamia na Kuzuia Majanga. Kwa mwaka huu zoezi limepangwa kufanyika Mjini Gako, Rwanda kuanzia tarehe 08 – 23 Juni, 2024 likifuatiwa na kikao cha tathmini (After Action Review - AAR) tarehe 24 – 26 Juni, 2024 na litashirikisha wadau kutoka vyombo vya ulinzi na usalama, Wizara/Taasisi za Serikali na Asasi zisizo za kiserikali.

### 3.2.4.1.1 Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki

112. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuongoza wadau wa ndani katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kukuza biashara, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza uwekezaji wa ndani baina ya nchi wanachama na kuendeleza viwanda.

113. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023 thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania ndani Jumuiya ya Afrika Mashariki yalikuwa Dola za Marekani bilioni 1.074 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 1.415 mwaka 2022. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na mchele, saruji, makaa ya mawe, bidhaa za petrol, mahindi, karanga na mbolea. Aidha, Tanzania ilinunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 528 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 578 kwa mwaka 2022. Kupungua kwa mauzo na manunuzi ya Tanzania ndani ya Jumuiya kunatokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi za Jumuiya kulikotokana na kudorora kwa uchumi wa dunia. Aidha, licha ya kupungua kwa biashara, Tanzania imeendelea kuwa na urari chanya wa biashara baina yake na nchi za Jumuiya.

114. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwezesha biashara, Jumuiya imeendelea kuweka mifumo ya kurahisisha biashara na kutatua migogoro ya kibiashara ndani ya Jumuiya ikiwa ni pamoja na kuanzisha programu-tumizi (application) ya simu ya kutoa taarifa za vikwazo vya biashara visivyo vya kodi. Programu hiyo imepewa jina la "NTB Reporting" ambayo imeunganishwa na mifumo mingine ya utoaji taarifa za vikwazo. Aidha, Jumuiya imeanza utaratibu wa kutoa cheti cha uasili wa bidhaa za kielektroniki, ambapo kupitia utaratibu huo Mamlaka ya Mapato Tanzania inaweza kupokea vyeti hivyo moja kwa moja kutoka mamlaka za mapato za nchi nyingine wanachama kutokana na kuunganishwa kwa mifumo ya kiforodha kupitia utaratibu wa Himaya Moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## Takwimu za Biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama 2018 - 2023

**Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Nchi za EAC (2018-2023)**

**Thamani (USD Million)**

| Nchi | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Burundi | 61.37 | 87.93 | 177.73 | 163.26 | 212.82 | 172.32 |
| Democratic Republic of Congo | 150.75 | 164.08 | 144.16 | 207.23 | 280.54 | 312.81 |
| Kenya | 227.92 | 269.88 | 230.23 | 397.22 | 381.66 | 176.52 |
| Rwanda | 107.18 | 190.92 | 205.30 | 277.80 | 262.54 | 187.99 |
| South Sudan | 1.31 | 2.03 | 3.42 | 8.95 | 13.11 | 19.24 |
| Uganda | 121.13 | 123.66 | 191.19 | 314.02 | 264.20 | 310.76 |
| **Jumla** | **669.66** | **838.51** | **952.02** | **1,368.48** | **1,414.87** | **1,179.64** |
| **WASTANI (3yrs)** | | | **2,460.19** | | | **3,962.99** |


**Manunuzi ya Bidhaa kutoka Nchi Wanachama (2018-2023)**

**Thamani ya Manunuzi (USD Million)**


| Nchi | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Burundi | 1.0 | 0.3 | 0.3 | 0.6 | 2.6 | 3.06 |
| Congo DR | 0.7 | 1.3 | 2.1 | 2.6 | 3.1 | 2.91 |
| Kenya | 245.6 | 266.5 | 253.5 | 413.0 | 426.6 | 408.89 |
| Rwanda | 1.4 | 1.5 | 2.1 | 2.2 | 3.1 | 1.38 |
| South Sudan | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.02 |
| Uganda | 52.4 | 58.6 | 77.4 | 109.6 | 142.6 | 107.32 |
| JUMLA | 301.4 | 328.2 | 335.3 | 528.0 | 578.0 | 523.6 |
| **WASTANI (3yrs)** | | | **964.9** | | | **1629.6** |
| **TOTAL TRADE** | **971.06** | **1,166.72** | **1,287.31** | **1,896.52** | **1,992.87** | **1,703.22** |

*Mauzo ya bidhaa kama yalivyowasilishwa kwa Graph bar*

Mauzo ya Bidhaa 2018- 2023




Manunuzi 2018- 2023





115. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kuendelea kwa jitihada za kurahisisha biashara ndani ya Jumuiya, idadi ya vikwazo vya biashara visivyo vya kodi baina ya Tanzania na nchi nyingine wanachama imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2021/22 vikwazo vinavyoihusu Tanzania vilikuwa 14, mwaka 2022/23 vilipungua hadi kufikia saba (7); na mwezi Februari 2024 vikwazo hivyo vimebaki vinne (4)

116. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuimarika kwa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya imekuwa ikipokea maombi mbalimbali kutoka nchi zilizo nje ya Jumuiya ya kufanya majadiliano ya kuanzisha eneo huru la biashara baina ya Jumuiya na nchi hizo. Hadi kufikia sasa, Nchi ambazo tayari zimeomba kuwa na majadiliano na Jumuiya ni Uturuki, China, Singapore, Uingereza, Pakistan, Serbia na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Jedwali la Vikwazo Vya Biashara 2023/2024

| Na. | Nchi | Idadi ya vikwazo | Vikwazo vilivyotatuliwa | Vikwazo Vilivyosalia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uganda | 5 | 2 | 3 |
| 2 | Tanzania | 4 | 0 | 4 |
| 3 | Sudani Kusini | 1 | 0 | 1 |
| 4 | Kenya | 1 | 0 | 1 |
| 5 | Burundi | 0 | 0 | 0 |
| 6 | Rwanda | 0 | 0 | 0 |
| 7 | DRC | 0 | 0 | 0 |
| 8 | Somalia | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **11** | **2** | **9** |




117. **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha Jumuiya inalinda maslahi yake ya ukuaji wa uchumi na sekta za uzalishaji, katika kipindi hiki Jumuiya imepitisha Andiko la Kisera (policy paper) la kuongoza nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadiliana Mikataba ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara na nchi nyingine zilizo nje ya Jumuiya. Lengo la Andiko hilo ni kutoa mwongozo kwa Jumuiya katika majadiliano na nchi zilizo nje ya Jumuiya.

### 3.2.4.1.2 Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

118. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kufikia umoja wa fedha ifikapo mwaka 2031 kwa mujibu wa mpango muelekeo mpya uliowekwa na nchi wanachama. Awali nchi wanachama zilikuwa zikitekeleza mpango muelekeo wa miaka 10 unaofikia ukomo mwaka

2024. Nchi Wanachama ziliamua kuufanyia marekebisho Mpango huo katika Mkutano wa 43 wa Baraza la Mawaziri baada ya kupokea tathmini ya hali halisi ya nchi wanachama kufikia vigezo vya kuoanisha uchumi mpana (macroeconomic convergence criteria).

119. **Mheshimiwa Spika,** tathmini ilibaini nchi Wanachama kushindwa kufikia kwa ukamilifu vigezo vya uoanishaji wa uchumi mpana kulingana na mpango kazi kutokana na athari za UVIKO-19 na miundombinu duni ya kiuchumi. Nchi nne (Tanzania, Kenya, Rwanda na Uganda) ndizo zilifikisha lengo la kuwa na mfumuko wa bei usiozidi 8% mwaka 2021. Burundi na Sudan Kusini hazikuweza kukidhi kigezo hicho. Vilevile nchi tatu (Tanzania, Rwanda na Kenya) ndizo zilikidhi kigezo cha kuwa na akiba ya fedha za kigeni ya kutosheleza mahitaji ya miezi minne na nusu (4.5months). Burundi, Sudan Kusini na Uganda hazikufikia kigezo hicho. Aidha, Nchi tatu (Tanzania, Sudan Kusini na Uganda) ndio zilifikia kigezo cha kiwango cha juu cha deni la Taifa kisichozidi asilimia 50. Nchi za Burundi, Rwanda na Kenya hazikuweza kukidhi kigezo hicho. Mwisho, hakuna nchi iliyoweza kukidhi kigezo cha Kiwango cha Juu cha Nakisi ya Bajeti ikijumuisha misaada kisichozidi asilimia 3 ya pato la taifa katika Jedwali Na.3

120. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tayari nchi Wanachama zimekamilisha maandalizi ya sheria za kuanzisha taasisi zitakazosimamia Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Taasisi hizo ni Taasisi ya Fedha ya Afrika Mashariki (East African Monetary Institute–EAMI) ambayo baada ya kukamilisha kazi yake itabadilika na kuwa Benki Kuu ya Jumuiya (The East African Central Bank); Taasisi ya Takwimu ya Afrika Mashariki (East African Statistics Bureau); Kamisheni ya Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Matakwa ya Itifaki ya Umoja wa Fedha (East African Surveillance, Compliance and Enforcement Commission); na Kamisheni ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki (East African Financial Services Commission). Hatua inayoendelea hivi sasa ni Jumuiya kukubaliana nchi mwenyeji (host country) wa kila taasisi.

Jedwali Na. 3 Ufikiaji wa vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana

| Na. | Kigezo | Burundi | Kenya | Rwanda | Sudan Kusini | Tanzania | Uganda |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfumuko wa bei usiozidi 8% | x | v | v | x | v | v |
| 2. | Nakisi ya Bajeti ikijumuisha misaada kisichozidi asilimia 3 ya pato la taifa | x | x | x | x | x | x |
| 3. | kiwango cha juu cha deni la Taifa kisichozidi asilimia 50 ya Pato la Taifa | x | x | x | v | v | v |
| 4. | Akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza miezi minne | x | v | v | x | v | x |

*Chanzo: Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Masuala ya Uchumi.*

Tanbihi: x-Nchi haijafikia kigezo
v-Nchi imefikia kigezo

#### 3.2.4.1.3 Utekelezaji wa Miradi na Programu za Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii

121. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa mkopo wa masharti nafuu wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 12 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa upande wa Tanzania kwa ajili ya kugharamia awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha kutoa Huduma kwa Pamoja (OSBP) cha Manyovu/ Mugina kilichopo katika mpaka wa Tanzania na Burundi. Serikali imeendeleza jitihada za kutekeleza azma hii ambapo mwezi Novemba 2023 ilitoa fedha za nyongeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.3 ili kufikia Dola za Marekani milioni 20.3 zinazohitajika kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo hicho. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni ya kutangaza zabuni ili kupata mkandarasi mwenye sifa za kutekeleza ujenzi wa Kituo hicho.

122. **Mheshimiwa Spika,** matarajio ni kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa OSBP ya Manyovu/Mugina ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo hicho kutachochea ukuaji wa biashara na kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na Burundi pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Aidha, Wizara inaendelea na uratibu wa upatikanaji wa fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 11.7 kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa kituo hicho. Jumla ya gharama zinazohitajika kukamilisha mradi huo ni Dola za Marekani milioni 32.

123. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa eneo moja la mtandao wa mawasiliano la Afrika Mashariki (East Africa One Area Network) unaolenga kupunguza gharama za mawasiliano kwa njia ya simu za mkononi miongoni mwa wakazi wa nchi wanachama. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tangu Tanzania imeanza utekelezaji wa mpango huo mwezi Agosti 2023, gharama zinazotozwa kwa mawasiliano ya simu za mkononi za kuzuru (roaming) kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimepungua kutoka Dola za Marekani 0.25 hadi kufikia kiwango kisichozidi Dola za Marekani 0.07 kwa dakika kwa gharama za jumla na Dola za Marekani 0.10 kwa dakika kwa gharama za rejareja. Vilevile, gharama kwa mpokeaji wa simu iliyounganishwa (International Direct Dialling - IDD) kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeondolewa.

124. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaendelea kupata umeme wa uhakika, Wizara imeendelea kuratibu ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuongeza matumizi ya rasilimali za Majishirikishi kwa maendeleo ya pamoja. Mradi wa kufua umeme wa maji wa Rusumo, wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 80 umekamilika mwezi Machi, 2024 kwa asilimia 100. Nchi zinazonufaika na umeme huo kwa kuchukua Megawati 27 kila nchi ni Tanzania, Burundi na Rwanda ambazo pia ni washirika katika mradi huu.

125. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Jamhuri ya Rwanda na Jamhuri ya Uganda zinakusudia kutekeleza Mradi wa Kufua Umeme wa Nsongezi (39MW) kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera ambayo ni majishirikishi. Katika kipindi hiki, rasimu ya Hati ya Makubaliano (MoU) ili kuweka msingi wa utekelezaji wa Mradi huo imeandaliwa.

126. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Julai 2023, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa fedha kiasi cha Euro milioni 5.3 kutoka Umoja wa Ulaya na Serikali ya Shirikisho la Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo (KfW). Fedha hizo ni sehemu ya fedha zilizotolewa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa msaada na Washirika hao wa Maendeleo jumla ya Euro milioni 38.9

(Serikali ya Ujerumaini imetoa Euro milioni 30 na Umoja wa Ulaya umetoa Euro milioni 8.9) ili kutekeleza Programu ya Pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria inayoratibiwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ya Afrika Mashariki (Lake Victoria Basin Integrated Water Resources Management Programme). Fedha hizo (Euro milioni 5.3) zitaiwezesha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kukarabati na kupanua mtandao wa majitaka kwa kilomita zaidi ya 14.4 ambapo utaunganisha kaya zaidi ya 1,600 kwenye mtandao huo.

127. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Septemba 2023, Wizara iliongoza na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Maadhimisho ya 12 ya Siku ya Mara yaliyofanyika Mugumu, Serengeti kwa lengo la kuhimiza ushirikiano wa kikanda katika uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Maadhimisho hayo yaliyoandaliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Kenya yalijumuisha upandaji wa miti zaidi ya 20,000, uwekaji wa vigingi na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi Ikolojia ya Bonde la Mto Mara.

128. **Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na mafanikio ya maadhimisho ya Siku ya Mara, mwezi Februari 2024, Mkutano wa 22 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria uliridhia tarehe 29 Novemba ya kila mwaka kuwa Siku ya Ziwa Victoria. Lengo la kuadhimisha siku hiyo ni kuhamasisha utunzaji na uhifadhi wa Ziwa Victoria kwa maendeleo endelevu. Hivyo, maadhimisho ya kwanza ya Siku ya Ziwa Victoria yatafanyika Tanzania tarehe 29 Novemba 2024.

129. **Mheshimiwa Spika,** mwezi Julai 2023, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa fursa za mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi wa afya ili kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kuboresha huduma za afya nchini. Watumishi 22, kati yao 12 kutoka Tanzania Bara na 10 kutoka Zanzibar wamepata ufadhili wa masomo ya shahada za uzamili katika taaluma za usimamizi wa mnyororo wa ugavi wa afya, uchambuzi na ithibati ya ubora wa dawa kwenye Chuo Kikuu cha Rwanda. Ufadhili wa Masomo hayp umetolewa na Kituo cha Umahiri wa Chanjo, Kinga na Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi wa Afya cha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

130. **Mheshimiwa Spika,** Kufikia mwezi Machi 2024, watumishi 104, kati yao 63 kutoka Tanzania Bara na 41 kutoka Zanzibar wamepata mafunzo ya muda mfupi ya usimamizi wa mnyororo wa ugavi, dawa, chanjo na maeneo mengine ya tiba na afya. Ufadhili wa watumishi wote (wa muda mrefu na muda mfupi) umetolewa na Kituo cha Umahiri wa Chanjo, Kinga na Mnyororo wa Thamani cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichopo nchini Rwanda. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu, nawasihi wanufaika wa mafunzo hayo kutumia vizuri ujuzi walioupata katika kuboresha utendaji kazi katika maeneo yao.

### 3.2.4.1.4 Bunge la Afrika Mashariki (EALA)

131. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kufanikisha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Katika kipindi hiki, Bunge lilijadili na kupitisha maazimio kadhaa ambayo yanaimarisha Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kama ifuatavyo:-

i. Azimio la Bunge kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi Wanachama kuharakisha mchakato wa urazinishaji wa Kodi za ndani ili kukuza biashara na uwekezaji katika Jumuiya kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa EAC, Itifaki ya Soko la Pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge. Kimsingi Azimio hili, linasisitiza umuhimu wa kuondoa changamoto za viwango tofauti vya kodi za ndani;



ii. Azimio la Bunge la kumpongeza Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

iii. Azimio la Bunge kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuzielekeza Nchi Wanachama kufanya utafiti kuhusu - Matumizi ya viumbe vilivyobadilishwa Vinasaba – GMOs) pamoja kuandaa mdahalo miongoni mwa Nchi Wanachama kwa ajili ya kujadili masuala yote yanayohusiana na GMOs ili kufikia msimamo/muafaka wa pamoja utakaoleta maelewano na ambao utapelekea uwianishaji wa Sera na Sheria za Nchi Wanachama;

iv. Azimio la Bunge kuhusu kupendekeza kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kupiga marufuku ya uuzwaji wa ngozi mbichi nje ya Jumuiya na uingizaji wa bidhaa za ngozi katika Jumuiya; na

v. Azimio la Bunge la Kuzipongeza Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu ya Mataifa ya Afrika Mwaka 2027.

### 3.2.4.2 Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

132. **Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajia kuwa Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC (Organ) kuanzia Agosti 2024 hadi Agosti 2025. Hatua hii inafuatia uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti ajaye wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC katika Mkutano wa 43 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika mwezi Agosti 2023 jijini Luanda, Angola.

133. **Mheshimiwa Spika,** Uteuzi huo utaendelea kuimarisha ushawishi wa Tanzania katika ukanda wa SADC, hususan kwenye nyanja za amani, ulinzi na usalama ikizingatiwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa Waasisi wa SADC walioshiriki kwa hali na mali katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Aidha, nafasi hiyo italeta manufaa ya kiuchumi, ikiwemo kuongezeka kwa pato la taifa kupitia utalii wa mikutano.

134. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo pia uliidhinisha Itifaki ya Kazi na Ajira ya SADC, kutoa Tamko la Kuharakisha Hatua za Kutokomeza janga la UKIMWI kwa Afya ya Umma katika kanda ya SADC na kuidhinisha Mpango Mkuu wa Gesi wa Kanda (Regional Gas Master Plan, 2023-2038). Aidha, ulipokea taarifa ya ujenzi na uwekaji wa Sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Jengo la Amani na Usalama lililopo Makao Makuu ya Umoja wa Afrika, Addis Ababa, Ethiopia.

135. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika mwezi Novemba 2023 jijini Luanda, Angola. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliolenga kujadili hali ya Ulinzi na Usalama katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Katika Mkutano huo, bajeti ya kupeleka Misheni ya Ulinzi wa Amani Mashariki mwa DRC (SAMIDRC) iliidhinishwa. Ni matarajio ya Serikali kuwa Misheni hiyo itachagiza juhudi za kuimarisha hali ya usalama Mashariki mwa DRC na hivyo kuwezesha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kutekeleza shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa maendeleo ya nchi hiyo.

136. **Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwa SADC, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kujitolea na kuitikia wito wa kuchangia juhudi za kuimarisha amani, usalama, na utulivu wa kisiasa katika kanda. Jitihada hizo zinaakisi misingi ya Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania inayohusu kustawisha amani, usalama na ujirani mwema. Hivyo, kwa kuzingatia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa SADC (Mutual Defence Pact) na kufuatia maombi ya Serikali ya DRC, Tanzania iliungana na nchi wanachama nyingine za SADC kupeleka Misheni ya Ulinzi wa Amani mashariki mwa DRC (SAMIDRC) Desemba 2023. Lengo la misheni hiyo ni kuisaidia Serikali ya DRC kurejesha hali ya usalama mashariki mwa nchi hiyo.

137. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuchangia katika Misheni za Ulinzi wa Amani, Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi za kidiplomasia za kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro wa DRC kupitia Mchakato ya Nairobi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ule wa Luanda uliochini ya Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) kwa baraka za Umoja wa Afrika.

138. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Misheni za Uangalizi wa Uchaguzi ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SEOM) katika chaguzi kuu za Jamhuri ya Madagascar na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zilizofanyika Novemba na Desemba,2023 mtawalia.

139. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Madagascar, Mheshimiwa Andry Rajoelina wa Chama cha Young Malagasies Determined alitangazwa kuwa mshindi wa Kiti cha Urais kwa muhula wa pili kwa kupata jumla ya kura 2,858,947 sawa na asilimia 58.69 na kuapishwa tarehe 16 Desemba 2023. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Sherehe hizo.

140. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa DRC, Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi alitetea nafasi ya urais kwa kupata jumla ya kura 13,215,366 sawa na asilimia 73 ya kura zilizopigwa. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Sherehe za Uapisho zilizofanyika tarehe 20 Januari, 2024.

141. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kushiriki katika Uzinduzi wa Sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere uliofanyika tarehe 18 Februari, 2024 katika Kituo cha Amani na Usalama cha Mwalimu Julius Nyerere kilichopo katika jengo la Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa, Ethiopia.

142. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya SADC, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC) walishiriki katika Uzinduzi wa sanamu hiyo uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU). Ujenzi wa sanamu hiyo ni kielelezo cha kuuenzi mchango thabiti wa Baba wa Taifa na Nchi kwa ujumla katika juhudi za ukombozi wa nchi za Afrika hususan zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara. Nchi wanachama wa SADC ziligharamia ujenzi wa sanamu hiyo ulioanza Agosti 2022 na kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023.

143. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Utatu wa Asasi Mbili za SADC (Double Troika), Nchi zinazochangia Vikosi vya Walinda Amani katika Misheni ya Ulinzi wa Amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (SAMIDRC) na zinazochangia Vikosi vya Walinda Amani katika Misheni ya Ulinzi wa Amani nchini Msumbiji (SAMIM) uliofanyika tarehe 23 Machi, 2024. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo ulipokea taarifa kuhusu hali ya usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Misheni ya SAMIDRC na Mpango wa Kupunguza na Kuondoa vikosi vya SAMIM nchini Msumbiji ifikapo tarehe 15 Julai 2024.

144. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanikisha ushiriki wa Tanzania katika Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) lililofanyika Luanda, Angola mwezi Machi, 2024. Baraza hilo liliitishwa mahsusi kwa lengo la kupitisha bajeti ya SADC kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Maamuzi yaliyofikiwa ni pamoja na agizo kwa Sekretarieti ya SADC kutafuta rasilimali fedha kutoka kwenye michango ya nchi wanachama na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kukamilisha zoezi la kuthibitisha ubora wa nyaraka muhimu za SADC zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili; na Sekretarieti kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Mpango Mkakati Elekezi wa Maendeleo wa Kanda (RISDP) kwa kipindi cha 2020 – 2030.

145. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Baraza hilo liliziagiza Nchi Wanachama kufanya tathmini ya kitaifa kuhusiana na athari ya ukame na mafuriko ili kubaini afua zinazohitajika, kuharakisha utekelezaji wa programu ya mbolea ya kikanda na kuanzisha taratibu za kuwa na hifadhi za nafaka za Kikanda; na uchapishaji wa Juzuu tisa (9) za chapisho la Brigedia Generali (Mst.) Hashim Mbita katika lugha ya Kiswahili kukamilika ifikapo mwezi Julai 2024.

146. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu athari za El Nino uliofanyika tarehe 20 Mei, 2024 kwa njia ya mtandao. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania kushiriki Mkutano huo kwa niaba ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pamoja na masuala mengine, Mkutano uliazimia kuweka hatua za pamoja kukabiliana na athari za El Nino ikiwemo Kuzindua Mpango wa Kanda wa kuhamasisha Misaada ya Kibinadamu (SADC Regional Humanitarian Appeal) wenye thamani ya takriban Dola za

Marekani Bilioni 5.5. Mpango huo unalenga kuchagiza upatikanaji wa rasilimali kutoka kwa wadau wa kitaifa, kanda na kimataifa ili kuzisaidia nchi wanachama kukabiliana na athari za ukame na mafuriko yaliyosababishwa na mvua za El Nino. Katika Mkutano huo, Ofisi ya Uratibu wa Misaada (Office for Coordination of Humanitarian Affairs – OCHA) na Shirika la Chakula Duniani (FAO) ziliahidi kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 33 milioni na 10 milioni mtawalia katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango husika.

### 3.2.4.3 Jumuiya ya Nchi za Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA)

**147. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 23 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Nchi zilizopo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) uliofanyika mwezi Oktoba 2023, jijini Colombo, Sri Lanka. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo uliidhinisha bajeti ya IORA kwa mwaka 2024 ya kiasi cha Dola za Marekani 503,714.

**148. Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo pia uliridhia pendekezo la Tanzania kuhusu kufanya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya ya IORA kwa kuzingatia utaratibu wa mzunguko wa Nchi Wanachama kuanzia mwaka 2025. Nchi ya Mauritius imekuwa ikitekeleza jukumu la ukaguzi wa hesabu za IORA kwa kipindi chote tangu kuanzishwa kwake. Lengo la mabadiliko hayo ni kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji wa Jumuiya hiyo.

**149. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Maadhimisho ya miaka 27 ya Siku ya Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association – IORA Day) yaliyofanyika tarehe 2 Machi, 2024, Mauritius. Maadhimisho hayo hufanyika kila mwaka na kutoa fursa kwa nchi wanachama kujadili na kutathmini utekelezaji wa shughuli za IORA na pia yanawezesha nchi hizo kuonesha bidhaa mbalimbali wanazozalisha. Katika Maonesho hayo, Tanzania ilipata fursa ya kutangaza bidhaa inazozalisha ikiwemo korosho, chai, asali, kahawa na khanga.

### 3.2.4.4 Umoja wa Afrika (AU)

**150. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari 2024, Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo, pamoja na masuala mengine, ulipitisha Mpango wa Pili wa Miaka 10 wa Utekelezaji wa Ajenda ya 2063 ya Maendeleo ya Afrika pamoja na kuridhia kaulimbiu ya Umoja wa Afrika kwa mwaka 2024 isemayo, "Kumuelimisha Mwafrika kwa ajili ya Karne ya 21 Kujenga mifumo imara na stahimilivu kwa ajili ya kutoa elimu bora inayofaa Barani Afrika".

**151. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa kaulimbiu hiyo utahusisha Serikali za nchi wanachama kuchukua hatua thabiti katika kutekeleza, pamoja na mambo mengine, masuala yafuatayo:

i. Kuboresha taaluma ya ufundishaji ili kuhakikisha ubora na ufanisi katika ngazi zote za elimu sanjari na kuongeza upatikanaji wa elimu bora kwa kujenga, kukarabati na kutunza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kutekeleza sera zitakazozingatia masuala ya afya na kuhakikisha kunakuwepo na mazingira wezeshi ya kujifunzia;

ii. Kutumia fursa ya TEHAMA katika kuboresha upatikanaji wa elimu bora na kuimarisha usimamizi wa mifumo ya elimu na mafunzo, kupanua elimu ya mafunzo ya ufundi (amali) sambamba na kuharakisha utekelezaji wa mikakati inayolenga kuboresha usawa wa kijinsia katika elimu;

iii. Kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu na ujuzi stahiki ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaomaliza masomo katika ngazi zote sanjari na kurazinisha (harmonise) mipango ya elimu ya kitaifa na kikanda kupitia mtangamano; na

iv. Kuhamasisha masomo ya sayansi kwa lengo la kujenga utamaduni wa kupenda masomo hayo miongoni mwa vijana sanjari na kuboresha tafiti na ubunifu katika ngazi ya elimu ya kati na elimu ya juu.

152. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo ulipokea na kupitisha Azimio la Dar es Salaam kuhusu Rasilimali Watu. Aidha, ulimpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake katika juhudi za uendelezaji rasilimali watu barani Afrika.

153. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari 2024 uliichagua Tanzania kuhudumu kwa muhula wa pili Ujumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2026 ikiwakilisha nchi zilizo kwenye Kanda ya Mashariki ya Afrika. Nafasi hiyo ni fursa muhimu kwa Tanzania kuendeleza uongozi na ushawishi katika jitihada za kudumisha amani na kusuluhisha migogoro kwa njia ya amani Barani Afrika.

154. **Mheshimiwa Spika,** Nitumie fursa hii pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Mei 2024, Tanzania ni Mwenyekiti wa Baraza hilo. Katika kipindi hiki, nchi yetu imepata heshima ya kuwa mwenyeji wa Maadhimisho ya Miaka 20 ya Baraza hilo, ambapo tarehe 25 Mei 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mgeni rasmi katika kilele cha Maadhimisho hayo.

155. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Wanachama wa Umoja wa Afrika kuhusu Tabianchi (Africa Climate Summit) uliofanyika mwezi Septemba 2023 jijini Nairobi, Kenya. Mkutano huo uliridhia Azimio la Nairobi kuhusu Ukuaji wa Uchumi wa Kijani na Suluhu ya Ugharamiaji Tabianchi (Nairobi Declaration on Green Growth and Climate Finance Solutions). Miongoni mwa masuala yaliyokubaliwa na nchi wanachama wa AU kwenye Azimio hilo ni:

i. Kuitaka Jumuiya ya Kimataifa hususani nchi zilizoendelea kuchukua hatua za haraka katika kutekeleza Mkataba wa Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2015;

ii. Kuhimiza mageuzi katika mfumo wa kidunia wa ugharamiaji wa programu na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (global climate finance architecture) ili kutoa unafuu kwa nchi za Afrika kunufaika na mikopo ya masharti nafuu; na

iii. Kuendelea kushawishi uanzishwaji wa masoko ya hewa ukaa kwa ajili ya kufadhili miradi ya miundombinu ya nishati jadidifu.

### 3.2.4.5 Eneo Huru la Biashara Barani Afrika

156. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuongoza wadau wa ndani katika majadiliano ya kikanda kuhusu Itifaki na makubaliano mengine ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika. Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika uliofanyika mwezi Februari 2024 jijini Addis Ababa, Ethiopia pamoja na mambo mengine ulipitisha Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara Barani Afrika.

157. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania ni kinara wa kuhamasisha wanawake na vijana katika biashara ndani ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika kutokana na mchango na umahiri wake katika kusimamia maendeleo ya kiuchumi ya wanawake. Katika kutimiza lengo la kuwezesha wanawake na vijana kushiriki kikamilifu kwenye biashara barani Afrika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alikuwa mwenyeji wa makongamano mawili ya wanawake na vijana katika biashara.

158. **Mheshimiwa Spika**, kongamano la kwanza lilifanyika Septemba, 2022 na lilijikita katika kubainisha changamoto zinazowakabili wanawake na vijana na hivyo kutotumia ipasavyo fursa za biashara zitokanazo na AfCFTA. Kongamano la Pili lilifanyika Disemba, 2023 na lililenga kutoa fursa kwa wadau kujadili majawabu ya changamoto zilizobainishwa katika kongamano la kwanza ambayo yamejumuishwa katika rasimu ya Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara ndani ya AfCFTA. Jitihada hizi za Mheshimiwa Rais na kinara wa uhamasishaji wa wanawake na vijana katika biashara Barani Afrika zimechochea kukamilika kwa rasimu ya itifaki ya Wanawake na Vijana katika biashara Barani Afrika kwa wakati na rasimu ya itifaki hiyo kupitishwa na Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika mwezi Februari, 2024.

159. **Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa Itifaki ya Wanawake na Vijana katika biashara Barani Afrika ni chachu katika kutatua changamoto zinazowakabili na hivyo kutafungua masoko katika sekta muhimu ambazo wanawake na vijana wanajishughulisha kama vile kilimo, viwanda vidogo vidogo na biashara ya huduma.

160. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Tanzania inatumia ipasavyo soko la Eneo Huru la Biashara la Afrika na kutumia fast mover advantage, Tanzania iliamua kuwa sehemu ya mpango wa majaribio wa utekelezaji wa AfCFTA unaojulikana kama Guided Trade Initiative ulioanza mwaka 2022 ili kuchagiza utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA. Tanzania imekuwa sehemu ya nchi zilizofanya vizuri zaidi kupitia mpango huu kwa kuuza bidhaa nyingi ndani ya soko la AfCFTA.

161. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki jumla ya kampuni 11 za Tanzania zimepatiwa vyeti vya uasili wa bidhaa vya AfCFTA vilivyoziwezesha kampuni hizo kuuza bidhaa kwenye nchi wanachama wa AfCFTA kupitia mpango wa majaribio. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi kupitia mpango huo ni katani, kahawa, tumbaku, viungo na karanga. Nchi ambazo bidhaa za Tanzania zimeuzwa kupitia utaratibu wa AfCFTA ni Algeria, Nigeria, Misri, Morocco na Ghana

### 3.2.5 Ushirikiano wa Kimataifa

162. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wa kimataifa ni mhimili muhimu wa Sera ya Nje ya nchi yetu. Katika mwaka 2023/2024 Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano, makongamano na majukwaa mbalimbali yanayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za kidunia. Changamoto hizo ni pamoja na magonjwa ya mlipuko kama vile UVIKO 19, migogoro na mabadiliko ya tabianchi. Wizara imedhamiria kuimarisha ushiriki na ushawishi kwenye majadiliano katika majukwaa ya kimataifa kwa kuzingatia maslahi ya nchi tukiongozwa na misingi ya Sera ya Mambo ya Nje, ukiwemo ule wa kutofungamana na upande wowote.

163. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama za Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika mwezi Desemba 2023, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Mkutano huo ulikuwa na kaulimbiu isemayo "Unite, Act, Deliver" iliyolenga kuzihamasisha Nchi Wanachama

kuungana na kutekeleza kwa pamoja sera, mipango na mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na mambo mengine, nchi wanachama zilifikia makubaliano katika masuala yafuatayo: -

i. Lengo la dunia la kuhimili mabadiliko ya tabianchi (Global Goal on Adaptation) na mwongozo wake ambao unabainisha mwelekeo ambao jumuiya ya kimataifa inapaswa kufuata ili kuwezesha jitihada za kuhimili mabadiliko ya tabianchi; na shabaha za kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha, teknolojia na kujenga uwezo stahiki wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi;

ii. Uendeshaji wa mfuko wa kukabiliana na upotevu na uharibifu (loss and damage fund) utokanao na mabadiliko ya tabianchi pamoja na uundwaji wa bodi ya ushauri ya mfuko huo, ambapo kwa mujibu wa makubaliano Benki ya Dunia itausimamia mfuko kwa kipindi cha miaka mitano (5) na Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Majanga ndiyo itakuwa Sekretarieti ya Bodi ya Ushauri. Aidha, fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni 792 zimeahidiwa kutolewa kwa ajili mfuko huo;

iii. Kukamilika kwa tathimini ya kwanza ya utekelezaji wa makubaliano ya Paris na kupitishwa kwa mchakato wa kuanza tathmini ya pili. Kwa mujibu wa tathmini ya kwanza nchi zinapaswa kupunguza uzalishaji wa gesijoto kwa asilimia 43 ifikapo mwaka 2030 ili kudhibiti joto la dunia kupanda kwa zaidi ya nyuzi joto 1.5;

iv. Nchi kuahidi kupunguza matumizi ya nishati inayotokana na mabaki ya wanyama na mimea (fossil fuels); na

v. Kukubaliana kuongeza uzalishaji wa nishati jadidifu mara tatu (3) zaidi kufikia mwaka 2030.

164. **Mheshimiwa Spika**, pembezoni mwa Mkutano wa COP28, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Programu ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Wanawake wa Afrika (African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP). Programu hiyo inalenga kusaidia wanawake Barani Afrika, hususan wanaoishi vijijini, kupunguza matumizi ya nishati zinazozalisha hewa ukaa yenye athari hasi kwa mazingira na afya zao.

165. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, utekelezaji wa Programu hii utasaidia jitihada za kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni. Shabaha ya tukio hilo la uzinduzi ilikuwa kukusanya fedha za ufadhili kutoka kwa washirika wa maendeleo, ambapo baadhi ya taasisi zikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Nishati (IEA), Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Watoto (UNICEF) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ziliahidi kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Programu hiyo.

166. **Mheshimiwa Spika,** katika mwendelezo wa suala hili, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa nchi kwenye Mkutano wa Kilele kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika (Summit on Clean Cooking in Africa), uliofanyika mwezi Mei 2024 Paris, Ufaransa. Katika Mkutano huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mwenyekiti Mwenza akiungana na Dkt. Fatih Birol, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kimataifa ya Nishati (International Energy Agency); Mhe. Jonas Gahr Støre, Waziri Mkuu wa Norway; na Dkt. Akinwumi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mkutano huo, uliokuwa na kaulimbiu isemayo Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika (Clean Cooking in Africa), ulilenga kulifanya suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia kuwa la kipaumbele

katika ajenda ya kimataifa; kuainisha hatua madhubuti za kisera zitakazoharakisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kutoa fursa ya washiriki kutoa ahadi za kifedha, sera na ubia ili kufikia azma ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

167. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa matokeo ya Mkutano huo ni pamoja na kutolewa ahadi ya fedha kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.2 kutoka kwenye sekta za umma na binfasi kwa ajili ya kushajihisha matumizi ya nishati safi ya kupikia barani Afrika. Fedha hizo ni sehemu ya kiasi cha dola za Marekani bilioni 4 zinazohitajika kila mwaka kuanzia mwaka 2024 hadi 2030 kufikia lengo la matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wote barani Afrika.

168. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo ulifanyika siku chache baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa miaka 10 (2024-2034) wenye thamani ya shilingi trilioni 4.6. Kwa muktadha huo, Mkutano ulitambua na kupongeza uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais kama kinara wa ajenda hii barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kadhalika, makundi mbalimbali ya nchi zilizoendelea, zikiwemo G20 na G7, yalithibitisha kuingiza ajenda hii kwenye maazimio ya mikutano yao, sambamba na Mkutano wa 29 wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP29).

169. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) uliofanyika mwezi Januari 2024, Davos, Uswisi. Mkutano huo, uliofanyika kwa ngazi mbalimbali, ulitoa fursa kwa viongozi na wawakilishi wa kiserikali, sekta binafsi, asasi za kiraia, wanataaluma na watafiti kujadili mada mbalimbali kuhusu changamoto za maendeleo na utatuzi wake. Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeshiriki kwenye vikao vilivyojadili namna ya kutengeneza fursa katika nchi za Afrika, hususan kwenye sekta ya kilimo kama ilivyokubaliwa na Mkutano COP28. Aidha, alishiriki kwenye mjadala kuhusu namna ya kuimarisha utawala bora ili kuhakikisha mabadiliko endelevu na ukuaji wa uchumi katika muktadha wa changamoto zinazoikabili dunia kwa sasa.

170. **Mheshimiwa Spika**, pembeni mwa mkutano huo, ujumbe wa Tanzania ulifanya mikutano ya pande mbili na wadau mbalimbali ikiwemo Taasisi ya Global Plastic Action Partnership (GPAP) ya nchini Uswisi, ambapo Serikali na Taasisi hiyo zilikubaliana kutekeleza mradi wa kudhibiti taka za plastiki jijini Dodoma, ikiwa ni pamoja na kuzichakata tena kwa matumizi mengine; na kuanzisha mpango wa kupunguza uzalishaji wa taka zenye athari zaidi kwenye maeneo ya Bahari.

171. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wanachama wa kundi la nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) uliofanyika mwezi Januari 2024, Kampala, Uganda. Katika Mkutano huo, Jamhuri ya Uganda ilipokea Uenyekiti wa kundi hilo utakaodumu kwa kipindi cha miaka mitatu (2024 - 2027). Aidha, Mkutano uliridhia ombi la Jamhuri ya Sudan Kusini kujiunga na kundi hilo; na kupongeza uamuzi wa nchi za G20, uliofikiwa katika mkutano wa mwezi Septemba 2023 wa kuupatia Umoja wa Afrika uanachama wa kudumu wa kundi hilo.

172. **Mheshimiwa Spika,** Nchi Wanachama wa NAM zilipitisha Azimio la Kampala linalojumuisha masuala mbalimbali kuhusu misimamo ya nchi za NAM, ikiwemo:

i. Kuhuisha mchango wa NAM ili uendane na nyakati za sasa katika Jumuiya ya Kimataifa

kwa kuzingatia misingi ya umoja huo ya Bandung (1955) na Belgrade (1961) kwa lengo la kuhakikisha amani, usawa na ustawi wa dunia;

ii. Kuimarisha Umoja wa Mataifa kama chombo cha msingi cha diplomasia ya ushirikiano ya kimataifa kwa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya ulinzi na usalama pamoja na kuchochea maendeleo duniani;

iii. Kupinga aina zote za ukandamizaji unaofanywa na nchi moja dhidi ya nchi nyingine katika misingi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii sanjari na kuendelea kuhimiza ushirikiano miongoni mwa nchi zinazoendelea (south-south cooperation) na ushirikiano baina ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea (north-south cooperation);

iv. Kuendelea kudai mageuzi katika mifumo ya kimataifa ya kifedha (international financing architecture) na mifumo ya kibiashara (world trading systems) ili kupunguza pengo la kiuchumi kati ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea sanjari na kuongeza mchango wa nchi zinazoendelea katika uchumi wa dunia na mnyororo wa uongezaji thamani;

v. Kuendelea kuhimiza ushirikiano katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kudhibiti magonjwa ya mlipuko, uhalifu unaovuka mipaka, uzagaaji na biashara haramu ya silaha ndogondogo na nyepesi na kulinda haki za wahamiaji; na

vi. Kuunga mkono utekelezaji wa Agenda 2030 ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango Kazi wa Addis Ababa wa mwaka 2015 kuhusu Ugharamiaji wa Sera na Vipaumbele vya Agenda hiyo.

173. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Wasafiri na Utalii Duniani (WTTC) uliofanyika mwezi Novemba 2023, Kigali, Rwanda. Mkutano huo ulijadili mchango wa Bara la Afrika katika ukuaji wa sekta ya utalii duniani; matumizi ya teknolojia ya habari na ubunifu; athari za mabadiliko ya tabianchi; na umuhimu wa mafunzo ya kujenga uwezo wa jamii kwa ajili ya kuimarisha sekta utalii.

174. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia mkutano huo, Tanzania ilijiunga rasmi kuwa mwanachama wa Baraza la WTTC na kutumia Jukwaa hilo kutangaza vivutio vyake vya utalii. Uanachama katika Baraza hilo utaiwezesha Tanzania kupata taarifa na takwimu muhimu kuhusu sekta ya utalii na kunufaika na mtandao mpana wa wadau wa sekta hiyo ikiwemo kampuni za usafirishaji na wamiliki wa hoteli.

175. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Jukwaa la Uwekezaji Afrika (Africa Investment Forum) uliofanyika mwezi Novemba 2023, Marrakech, Morocco. Kaulimbiu ya Mkutano huo ilikuwa Kufungua Minyororo ya Thamani Barani Afrika (Unlocking Africa's Value Chains).

176. **Mheshimiwa Spika,** pembezoni mwa Mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kunadi miradi 16 ya kitaifa ya maendeleo kwenye kikao cha wafadhili kilichoandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na: Ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mtwara hadi Mbambabay – Liganga/ Mchuchuma yenye urefu wa kilometa 1,000, unaokadiriwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 5.9; na Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani Zanzibar, ambao Awamu ya Kwanza inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 400.

177. **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Jukwaa la Kimataifa la Chakula Duniani uliofanyika mwezi Oktoba 2023, Roma, Italia. Mkutano huo ulikwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 78 ya uwepo wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) pamoja na Siku ya Chakula Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 16 Oktoba ya kila mwaka.

178. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mkutano huo, Tanzania ilieleza jitihada Serikali za kukuza na kuboresha sekta ya kilimo nchini kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula, kuzalisha ajira kwa vijana na kujenga uchumi stahimilivu. Vilevile, ilitoa wito kwa FAO na washirika wa maendeleo kuunga mkono juhudi hizo kwa kuongeza ufadhili wa miradi na programu zinazotekelezwa katika sekta ya kilimo na sekta mtambuka ikiwemo maji, uhifadhi wa mazingira na miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji.

179. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushindi wa Tanzania katika Uchaguzi wa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika mwezi Oktoba 2023, Luanda, Angola ambapo Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliibuka mshindi wa kiti hicho dhidi ya wagombea kutoka Malawi, Somalia na Senegal, kwa kupata kura 172 kati ya 303 zilizopigwa. Kufuatia matokeo hayo, Mheshimiwa Tulia anakuwa Rais wa 31 wa IPU na mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo.

180. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa dhati kwa ushindi kishindo ulioiletea Nchi yetu heshima kwenye medani za Kimataifa. Aidha, nikutakie kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yako ambayo bila shaka yatastawisha mahusiano na ushirikiano baina ya Mabunge huru duniani.

181. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 78 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika mwezi Septemba 2023, New York, Marekani. Kupitia kikao hicho, Tanzania ilipaza sauti na kulaani uwepo wa migogoro na vita vinavyoendelea duniani vyenye athari kwa amani, usalama, uchumi na maendeleo ya nchi zinazohusika moja kwa moja na zisizohusika na migororo hiyo, ikiwemo Tanzania.

182. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania pia ilirejea utayari wake wa kuendelea kuchangia jitihada za Umoja wa Mataifa za utatuzi wa migogoro na ulinzi wa amani duniani. Napenda nilitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Machi 2024 Tanzania ilikuwa na walinda amani 1,537 ikishika nafasi ya 11 kati ya nchi 119 zinazochangia walinda amani katika misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa.

183. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Tanzania iliutaka Umoja wa Mataifa kubaini na kulaani kwa uwazi vitendo vya uchochezi wa migogoro kote duniani, hususan barani Afrika, wenye lengo la kujinufaisha na biashara ya silaha au kujihusisha na uvunaji haramu wa rasilimali. Kwa upande mwingine, Tanzania ilieleza mafanikio yake katika kukabiliana na ugaidi na uhalifu wa kuvuka mipaka; na utekelezaji wa Agenda 2030 ya Umoja kuhusu Maendeleo Endelevu, ambapo ilisisitiza umuhimu wa Jumuiya ya Kimataifa kuongeza ufadhili na uwekezaji katika kufanikisha wa malengo hayo kwa wakati.

184. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania ilitekeleza wajibu wake wa kuwasilisha taarifa ya hiari ya mapitio ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Jukwaa la Ngazi ya Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa, lililofanyika mwezi Julai 2023, jijini New York, Marekani, ikiwa ni mara ya pili kufanya hivyo baada ya wasilisho la awali la 2019. Taarifa hiyo ilibainisha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa malengo hayo ikiwemo

kuimarisha huduma za jamii, miundombinu, mapambano dhidi ya umaskini na maradhi pamoja na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kuwasilishwa kwa taarifa hiyo ni kiashiria cha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza makubaliano ya kimataifa yanayohusu maendeleo. Vilevile, inatoa nafasi kwa nchi yetu kujadiliana na Washirika wa Maendeleo kuhusu upatikanaji wa fedha za kugharamia utelekezaji wa programu na mipango ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

185. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Kundi la Nchi 77 na China (G77+China) uliofanyika mwezi Septemba 2023, Havana, Cuba. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuzikutanisha nchi zinazoendelea kujadiliana namna bora ya kujenga ustahimilivu wa kiuchumi kupitia maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

186. **Mheshimiwa Spika,** kupitia mkutano huo, Tanzania ilieleza vipaumbele vyake ikiwa ni pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kuimarisha tafiti na kuongeza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuleta mapinduzi ya kiuchumi katika sekta za kilimo, nishati, elimu, afya, madini, maendeleo ya miundombinu, maji na mazingira. Kadhalika, Tanzania ilizisihi nchi za G77 na China kutumia uzoefu uliopatikana kutokana na changamoto za UVIKO-19, kupanda kwa bei za bidhaa, mizozo ya kisiasa na athari za mabadiliko ya tabianchi kama sababu ya kuongeza uwekezaji katika sayansi, teknolojia na ubunifu.

187. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 45 wa Kamati ya Urithi wa Dunia ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni uliofanyika mwezi Septemba 2023, jijini Riyadh, Saudi Arabia. Katika Mkutano huo, nchi wanachama zilijadili kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa mwaka 1972 na matumizi ya hazina ya urithi wa dunia. Kadhalika, Mkutano ulifanya uamuzi kuhusu maeneo yaliyomo kwenye orodha ya urithi wa dunia na kujadili hali ya uhifadhi wa maeneo hayo, ambapo Tanzania ilitetea maeneo ya Mji Mkongwe wa Zanzibar, Pori Tengefu la Selous na Bonde la Ngorongoro kuendelea kuwepo kwenye orodha ya urithi wa dunia.

188. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa nchi za BRICS (Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini) uliofanyika mwezi Agosti 2023, Johannesburg, Afrika Kusini. Mkutano huo ulilenga kujadili namna ya kuimarisha ushirikiano wenye manufaa kwa pande zote kati ya nchi za BRICS na nchi za Afrika pamoja na nchi nyingine zinazoendelea (Global South), hususan kwenye maeneo ya ukuaji wa uchumi, maendeleo, amani na ushirikiano wa kimataifa. Miongoni mwa matokeo muhimu ya mkutano huo ni tamko la BRICS la kuongeza wigo wa wanachama, ambapo Argentina, Misri, Ethiopia, Iran, Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu zilipewa uanachama. Kwa upande wake, Tanzania ilitumia mkutano huo kufanya mazungumzo ya kimkakati na viongozi kutoka nchi mbalimbali zikiwemo: China, Iran, Bangladesh na Afrika Kusini.

189. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika wa Mzunguko wa 21 wa Mfuko wa Maendeleo wa Benki ya Dunia (IDA 21 Africa Heads of State Summit) uliofanyika mwezi Aprili 2024, Nairobi, Kenya. Ushiriki wa Tanzania kwenye mkutano huo umeiwezesha nchi yetu kuwasilisha vipaumbele vyake ili kujumuishwa katika vipaumbele vya nchi za Afrika kwa lengo la kunufaika na ufadhili kupitia Mfuko huo. Aidha, kupitia Azimio la Nairobi, Wakuu wa Nchi za Afrika walipata fursa ya kutoa kauli ya pamoja kuhusu ushiriakino baina ya serikali zao na baina ya serikali zao na wabia wa maendeleo katika muktadha wa Mfuko huo.

### 3.2.6 Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (OACPS)

**190. Mheshimiwa Spika,** mwezi Desemba 2023, Wizara ilifanikisha Tanzania kusaini Mkataba wa Ubia baina ya Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (Organisation of African, Caribbean and Pacific States - OACPS) na Umoja wa Ulaya (EU), ambao utatumika kama nyenzo ya kisera na kisheria ya kuratibu uhusiano wa kiuchumi kati ya pande hizo mbili kwa kipindi cha miaka 20 ijayo.

**191. Mheshimiwa Spika,** majadiliano ya mkataba huo unaojulikana kama Mkataba wa Samoa (Samoa Agreement) yalianza mwaka 2018 na utekelezaji wake utahusisha nchi 79 za OACPS na nchi 27 za EU. Maeneo ya kipaumbele katika Mkataba huo ni masuala ya demokrasia na haki za binadamu; ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu; mabadiliko ya tabianchi; maendeleo ya jamii; amani na usalama na uhamiaji na uhamaji.

**192. Mheshimiwa Spika,** kusainiwa kwa Mkataba wa Samoa ni mwendelezo wa mikataba ya ubia kati ya nchi za OACPS na EU ambayo inalenga kuweka misingi ya biashara kati ya pande hizo kwa lengo la kupunguza umaskini katika nchi za OACPS na kuongeza ushiriki wa nchi hizo katika mnyororo wa uongezaji thamani duniani. Kabla ya Mkataba wa Samoa, pande mbili zilisaini Mkataba wa Lomé mwaka 1975 na Mkataba wa Cotonou mwaka 2000.

### 3.2.7 Uratibu wa Watanzania wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora)

**193. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa diaspora, Wizara imeendelea kushiriki katika kuweka mazingira wezeshi yakiwemo ya kisera na kisheria kama hatua muhimu ya kuchochea ushiriki wa Watanzania waishio nje ya Nchi (Tanzania Citizen Diaspora) na Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania (Tanzania Non Citizen Diaspora) katika maendeleo ya Taifa. Hatua hizi ni pamoja na kujumuisha masuala ya Diaspora katika mapitio ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 na kutoa Hadhi Maalum (Special Status) kwa Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania ili kuwapa haki na upendeleo mahsusi.

**194. Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwamko wa Diaspora katika kuchangia maendeleo ya Taifa umeendelea kuongezeka, ambapo wameendelea kuchangia katika sekta mbalimbali zikiwemo nyumba, kilimo, teknolojia, utalii, uchumi wa buluu,afya na elimu. Mathalan, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2023 uwekezaji wa Diaspora katika sekta nyumba na viwanja, kupitia Shirika la Nyumba la Taifa na kampuni za KC Land Development Plan na Orange Tanzania ulifikia shilingi bilioni 9.28 kutoka shilingi bilioni 4.4 kwa mwaka 2022. Aidha, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2023 uwekezaji wa Diaspora katika Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja (UTT-AMIS) ulikuwa shilingi bilioni 6.4 kutoka shilingi bilioni 2.5 za kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2022. Vilevile, fedha zilizotumwa nchini na Diaspora kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2023 zilikuwa Dola za Marekani milioni 751.6.

**195. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Kampuni ya Livy Africa ambayo inamilikiwa

na Diaspora imewekeza katika uzalishaji wa chokoleti (Mababu Chocolate) kwa kutumia kakao kutoka Kyela, Mbeya. Uwekezaji huu umetoa ajira kwa vijana na kuongeza kipato kwa wakulima wa zao la kakao wilayani Kyela na maeneo jirani. Aidha, Kampuni hii imeendelea kutoa elimu ya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa kwa wakulima wadogo. Vilevile, mwezi Machi 2024 Diaspora kwa kushirikiana na Taasisi ya Al- Wadood ya Oman walitoa misaada ya kijamii ikiwemo uchimbaji wa visima vya maji katika vijiji vilivyoko Wilaya za Wete na Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

196. **Mheshimiwa Spika,** serikali pia inatambua na kupongeza mchango wa Diaspora katika kuanzisha mfumo wa kifedha wa NALA unaotoa huduma ya kutuma fedha kutoka nchi 21 zilizopo Ulaya na Amerika kwenda nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania. Mfumo huu ni kielelezo cha ubunifu wa Diaspora wenye mchango muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

197. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuwashawishi Diaspora kuchangia zaidi katika maeneo haya na mengine ya kimkakati, ikiwemo rasilimaliwatu, ujuzi na teknolojia hususan akili mnemba (artificial intelligence), madini ya kimkakati, uchumi wa buluu na gesi asilia.

198. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitumie fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ipo katika hatua za kukamilisha kutoa Hadhi Maalumu (Special Status) kwa Raia wa Nchi Nyingine Wenye Asili ya Tanzania (Tanzania Non- Citizen Diaspora) ambapo itawasilisha katika Bunge hili muswada wa marekebisho madogo ya Sheria za Uhamiaji Sura ya 54 na Sheria ya Ardhi Sura ya 113 ili kuwezesha utekelezaji wake. Kutolewa kwa Hadhi hiyo kutawezesha Raia hao kunufaika na baadhi ya haki na upendeleo kutokana na asili yao. Aidha, hatua hii pia itawezesha Taifa kunufaika zaidi katika maeneo mbalimbali ya kisekta ikiwemo kupokea fedha za kigeni, ujuzi adimu, uwekezaji, kutangaza utalii, kubidhaisha Kiswahili; kuchochea fursa za Uchumi wa Buluu na manufaa mengine kwa ndugu, jamaa na marafiki.

199. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuboresha huduma katika maeneo ambayo hayahitaji mabadiliko ya sheria kwa kutoa elimu kwa umma. Maeneo hayo ni pamoja na kupata huduma za kifedha; kushiriki katika uwekezaji; uanachama katika mifuko ya hifadhi ya jamii na mifuko ya bima ya afya. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya utambuzi na wa usajili wa diaspora kidijitali (Diaspora Digital Hub) ili kuwezesha upatakanaji wa takwimu sahihi za kufanikisha maamuzi ya kisera.

200. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na juhudi nilizozitaja, Serikali itaendelea kuzihamasisha Taasisi za Umma na sekta binafsi kuanzisha Madawati Mahsusi ya kutoa Huduma kwa Diaspora ili kuboresha huduma kwa kundi hilo. Wizara inatambua na kupogenza Wizara, Idara na Taasisi za Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambazo zimeshaanzisha madawati hayo, zikiwemo: Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Taasisi nyingine ni Benki Kuu ya Tanzania (BOT); Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC), Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na Benki za biashara ikiwemo ABSA, Azania, CRDB, EXIM, EQUITY, NBC, NMB, PBZ, STANBIC na TCB.

## 3.2.8 Kuratibu Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli

**201. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu masuala ya haki na kinga kwa Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa hususan Mkataba wa Vienna kuhusu Uhusiano wa Kidiplomasia wa mwaka 1961 na Waraka Na. 2 wa Rais wa mwaka 1964 kuhusu Mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na Jumuiya ya Wanadiplomasia. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha uhusiano na Jumuiya ya Wanadiplomasia hapa nchini, Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa mashauriano kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya maendeleo. Katika kipindi hiki, Wizara iliratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho kwa Mabalozi wa nchi za Rwanda, Libya, Burundi, Ujerumani, Norway, Qatar, Saudi Arabia na Umoja wa nchi za Ulaya.

**202. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu sherehe za Mwaka mpya kwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa yaliyopo Nchini (Sherry Party). Sherehe hizi ni mahsusi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukutana na kuzungumza na Wanadiplomasia hao kwa lengo la kuukaribisha mwaka mpya, kutoa mrejesho wa masuala muhimu yaliyojiri katika utekelezaji wa diplomasia na uhusiano baina Tanzania na Nchi au Mashirika yao, kutoa dira, mwelekeo, na vipaumbele vya nchi kwa mwaka unaoanza.

**203. Mheshimiwa Spika,** kwa vipindi tofauti, nimekutana na kuzungumza na Mabalozi na Wawakilishi wa Jumuiya ya Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kujitambulisha, kuwapa taarifa na ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kisera, kubadilishana uzoefu wa masuala ya kiutendaji na kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili wanadiplomasia hapa nchini. Aidha, Mikutano hii imeiwezesha kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na nchi/mashirika ya Kimataifa.

**204. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Novemba, 2023 Serikali ya Denmark ilibatilisha Uamuzi wake wa kufunga Ubalozi wake hapa nchini kama ilivyokuwa imetangazwa hapo awali mwezi Agosti 2021, kuwa Ubalozi huo ungefungwa ifikapo mwezi Juni 2024. Uamuzi huo unafatia nchi hiyo kutambua na kuthamini kuwa Tanzania imeendelea kuwa mmoja wa washirika wake wa kihistoria na kwamba maamuzi yaliyofanyika awali hayakuwa sahihi. Napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa Wizara yangu itaendelea kuhakikisha kuwa Balozi zote na Mashirika ya kimataifa yaliyopo nchini yanaendelea kupewa ushirikiano wa karibu katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu kikamilifu.

### 3.2.8.1 Kuimarisha Utendaji Kazi wa Balozi na Konseli Kuu

**205. Mheshimiwa Spika,** sanjari na kuhakikisha mahitaji ya uendeshaji wa Balozi na Konseli Kuu za Tanzania yanalipwa kwa wakati, Wizara imeendelea kupeleka watumishi wenye sifa kuhudumu katika Balozi na Konseli Kuu. Katika mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ilipeleka Watumishi 7 katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi na kuwarejesha watumishi 7 nyumbani. Aidha, Wizara inakamilisha taratibu za kupeleka watumishi zaidi mara fedha zitakapopatikana. Kipekee, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuteua na kuwapangia vituo mabalozi.

**206. Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha tunakwenda sambamba na maono na matarajio

ya Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, mnamo mwezi Aprili mwaka huu tulifanya kikao na Mabalozi wote, Makonseli Wakuu, Wakuu wa Utawala na Fedha katika Balozi zetu zote duniani na pamoja nasi viongozi na Menejimenti ya Wizara tulifanya mkutano wa faragha huko Kibaha, Mkoani Pwani uliokuwa na azma kuu ya kujitathmini. Katika Mkutano huo ambao ulipata heshima ya kumsikiliza Mheshimiwa Rais na viongozi wengine Serikalini, tulikuwa na azma kuu ya kuzibainisha kwa pamoja changamoto zote zinazotukabili kama Wizara, majawabu ya changamoto hizo na pia kutengeneza mpango kazi wa kutuvusha katika kukabiliana na changamoto zenyewe. Nafurahi kukujulisha kuwa imekuwa ni fursa nzuri ya kujenga timu inayojitambua na inayotambua tunachopaswa kufanya katika utekelezaji wa diplomasia ya Uchumi kwa manufaa ya nchi yetu.

#### 3.2.8.2 Balozi za hapa nchini kuhamia Dodoma

**207. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Wizara imeendelea kuhamasisha balozi za mataifa mbalimbali zilizopo nchini na mashirika ya kimataifa kuhamia makao makuu ya serikali Dodoma. Napenda kulifahamisha bunge lako tukufu kuwa mpaka sasa jumla ya balozi zimefungua ofisi hizo ikiwemo uingereza, ufaransa, ujerumani, China na Mashirika ya kimataifa kama vile UNRC, UNDP, UNHCR, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UN WOMEN, FAO, WFP, WHO na IOM. Aidha, Serikali ya Ethiopia imeshaweka jiwe la msingi kwa ajili ujenzi wa ofisi ya Ubalozi na Makazi ya balozi katika eneo walilotengewa Mtumba.

### 3.2.9 Diplomasia ya Umma

**208. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kupitia Diplomasia ya Umma. Diplomasia ya Umma ni mkakakati wa Wizara unaolenga kuitangaza taswira ya Tanzania kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha maoni na mitazamo ya jamii ya Watanzania kimataifa inaakisi na kuendana na Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania kwa lengo la kunufaika kiuchumi. Katika kutekeleza Diplomasia ya Umma, Wizara imejikita katika utoaji wa elimu kwa umma kwa kushajihisha na kurajamu chapa ya Tanzania kupitia Diplomasia ya Utamaduni na Michezo; Diplomasia ya Diaspora na Diplomasia ya Mikutano.

**209. Mheshimiwa Spika,** vilevile Wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa Diplomasia ya Umma ambao unajumuisha masuala yote ya elimu kwa umma na kutangaza na kuitangaza nchi kimkakati na kwa ukamilifu. Diplomasia ya Umma inatekelezwa na Wizara, Balozi za Tanzania Nje, kwa kushirikiana na taasisi za umma na binafsi. Katika kutekeleza jukumu hilo, msisitizo umeelekezwa kwenye kutangaza fursa zitokanazo na ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo ili kujiongezea kipato, maarifa na kuongeza Pato la Taifa.

**210. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano na vyombo vya habari ikiwemo vituo vya televisheni, radio na magazeti. Aidha, Wizara inatumia tovuti na mitandao ya kijamii katika utekelezaji wa Diplomasia ya Umma. Ushirikiano huu umewezesha kufikisha kwa haraka habari kwa umma kuhusu manufaa ya ziara zinazofanywa na viongozi wakuu wa kitaifa nje ya nchi na ziara za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa taasisi za kimataifa hapa nchini, mikutano ya kikanda na kimataifa inayofanyika ndani na nje ya nchi na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na watendaji wa Wizara waliopo ndani na nje ya nchi.

**211. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliendesha programu maalum za elimu kwa umma kuhusu azma ya Serikali kufanya marekebisho ya Sera

Mpya ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 katika jiji la Arusha, Dar es Salaam, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na jiji la Mwanza. Programu hizo pia zilihusisha vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii, zilizolenga kukusanya maoni ya wadau ili yatumike katika marekebisho ya Sera hiyo.

212. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendesha kampeni ya elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu fursa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kuingiza bidhaa nchini Uingereza bila kutozwa kodi. Fursa hii ni utekelezaji wa Mpango wa Serikali ya Uingereza kuruhusu nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania kuingiza bidhaa nchini humo kwa kuzingatia uasili wa bidhaa husika. Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza, Ubalozi wa Uingereza nchini na sekta binafsi ilibainisha namna wafanyabiashara wa Tanzania wanavyoweza kunufaika na Mpango huo katika kulifikia soko hilo.

213. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki kwenye Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika mwezi Julai 2023 jijini Dar es Salaam; Maonesho ya Siku ya Mara yaliyofanyika mwezi Septemba 2023 Wilaya ya Serengeti, Mara; na Maonesho ya 23 ya Jua Kali Nguvu Kazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika mwezi Desemba 2023 jijini Bujumbura. Ushiriki wa Tanzania kwenye maonesho haya ya kimataifa ni sehemu ya utekelezaji wa Diplomasia ya Umma.

214. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuelimisha na kuhabarisha umma kwa kuchapisha makala maalumu za kielektroniki na nakala ngumu za majarida, mabango na vipeperushi mbalimbali. Wizara pia ilichapisha kalenda, shajara, na vitabu vinavyoelezea kuhusu ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine ambavyo vimesambazwa kwa wadau mbalimbali wa Wizara ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

### 3.2.10 Kujengea Uwezo wa Watumishi na Kuimarisha Mazingira ya Kazi

215. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wa kazi na kuongeza morali kwa watumishi. Wizara ina jumla ya watumishi 600 wa kada mbalimbali ambapo watumishi 235 wapo kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi na watumishi 365 wapo Makao Makuu ya Wizara.

216. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Mabalozi wanne (4) ambao kati ya hao mabalozi wawili (2) wamesharipoti vituoni na wanaiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi ya Kuwait na Visiwa vya Comoro. Sambamba na teuzi hizo, Mheshimiwa Rais, aliwapangia vituo Mabalozi kumi na tano (15) katika balozi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Muscat-Oman, Ottawa - Canada, Vienna - Austria, Kigali - Rwanda, Bujumbura - Burundi, Kampala – Uganda, Doha - Qatar, Algiers - Algeria, Berlin -Ujerumani, Riyadh – Saudi Arabia, Beijing - China, Nairobi - Kenya, Pretoria - Afrika Kusini, Lilongwe – Malawi, Ankara - Uturuki na Windhoek - Namibia. Aidha, Mheshimiwa Rais aliwahamisha vituo Mabalozi watano kutoka Riyadh kwenda Paris, kutoka Kigali kwenda Cairo, kutoka Berlin kwenda Geneva, Doha kwenda Kuala Lumpur na kutoka Beijing kwenda London.

217. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuhakikisha inaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 83 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi waliohudhuria mafunzo ya muda mrefu ni 20 na mafunzo ya muda mfupi ni 63. Mafunzo haya yameongeza maarifa, ujuzi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara.

218. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile katika kipindi hicho, Wizara imepokea jumla ya watumishi thelathini na nne (34) kwa njia ya uhamisho na watumishi arobaini na nne (44) kama ajira mpya ambapo watumishi thelathini (30) ni Maafisa Mambo ya Nje Daraja la II, watumishi wanne (04) ni wa Kada ya Madereva, watumishi wawili (02) kutoka Kada ya TEHAMA, watumishi wanne (04) Kada ya Wasaidizi wa Kumbukumbu, mtumishi mmoja (01) kutoka Kada ya Katibu Mahsusi, mtumishi mmoja (01) kutoka kada ya Afisa Biashara, Mtumishi mmoja (01) kada ya Afisa Ustawi wa Jamii, mtumishi mmoja (01) kutoka kada ya Afisa Maendeleo ya Jamii na mtumishi mmoja (01) kutoka kada ya Afisa usafiri. Waajiriwa wapya hao wamepatiwa mafunzo elekezi ya awali (induction course) katika masuala mbalimbali ya kiutumishi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imefanikiwa kupata kibali cha kuajiri watumishi hamsini (50) wa Kada mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Taratibu za usaili kwa ajili ya kujaza nafasi hizo zitafanyika baada ya kupokea kibali cha utekelezaji kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

219. **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa Bajeti ya Mishahara iliyoidhinishwa kwa mwaka wa Fedha wa 2022/2023 jumla ya Watumishi 61 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo na mishahara yao kurekebishwa na watumishi saba walibadilishwa kada. Vilevile, watumishi 32 walithibitishwa kazini na watumishi 90 walithibitishwa katika vyeo walivyokuwa wamepandishwa.

## 3.2.11 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizo Chini ya Wizara

### 3.2.11.1 Uendelezaji wa Viwanja na Ukarabati wa Majengo katika Balozi za Tanzania

**220. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 17,887,608,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,400,000,000 ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo kwenye balozi zetu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Wizara imepokea na kutumia fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha shilingi 16,762,726,958.61 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,780,120,117 zimeelekezwa katika ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani kwenye balozi sita (6) za Tanzania nje ya nchi ambazo ni Beijing, Geneva, Ottawa, Brussels, Stockholm na Windhoek.

**221. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia inaendelea na ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa Tanzania Washington D.C, Marekani ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2024 mkandarasi tayari amelipwa Shilingi 2,167,437,044.65 na anaendelea na kazi.

**222. Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Wizara inaendelea na mradi wa ukarabati wa majengo manne ya Ubalozi wa Tanzania Pretoria Afrika ya Kusini. Mradi huu unahusisha jengo la ubalozi; makazi ya balozi; makazi ya mkuu wa utawala; na makazi ya mwambata utawala. Mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Dola za Marekani 523,561.43 sawa na shilingi 1,293,950,000 pamoja na kodi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 18 Julai, 2023 na hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Mkandarasi ameshalipwa Shilingi 197,847,427.96.

**223. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa Ethiopia, Wizara imesaini mkataba na Kampuni ya ALLURE CONSTRUCTION PLC ya Addis Ababa kwa ajili ya uendelezaji wa viwanja vya Ubalozi kwa gharama ya Shilingi 1,164,856,025 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Mradi huu umeanza kwa ujenzi wa uzio ili kuvilinda viwanja hivyo visivamiwe. Aidha, mkandarasi amekwishakabidhiwa eneo la ujenzi na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2024/25.

**224. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Wizara imeingia Makubaliano ya ubia na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Nairobi. Mradi huo unahusu kuendeleza kiwanja kilichopo katika eneo la Upperhill jijini Nairobi kwa kujenga majengo pacha ya ghorofa ishirini na mbili (22). Aidha, Wizara imekamilisha taratibu za kisheria za makabidhiano ya nyaraka na kuhamisha rasmi majukumu ya ujenzi wa mradi kwenda NSSF.

**225. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) imekamilisha maandalizi ya nyaraka za kisheria kwa mradi wa Ujenzi wa jengo la Kitega Uchumi Kinshasa DRC. Utekelezaji wa mradi huo unafanyika katika kiwanja cha ubalozi kilichopo mtaa wa Boulevard de 30 Juin jijini Kinshasa ambapo utahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa ishirini na tano (25).

**226. Mheshimiwa Spika,** kadhalika Wizara inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya majengo ya Wizara pamoja na vitega uchumi katika viwanja vya Serikali vilivyopo



*Mchoro wa Nje wa Majengo ya Nairobi*

**Kigali, Rwanda**



**Lilongwe, Malawi**






*Mchoro wa Jengo la Kitega Uchumi, Kinshasa DRC*

**Maputo, Msumbiji**



**Bujumbura, Burundi**



katika balozi za Tanzania Kampala, Uganda, Abuja Nigeria na Lusaka Zambia. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara inakamilisha taratibu za kupata washauri elekezi, kufanya upembuzi yakinifu, kupima udongo, kufanya marejeo ya michoro ya majengo husika, kupata vibali vya ujenzi kutoka mamlaka za miji hiyo na kuanza ujenzi.

227. **Mheshimiwa Spika,** katika mpango madhubuti wa kuendeleza viwanja na milki zake zilizopo nje ya nchi, Serikali imeunda Timu ya Wataalam, ikiwa na jukumu la kuishauri Serikali namna bora ya kuendeleza na kusimamia milki hizo nje ya nchi. Maandalizi yanaendelea ya kumpata Mshauri Elekezi mwenye uzoefu wa Kimataifa katika Masuala ya Milki atakayeandaa nyaraka mbalimbali za uwekezaji, miongozo pamoja na kuishauri Serikali namna bora ya uendelezaji wa milki hizo kulingana na maeneo ya Balozi husika. Kwa sasa timu hiyo imeendelea na ukamilishaji wa nyaraka za ununuzi ili kumpata Mshauri Elekezi huyo.

### 3.2.11.2 Uendelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Wizara Nchini

228. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika Eneo la Lakilaki Arusha kwa kuzingatia makubaliano ya Serikali na Umoja wa Afrika. Mradi huu unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya CRJE (East Africa) Limited kutoka nchini China kwa gharama ya shilingi 62,968,086,187.78 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Aidha, usimamizi wa mradi unafanywa na mshauri elekezi kampuni ya Aru Built Environment Consulting Company (ABECC) ya Chuo Kikuu Ardhi kwa gharama za shilingi 2,956,000,000 pamoja na VAT. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2023 na hadi kufikia mwezi Aprili 2024 kiasi cha shilingi 11,777,968,375.04 kimelipwa kwa mkandarasi na ujenzi na kazi ya ujenzi inaendelea.

229. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia, imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara – Mtumba (Wing A) Dodoma unaofanywa na kampuni ya M/s Corporation Sole Works Superitendent (CSWS) kwa thamani ya shilingi 21,940,486,862.12 pamoja na VAT. Vilevile, Wizara imeingia mkataba wa usimamizi wa ujenzi wa jengo hilo unaofanywa na kampuni ya M/s Aru Built Environment Consulting Company (ABECC) wenye thamani ya shilingi 595,842,770.00 pamoja na VAT. Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, Wizara imekwishamlipa mkandarasi jumla ya shilingi 13,699,545,968.69 sawa na asilimia 62.44 na utekelezaji umefikia asilimia 77.6 ya kazi zote kwenye Mkataba.

230. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS-CFR), imeendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika kampasi ya Kurasini, Dar es Salaam. Mradi unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya M/s Corporation Sole Works Superitendent (CSWS) kwa gharama ya shilingi 4,450,359,568.80 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Aidha, usimamizi wa mradi huo unafanywa na mshauri elekezi kampuni ya Aru Built Environment Consulting Company (ABECC) ya Chuo Kikuu Ardhi kwa gharama za shilingi 190,000,000.00 pamoja na VAT. Kufikia mwezi Aprili 2024 mkandarasi amekwishalipwa shilingi 838,535,851.89 na utekelezaji wa kazi unaendelea.

## 3.2.12 Kusimamia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara

**231. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kuhakikisha zinafikia malengo ya kuanzishwa kwake. Katika kipindi hiki, taasisi hizo zilitekeleza majukumu kama ifuatavyo:

### 3.2.12.1 Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)

**232. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha ni taasisi inayojiendesha kwa faida pasipo kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Majukumu ya Kituo hicho ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba na ofisi kwa taasisi na watu binafsi. Vilevile, Kituo kinatoa huduma ya afya kupitia hospitali yake.

**233. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa majukumu ya AICC unaongozwa na Sheria iliyoanzisha Kituo hicho, mpango mkakati wa miaka mitano 2022/23 - 2026/2027 pamoja na miongozo mengine ya kitaifa na kisekta. Aidha, dira na dhima ya AICC inajielekeza katika kukuza na kutangaza diplomasia na utalii wa mikutano hapa nchini, katika ukanda na duniani.

**234. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 Kituo kilipanga kukusanya mapato ya shilingi 21,030,562,179 kutoka katika vyanzo vya ndani. Hadi kufikia mwezi Aprili 2024 Kituo kilikuwa kimekusanya shilingi 18,676,445,811 sawa na asilimia 89 ya malengo. Mapato hayo yalitokana na:

i. Huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) - shilingi 10,782,248,296 kati ya lengo la shilingi 10,325,768,321 sawa na asilimia 104;

ii. Upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi - shilingi 3,960,455,545 kati ya lengo la shilingi 5,237,121,368 sawa na asilimia 76; na

iii. Huduma za hospitali - shilingi 3,933,741,970 kati ya lengo la shilingi 5,467,672,490 sawa na asilimia 72.

**235. Mheshimiwa Spika,** Kituo kimetekeleza yafuatayo katika kipindi hiki:

i. Kuhudumia mikutano 320 ya kitaifa na mikutano 23 ya kimataifa ambayo ilileta jumla ya washiriki 82,439 wa kitaifa na 22,104 wa kimataifa. Baadhi ya mikutano ya kimataifa iliyohudumiwa na Kituo ni Africa Food System Summit (AGRF), 77th Session of African Court of Human and Peoples Right na Africa Human Capital Heads of State Summit;

ii. Kutoa huduma mbalimbali za afya kwa wagonjwa 62,858 wa nje na wagonjwa 845 waliolazwa. Vilevile, Kituo kiliendesha kliniki maalum ya matibabu ya moyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na kutoa matibabu kwa wagonjwa 587;

iii. Kusimika mifumo ya kielektroniki ambayo inalenga kuongeza tija na ufanisi wa kiutendaji na pamoja na kununua vifaa vya kisasa vya TEHEMA kwa ajili ya shughuli za mikutano. Mifumo hiyo ni Hospital Management Information System(e-HMIS), PEPMIS, PIPMIS na ESS;

iv. Kuendesha mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi ikiwemo mapambano dhidi ya Ukimwi, Rushwa pamoja na magonjwa yasiyoambukiza; na

v. Kufanya ukarabati wa kawaida wa nyumba 150 za makazi katika milki za Kituo zilizopo Arusha pamoja na ukarabati wa ofisi, kumbi na hospitali.

### 3.2.12.2 Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS-CFR)

236. **Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim ni kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma ya ushauri elekezi katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia, lugha za kigeni, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani. Mafunzo yanayotolewa ni katika ngazi za cheti, stashahada, shahada, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamili. Pia, Kituo kinafundisha lugha saba za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno; na kutoa mafunzo ya muda mfupi katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani.

237. **Mheshimiwa Spika,** dira ya Kituo ni Kuwa Kituo Mahiri cha Taalumu katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa (To be a centre of excellence in national, regional and international affairs). Dhima ya Kituo ni kutoa huduma bora za kitaaluma kupitia mafunzo, utafiti na ushauri elekezi katika nyanja za diplomasia na stadi za stratejia katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa (To provide high quality scholarly services through training, research and consultancy in diplomacy and strategic studies in the context of national, regional and international affairs)

238. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Kituo kilipanga kukusanya na kutumia shilingi 7,443,205,819. Kati ya fedha hizo shilingi 3,073,950,000 ni mapato kutoka kwenye vyanzo vya ndani; na shilingi 4,369,255,819 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Ruzuku hiyo inajumuisha shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 3,169,255,819 kwa ajili ya mishahara.

239. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024, Kituo kilikuwa kimekusanya na kupokea shilingi 5,230,916,477.14, sawa asilimia 70.28 ya mapato ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,170,504,647.14 ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 70.61 ya lengo la mwaka; shilingi 2,380,411,830.00 ni ruzuku ya mishahara kutoka Serikali Kuu sawa na asilimia 75.11 ya lengo la mwaka; shilingi 680,000,000.00 ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka Serikali Kuu, sawa na asilimia 56.67 ya lengo la mwaka. Kadhalika, Kituo kilipokea shilingi 204,638,467.00 ambayo ni ruzuku ya fedha za miradi ya maendeleo.

240. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024, Kituo kimetumia shilingi 4,669,761,922.19 sawa na asilimia 89.27 ya fedha zilizokusanywa na kupokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,618,306,403.68 ni kutoka vyanzo vya ndani, sawa na asilimia 74.56 ya makusanyo kutoka vyanzo vya ndani; shilingi 2,380,411,830.00 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 100 ya fedha zilizopokelewa; na shilingi 671,043,688.51 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na asilimia 98.68 ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa. Kadhalika, Kituo kilitumia shilingi 204,638,467.00 ambayo ni ruzuku ya fedha za miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, zilizopokelewa na kutumika ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4.

241. **Mheshimiwa Spika,** Kituo kimedahili wanafunzi 1,487 katika mwaka wa masomo 2023/24 ambapo kati yao, wanafunzi 102 wanafanya mafunzo katika ngazi ya Astashahada ya Awali, 147 Astashahada, 134 Stashahada, 673 Stashahada ya Juu, 310 Shahada, 78 Stashahada ya Uzamili na 43 Shahada ya Uzamili. Aidha, Kituo kiliendesha kozi tatu za muda mfupi zilizohudhuriwa na washiriki 185 kutoka taasisi za umma na binafsi;

Jedwali Na. 4 Mapato na Matumizi ya CFR Julai 2023 – Aprili, 2024

| Na. | Maelezo | Bajeti iliyodhinishwa 2023/2024 | Mapato Halisi hadi Aprili 2024 | Asilimia (%) | Matumizi Halisi hadi 29 Aprili 2024 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | C | D | D/C | E | E/D |
| 1 | Ruzuku ya Mishahara | 3,169,255,819 | 2,380,411,830 | 75.11 | 2,380,411,830 | 100 |
| 2 | Ruzuku ya Matumizi ya Mengineyo | 1,200,000,000 | 680,000,000 | 56.67 | 671,043,688.51 | 98.68 |
| 3 | Mapato ya Ndani | 3,073,950,000 | 2,170,504,647.14 | 70.61 | 1,618,306,403.68 | 74.56 |
| **Jumla Kuu** | | **7,443,205,819** | **5,230,916,477.14** | **70.28** | **4,669,761,922.19** | **89.27** |

*Chanzo: Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim*

**242. Mheshimiwa Spika,** Kituo kimetoa huduma ya ushauri elekezi kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Mkakati wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Kadhalika, Kituo kimefanya tafiti kuhusu Utekelezaji wa Diplomasia katika Miradi ya Umma na Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi nchini Tanzania.

**243. Mheshimiwa Spika,** Kituo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani mbalimbali kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Machi 2024, watumishi watano walihitimu mafunzo ya ngazi ya Shahada ya Uzamili, Watumishi 19 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu.

**244. Mheshimiwa Spika,** Kituo kiliendesha kongamano la Amani tarehe 29 Septemba, 2023 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere uliopo Dar es salaam kuadhimisha siku ya Amani Duniani.

**245. Mheshimiwa Spika,** Kituo kimeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo lenye vyumba tisa vya mihadhara ambao umefikia asilimia 24. Mradi unatekelezwa na Kampuni ya M/s Corporation Sole Works Superintendent (CSWS) kwa gharama ya shilingi 4,450,359,568.80 ikijumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Usimamizi wa mradi huo unafanywa na Mshauri Elekezi wa Kampuni ya Aru Built Environment Consulting Company (ABECC) ya Chuo Kikuu cha Ardhi kwa gharama za shilingi 190,000,000.00 pamoja na VAT. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Mkandarasi alikuwa amelipwa kiasi cha shilingi 838,535,851.00 ambayo inajumuisha shilingi 633,897,385.00 fedha ya malipo ya awali (advance payment) na shilingi 204,638,466.00 fedha ya malipo ya kazi.

### 3.2.12.3 Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM)

246. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) ni Wakala Maalumu wa Umoja wa Afrika ulioanzishwa mwaka 2003. Lengo la Msingi la APRM ni kukuza dhana ya Utawala bora kwa kutekeleza sera, viwango na taratibu zitakazopelekea kuimarika kwa siasa (political stability), kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi (high economic growth), uhakika wa maendeleo endelevu (sustainable development), na kuharakisha mtangamano wa kikanda na bara zima la Afrika kwa nchi hizo na kubainisha maeneo ambayo zinafanya vizuri ili kuyaimarisha pamoja na kubadilishana uzoefu.

247. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za APRM Tanzania ni shilingi 1,457,428,933 kati ya fedha hizo, shilingi 630,697,559 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 826,731,374 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha zote ni ruzuku kutoka Serikali Kuu.

**248. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili 2024, APRM Tanzania imepokea shilingi 1,019,979,471.12 sawa na asilimia 69.98 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, shilingi 646,800,168.52 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 373,179,302.60 ni kwa ajili ya mishahara.

**249. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2024, APRM Tanzania imetumia shilingi 823,700,332.42, sawa na asilimia 80.76 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 373,179,302.60 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 450,521,029.82 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jedwali Na. 5 linaonesha mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, kupokelewa na kutumika kwa kipindi husika.

**250. Mheshimiwa Spika,** APRM iliratibu na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 20 ya Kuanzishwa kwa APRM yaliyofanyika mwezi Desemba, 2023 jijini Johannesburg, Afrika Kusini. Zaidi ya kuhudhuria maadhimisho hayo,

Jedwali Na. 5: Mapato na Matumizi ya APRM Tanzania Julai 23 – Aprili 24

| Na. | Maelezo | Bajeti iliyodhinishwa 2023/2024 | Mapato Halisi hadi Aprili 2024 | Asilimia (%) | Matumizi Halisi hadi Aprili 2024 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | C | D | D/C | E | E/D |
| 1 | Ruzuku ya Mishahara | 630,697,559 | 373,179,302.60 | 59.17 | 373,179,302.60 | 100 |
| 2 | Ruzuku ya Matumizi ya Mengineyo | 826,731,374 | 646,800,168.52 | 78.24 | 450,521,029.82 | 69.65 |
| **JUMLA** | | **1,457,428,933** | **1,019,979,471.12** | **69.98** | **823,700,332.42** | **80.76** |

*Chanzo: APRM Tanzania*

APRM Tanzania Iipata fursa ya kushiriki katika mijadala kuhusu mafanikio, changamoto na kuweka mikakati ya kuboresha utekelezaji wa programu na mipango ya APRM.

251. **Mheshimiwa Spika,** APRM Tanzania iliratibu na kufanikisha ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Kikosi Kazi cha Wataalam kujadili Maboresho ya Muundo wa Hojaji za APRM (technical meeting working group workshop on the revision of APRM Governance Index Framework) uliofanyika mwezi Novemba, 2023 jijini Dar es Salaam. Mkutano ulihudhuriwa na washiriki kutoka nchi wanachama wa APRM ikiwemo Afrika Kusini, Uganda, Cape Verde, Nigeria, Ghana, Kenya, Cameroon, Namibia, Gambia, Togo, Zimbabwe na Msumbiji.

252. **Mheshimiwa Spika,** APRM Tanzania iliratibu na kufanikisha Mkutano kuhusu kuhuisha utekelezaji wa Programu za APRM pamoja na namna bora ya nchi za Afrika kukabiliana na Taasisi za Kimataifa za Moods, S & P pamoja na Fitch wakati wa kufanyiwa tathimini za uwezo wa nchi hizo Kukopesheka Kimataifa. Mkutano huu ulifanyika Tanzania, mwezi Agosti, 2023 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi, vyama vya siasa, viongozi wa dini, makundi maalumu na asasi za kiraia na wawakilishi wa APRM ngazi ya Bara la Afrika.

253. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha utendaji kazi wa APRM Tanzania ili iweze kuelimisha wadau na kukuza utawala bora kupitia Vyombo vya Habari, Tovuti na Mitandao ya Kijamii. Vilevile, APRM Tanzania ilishiriki vipindi 21 vya Radio na Televisheni na kuandaa Makala zilizosambazwa kwenye Magazeti mbalimbali. Aidha, APRM Tanzania ilishiriki katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (sabasaba) na kutumia fursa hiyo kuelimisha umma kuhusu Mpango wa Afrika wa kufanya tathmini ya utawala bora.



Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk akiwa na Naibu Waziri Mambo ya Nje Ethiopia Mhe. Balozi Birtukan Ayano wakifungua kitambaa kuonesha jiwe la Msingi la ujenzi wa Ubalozi wa Ethiopia katika mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma baada ya kuweka jiwe hilo huku wakishuhudiwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Ummy Nderiananga, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, Balozi wa Ethiopia nchini Mhe. Shibru Mamo Kedida, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na viongozi wengine wa Chama na Serikali.

# 04 Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana Nazo

254. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo katika kutekeleza mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024:

i. Uelewa mdogo wa wadau ikiwemo sekta binafsi kuhusu Diplomasia ya Uchumi na fursa zitokanazo na mtangamano na mahusiano ya kimataifa.

ii. Upungufu wa watumishi ukilinganisha na mahitaji ya majukumu ya Wizara. Wizara ina watumishi 600 na ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu Wizara inahitaji kuwa na watumishi 669 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

255. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imechukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na changamoto hizo:

i. Kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zitokanazo na ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi;

ii. Kuendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta, Taasisi za sekta binafsi kuchangamkia fursa mbalimbali zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa; na

iii. Kuendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kupatiwa vibali vya ajira mpya na mbadala za kujaza nafasi zilizo wazi.

# 05 Shukrani

256. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa ya hii kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha na kutekeleza vyema diplomasia ya nchi yetu hali inayopelekea Mataifa, Jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa kuunga mkono mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

257. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mataifa, Mashirika ya Kimataifa na Kikanda na wadau wengine kwa ushirikiano na mchango wao mkubwa uliowezesha kufanikisha mipango na miradi mbalimbali nchini. Miongoni mwa wadau hao ni pamoja na Afrika Kusini, Algeria, Angola, Australia, Austria, Brazil, Botswana, Burundi, Canada, China, Comoros, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hispania, Hungary, Indonesia, India, Israel, Italia, Iran, Ireland, Jamhuri ya Czech, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Korea, Japan, Kenya, Kuwait, Liechtenstein, Malawi, Malaysia, Marekani, Mauritius, Mexico, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Palestina, Poland, Qatar, Romania, Rwanda, Saharawi, Singapore, Sri Lanka, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Saudi Arabia, Shelisheli, Slovenia, Somalia, Sudan, Sudani Kusini, Sweden, Ufaransa, Ufilipino, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Ukraine, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno , Urusi, Uswisi, Uturuki, Vatican City, Vietnam, Zambia na Zimbabwe.

258. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, naomba kutoa shukrani kwa Taasisi za Kifedha na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa kama zifuatazo:- African Capacity Building Foundation (ACBF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); 88 Investment Climate Facility for Africa; Benki ya Exim ya China; Benki ya Exim ya India; Benki ya Exim ya Korea; Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Uchumi wa Korea (ECDF); Mfuko wa Maendeleo wa China na Afrika (CAD Fund); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID); Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (UKAID); Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (OPCW); Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); Shirika la Maendeleo la Saudi Arabia (SFD); na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS).

259. **Mheshimiwa Spika,** pia, natoa shukrani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa la

Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Israel (MASHAV); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA); Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Maendeleo la China (CIDCA); Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa 89 (UNIDO); na Taasisi ya Kimataifa ya Afya ya Korea (KOFIH).

260. **Mheshimiwa Spika,** mashirika mengine ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UNWOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmark (DANIDA); Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC); Umoja wa Ulaya (EU); Shirika la Afya Duniani (WHO); na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Vilevile, napenda kuwashukuru Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GiZ); Global Fund; International Committee of the Red Cross; International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies; Khalifa Fund for Enterprise Development (Khalifa Fund); Medecins Sans Frontieres (MSF); Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori (WWF); Aga Khan Foundation (AKDN) The Association of European Parliamentarians with Africa; The Bill and Melinda Gates Foundation; TradeMark Africa; Umoja wa Posta Duniani (UPU); International Telecommunication Union (ITU) Umoja wa Posta Afrika (PAPU) pamoja na mifuko na mashirika mengine ya misaada.

261. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa utendaji wao mahiri unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi, kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki; Balozi Dkt. Samwel William Shelukindo, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Stephen Patrick Mbundi, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje ma Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki; Balozi Said Shaib Mussa, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Bi. Christine Gideon Mwakatobe, Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC), Bw. Lamau A. Mpolo, Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM), na Bw. Felix Wandwe (ndc.), Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim; Wakuu wa Idara, Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi; Wakuu wa Vitengo; na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa weledi, ufanisi, umahiri, moyo wa uzalendo na kujitoa kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu.

# 06 Vipaumbele, Malengo na Majukumu ya Kuzingatiwa na Wizara Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

262. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa sera ya Mambo ya Nje ni mwendelezo wa utekelezaji wa sera ya Ndani ya Nchi. Kwa msingi huo, katika kuchangia utekelezaji wa falsafa ya R4, inayohimiza maridhiano (reconciliation), mageuzi (reforms), ustahimilivu (resilience) na kujenga upya (rebuilding), Balozi za Tanzania nje ya nchi zimepewa jukumu la kuielezea na kuitolea ufafanuzi falsafa hiyo na misingi yake, wanapotekeleza majukumu yao ya kiuwakilishi. Wizara inaamini kuwa utekelezaji wa suala hili, utaiwezesha jumuiya ya kimataifa kufahamu hatua muhimu zinazochukuliwa na Serikali ya awamu ya sita chini ya Mwanadiplomasia Namba moja Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kudumisha demokrasia, haki za binadamu, utawala bora na kulinda tunu za taifa, ikiwemo amani, umoja na mshikamano.

263. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu, Wizara imeandaa mpango mahsusi wa kupima utendaji kazi kwa kutumia viashiria vya matokeo (KPI's) utakaoanza kutumika katika mwaka 2024/25. Mpango huu utaainisha vipaumbele vya Serikali; mpango mkakati wa Wizara; na uhalisia wa eneo la uwakilishi. Aidha, Mpango huu utawawezesha Mabalozi wetu na Wakuu wa Idara na Vitengo, kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia shabaha zilizoanishwa. Napenda kulifahamisha lako Bunge tukufu kuwa, Mpango huu mahsusi wa Wizara utakelezwa kwa pamoja na mfumo wa usimamizi wa utendaji kazi katika utumishi wa umma (PEPMIS).

264. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imejipanga kuimarisha sauti ya Tanzania katika Umoja wa Mataifa ili kurejesha heshima ya nchi katika anga za kimataifa. Tutahakikisha tunapiga kura kimkakati na kuongozwa na Sera ya kutofungamana na upande wowote. Aidha, nchi yetu itaongeza ushiriki katika majukwaa yanayojadili masuala ya kidunia hususani masuala ya kiuchumi, mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali.

265. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mwanachama katika Taasisi, Mashirika na Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa. Uanachama huo una faida mbalimbali kwa nchi ikiwemo za kiuchumi, kiufundi na ushirikiano. Aidha, kupitia uanachama huo, Watanzania wanapata nafasi za ajira katika ngazi ya wataalam

na uongozi. Vilevile, nchi inapata nafasi ya kushiriki kwenye bodi za uongozi za taasisi na mashirika hayo, hivyo kuwa na ushawishi kwenye maamuzi ya kisera yanayopitishwa. Wizara inaboresha Mkakati wa kuhakikisha Watanzania wananufaika ipasavyo na fursa za ajira na ujumbe kwenye kamati zinazosimamia mikataba ya kimataifa pamoja na kusimamisha Watanzania wenye sifa kwenye nafasi za uongozi kwenye taasisi, mashirika ya kikanda na kimataifa. Wizara itaendelea kutumia ushawishi na uhusiano mzuri wa Tanzania na mataifa mbalimbali duniani kutafuta fursa za ajira na uungwaji mkono kwa wagombea wake kwenye chaguzi za kimataifa.

266. **Mheshimiwa Spika,** natoa rai kwa watanzania wote wenye sifa, wakiwemo Wabunge wa Bunge hili tukufu, kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika taasisi za kikanda na kimataifa. Na hapa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb.) kwa kujitokeza kuwania nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani – Kanda ya Afrika. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba Serikali imeridhia kumsimamisha Mhe. Ndugulile kuwa mgombea wa nchi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Balozi za Tanzania zilizopo ndani na nje ya Afrika zitahakikisha anapata ushindi katika uchaguzi huo.

267. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) ili kuhakikisha soko hilo linakuwa msingi imara wa kukuza mauzo nje ya nchi.

268. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Agenda ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kinara wa uhamasishaji wa wanawake na vijana katika eneo huru la biashara la Afrika, ili kuhakikisha wanawake na vijana wa Tanzania na bara la Afrika kwa ujumla wanakuwa mfano bora wa kutumia na kunufaika na fursa za soko huru la Afrika.

269. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imejiwekea vipaumbele, malengo na majukumu ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:

## 6.1 Vipaumbele

i. Kuratibu utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ili kuchochea Uwekezaji, Utalii, na Biashara pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa maendeleo ya Nchi kwa Ujumla;

ii. Kuendelea kuimarisha uratibu na ushirikiano wa uwili pamoja na ushiriki wa Tanzania katika jumuiya na mashirika ya kikanda na kimataifa ili kulinda maslahi ya taifa; pamoja na kustawisha diplomasia ya kisasa na kujenga uhusiano wa karibu na nchi washirika;

iii. Kuongeza ushawishi wa Tanzania kwa Nchi nyingine katika masuala mtambuka, kwenye Jumuiya na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa;

iv. Kushiriki kwenye jitihada za kikanda na kimataifa za kudumisha amani, ulinzi na usalama; na

v. Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, kuimarisha utawala bora na rasilimaliwatu pamoja na kutekeleza miradi ya ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi ya watumishi na vitega uchumi katika balozi za Tanzania na makao makuu.

## 6.2 Malengo na Majukumu ya Kuzingatiwa

270. **Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuunda Kamati iliyokuwa na jukumu mahsusi la kufanya tathmini ya ufanisi na utendaji wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kubainisha mapungufu yanayokwamisha au kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. Kamati iliyoundwa ilisheheni wajumbe waliobobea katika taaluma ya diplomasia na uhusiano wa kimataifa, jambo ambalo limesaidia kuibua masuala mengi yenye tija kwa mustakabali wa taifa. Wizara ilipokea maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi ili kuendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita (6) chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

271. **Mheshimiwa Spika** kati ya mapendekezo yaliyowasilishwa ni kuhuishwa kwa muundo wa Wizara ili kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa ambapo Mheshimiwa Rais alishalitekeleza kwa kuteua Naibu Waziri na Katibu Mkuu wanaoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Aidha, kufuatia uteuzi wa viongozi hao, Wizara imehuisha muundo wake ili kuendana na mabadiliko hayo ya uongozi.

272. **Mheshimiwa Spika** Serikali inamiliki majengo na viwanja katika balozi mbalimbali za Tanzania nje ya nchi na Serikali kila mwaka inatenga fedha kwa ajili ya kuendeleza milki hizo, jambo ambalo huongeza gharama kwa serikali. Aidha katika kuondokana changamoto hiyo kwa serikali napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imepata ridhaa ya Matumizi ya njia mbadala za ufadhili (alternative financing modalities) wa miradi ya kununua, kukarabati na kujenga majengo ya Serikali nje ya nchi kwa ajili ya ofisi za balozi, makazi ya watumishi na vitega uchumi. Njia hizo ni pamoja na ubia (partnership) na hati fungani (bonds). Matumizi ya njia mbadala yatapunguza utegemezi wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo kuharakisha uendelezaji wa milki za Serikali nje ya nchi.

273. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati kuhusiana na maboresho ya Chuo cha Diplomasia, ili kiweze kutoa mchango unaotarajiwa katika nyanja ya uhusiano wa kimataifa na kukifanya kuwa kituo cha rejea cha fikra (Think Tank) katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikibadili jina chuo hiki kuwa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim. Hatua hii inaenda sambamba na kumuenzi mwanadiplomasia huyu nguli nchini Tanzania na katika Bara la Afrika.

274. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais inafikiwa, na kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais kuhusu Tathmini, Ufanisi na Utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, niliunda Kamati ya Wanadiplomasia Nguli na Wabobezi wakiongozwa na Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki (Mst), kufanya mapitio na tathmini ya kina ya Kituo hiki kwa lengo la kubaini maeneo yanayohitaji mageuzi na maboresho ili kufikia azma ya Mheshimiwa Rais. Baadhi ya maeneo hayo ni sheria ya kuanzishwa kwake; muundo; utawala, bajeti, mitaala, miundombinu, ajira na mahala kilipo.

275. **Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uzoefu kutoka katika shule za diplomasia ndani na nje ya bara la Afrika. Ni matumaini yetu kuwa, kukamilika kwa kazi ya Kamati hii mapema mwaka huu, kutatoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais kuhusu Wizara yetu na

hatimaye kuwezesha Kituo hiki kutimiza matarajio ya Mheshimiwa Rais na wadau wake kwa kizazi cha sasa na cha baadaye. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi zake za kufanya mazungumzo ya awali na nchi marafiki kwa lengo ili kuwezesha maboresho ya Kituo hiki.

i. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Diplomasia ya Uchumi ili kuhakikisha nchi inanufaika kiuchumi kutokana na uhusiano wetu wa kidiplomasia na nchi na taasisi mbalimbali duniani;

ii. Kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi, na ziara za Viongozi Wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini kwa lengo la kudumisha uhusiano wa kidiplomasia na kuwania fursa za kiuchumi;

iii. Kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama, hususan Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

iv. Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi na kukarabati majengo ya Balozi za Tanzania kwa kutumia njia mbadala ya kugharamia miradi ikiwemo ubia wa Serikali na Sekta Binafsi (public private partnership) na hati fungani.

v. Kuratibu ushiriki wa diaspora katika kuchangia maendeleo ya Taifa ikiwa ni pamoja kuimarisha na kukamilisha taratibu za utambuzi na usajili ili kuwezesha utekelezaji wa Hadhi Maalum kwa Raia wa Nchi nyingine wenye Asili ya Tanzania.

vi. Kuimarisha utendaji kazi wa Balozi na Konseli Kuu kwa kuzipatia rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi stahiki kulingana na mahitaji mahsusi ya vituo.

vii. Kuandaa nyaraka na miongozo ya kidiplomasia ikiwemo diplomasia ya umma na mawasiliano ya kimkakati, kitabu cha wanadiplomasia (diplomatic handbook) na Mwongozo kwa Wanadiplomasia waliopo nchini (diplomatic manual);

viii. Kuratibu na kushiriki mikutano ya ujirani mwema ili kuimarisha ulinzi na usalama, diplomasia na biashara kati ya Tanzania na nchi Jirani;

ix. Kuendelea na utekelezaji wa maboresho ndani ya Wizara kwa kuzingatia maelekezo ya Baraza la Mawaziri yaliyotokana na mapendekezo ya Kamati ya Rais ya kutathmini utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Kamati ya Wizara ya Mapitio ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim; na Taarifa Maalum ya Kutathmini hali ya Uwakilishi, Utumishi na Majengo katika Balozi za Tanzania Nje.

x. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa majukumu ya Wizara ikiwepo kukamilisha mfumo wa ufuatiliaji maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Dashboard), mfumo wa kuhifadhi utekelezaji wa Mikataba na Hati za makubaliano, na mfumo wa usajili wa Diaspora kijiditali (DDH);

xi. Kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuongeza fedha za kigeni nchini;

xii. Kuimarisha ukaguzi wa ndani na mifumo ya udhibiti Makao Makuu na Balozi za Tanzania; na utunzaji wa mali za Serikali;

xiii. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, na makubaliano ya uwili, kikanda na kimataifa kwa kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini;

xiv. Kuhuisha ushiriki wa Tanzania kwenye Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM);

xv. Kuendelea na maboresho ya miundombinu, muundo na utendaji kazi katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma;

xvi. Kuendelea na maboresho ya miundombinu, muundo na utendaji kazi katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) kwa lengo la kuongeza ufanisi na mapato kwa Taasisi na mchango wake kwa Taifa;

xvii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi; na

xviii. Kuendelea kutoa Elimu kwa Umma kupitia Diplomasia ya Umma kuhusu ushirikiano wa pande mbili, kikanda na kimataifa na fursa zinazopatikana kutokana na uanachama wa nchi yetu kwenye jumuiya za kikanda na kimataifa pamoja na mikataba/makubaliano tunayoingia na nchi ama mashirika ya kimataifa.

07

# Malengo ya Taasisi Zilizo Chini ya Wizara Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

## 7.1 Kituo Cha Kimataifa Cha Mikutano Arusha (AICC)

**276. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha ni mhimili muhimu wa Wizara katika utekelezaji wa Diplomasia ya Mikutano. Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuendelea kukiwezesha kituo hiki, ambapo mwezi Machi, 2024 alimteua Bi. Christine Gideon Mwakatobe kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo. Ni imani yetu sote kuwa Bi. Mwakatobe atayabeba maono ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kukuza Utalii kupitia Diplomasia ya Mikutano.

**277. Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii, kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kituo kimeanza mageuzi ya kuboresho utendaji kazi, kuleta ufanisi, kuongeza mapato na kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma. Miongoni mwa juhudi hizi ni pamoja na kuweka mifumo ya teknolojia ya kisasa ya usimamizi na uendeshaji wa Kituo ikiwemo katika milki zake, uendeshaji wa Hospitali na usimamizi na uendeshaji wa huduma ya mikutano. Aidha, Kituo kimejipanga kuendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ya changamoto za utoaji huduma ili kuhakikisha zinaendana na hali halisi ya soko.

**278. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hatua nilizoainisha, Kituo kimepanga kuendelea kuwajengea uwezo kwa watumishi wake kwa lengo la kuwaongezea weledi, ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu.

**279. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, AICC imepanga kukusanya mapato ya shilingi 29,523,318,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya ndani. Kiasi hiki ni nyongeza ya asilimia 40, ikilinganishwa na mapato ya mwaka wa fedha 2023/2024.

**280. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 AICC tayari imepokea uthibisho wa mikutano 22 yenye thamani ya shilingi 4,879,646,247 na USD 1,198,474.20. Kiasi hiki kinahusisha mikutano 17 ya Kitaifa na Kimataifa na yenye thamani TZS. 4,398,985,921.00 na USD 1,052,333.20 katika Kituo cha Arusha na mikutano mitano ya kitaifa na kimataifa yenye thamani ya TZS. 480,660,326 na USD. 146,141 katika kituo cha JNICC. Mafanikio haya ya awali yanatokana na juhudi kubwa ya kutangaza utalii wa mikutano ndani na nje ya nchi na kuimarisha huduma za kituo.

281. **Mheshimiwa Spika,** AICC inaendelea kukamilisha taratibu za ujenzi wa Kituo kipya cha kimataifa cha mikutano ambacho kitaitwa Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC) ndani ya jiji la Arusha. Kituo hiki kitakuwa cha kisasa na kikubwa zaidi Afrika Mashariki na Kati. Kituo hicho kitajengwa katika eneo linalomilikiwa na AICC lenye ukubwa wa ekari 21 na kitakuwa na uwezo wa kuchukua takribani watu 10,000 kwa mara moja katika ukumbi mmoja. Vilevile kitakuwa na kumbi zingine ndogo ndogo za mikutano zenye uwezo wa kuchukua watu 10 hadi 3,500 na eneo la maonesho kwa ajili ya matukio mbali mbali. Ujenzi wa MK-ICC utaipatia Tanzania fursa za kushindana vyema katika sekta ya utalii wa mikutano na kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia ya mikutano na maonesho hapa nchini. Kituo hicho kitaongeza mapato ya fedha za kigeni, pamoja na kuchochea kasi ya ukuaji wa Uchumi kwa Serikari na Sekta binafsi.

282. **Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Kituo cha MK-ICC utakapokamilika, utavutia mikutano mikubwa ya kitaifa na kimataifa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania iliibuka mshindi na kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa Kimataifa wa wafugaji nyuki duniani, Apimondia utakaofanyika mwezi Septemba, 2027 na kuleta wageni zaidi ya 5,000 katika nchi yetu. Wizara yetu imejipanga vyema na ipo tayari kuhakikisha kwamba kituo hiki kinajengwa na kukamilika kwa wakati.

283. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio haya yametokana na azma na juhudi za Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na Mwanadiplomasia namba moja ya kuifungua nchi kukuza utalii na uwekezaji.

## 7.2 Kituo Cha Uhusiano wa Kimataifa Cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS – CFR)

284. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Katika hatua ya kuboresha utendaji kazi wa Chuo cha Diplomasia, ili kiweze kutoa mchango unaotarajiwa katika nyanja ya uhusiano wa kimataifa na kukifanya kuwa kituo cha rejea na fikra (Think Tank) katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikibadili jina chuo hiki kuwa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim. Hatua hii inaenda sambamba na kumuenzi mwanadiplomasia huyu nguli nchini Tanzania na katika Bara la Afrika.

285. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais inafikiwa, na kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais kuhusu Tathmini, Ufanisi na Utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki , niliunda Kamati ya Wanadiplomasia Nguli na Wabobezi wakiongozwa na Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki (Mstaafu), ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Parole kufanya mapitio na thatmini ya kina ya Kituo hiki kwa lengo la kubaini maeneo yanayohitaji mageuzi na maboresho ili kufikia azma ya Mheshimiwa Rais. Baadhi ya maeneo hayo ni sheria ya kuanzishwa kwake; muundo; utawala, bajeti, mitaala, miundombinu, ajira na mahala kilipo.

286. **Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uzoefu kutoka katika shule za diplomasia ndani na nje ya bara la Afrika. Ni matumaini yetu kuwa, kukamilika kwa kazi ya Kamati hii mapema mwaka huu, kutatoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Mheshimiwa Rais kuhusu Wizara yetu na

hatimaye kuwezesha Kituo hiki kutimiza matarajio ya Mheshimiwa Rais na wadau wake kwa kizazi cha sasa na cha baadaye. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi zake za kufanya mazungumzo ya awali na nchi marafiki kwa lengo ili kuwezesha maboresho ya Kituo hiki.

**287. Mheshimiwa Spika,** Kituo kinakadiria kupokea na kutumia fedha kiasi cha shilingi 7,720,841,396 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,685,500,000 zitatokana na mapato kutoka vyanzo vya ndani na shilingi 5,035,341,396 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Ruzuku kutoka Serikali kuu inajumuisha shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 3,835,341,396 kwa ajili ya mishahara.

**288. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, SAS-CFR inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi yanayohusu masuala ya diplomasia, uhusiano wa kikanda na kimataifa, stratejia, lugha za kigeni, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa Amani;

ii. Kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwa Serikali na wadau wengine wa sekta binafsi kwenye maeneo yanayohusu diplomasia, uhusiano wa kikanda na kimataifa, stratejia, lugha za kigeni, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa Amani;

iii. Kukamilisha uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

iv. Kukitangaza chuo kitaifa na kimataifa ikiwemo kuingia mikataba ya mashirikiano na taasisi zingine za elimu ndani na nje ya nchi;

v. Kutekeleza mpango wa mabadiliko ya kitaasisi kulingana na maelekezo yaliyotolewa na viongozi wa juu na Mpango wa Chuo; na

vi. Kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi ikiwemo kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa Chuo.

## 7.3 Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia

**289. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, APRM Tanzania imepanga kutumia kiasi cha shilingi 1,257,428,928, ambazo ni fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi 626,731,369 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 630,697,559 ni kwa ajili ya mishahara.

**290. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, APRM Tanzania inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kukamilisha taarifa ya tathmini ya ndani (Country Self-Assessment Report) kwenye Utawala Bora; na

ii. Kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM, kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti.

# 08 Makadirio ya Mapato Na Matumizi ya Wizara Kwa Mwaka 2024/2025

## 8.1 Kituo Cha Kimataifa Cha Mikutano Arusha (AICC)

291. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,454,426,000 ikiwa ni maduhuli ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vilivyopo makao makuu na balozi za Tanzania nje. Vyanzo hivyo vya mapato vinajumuisha upangishaji wa nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na zoezi la kuthibitisha nyaraka.

292. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 241,069,232,000 kati ya fedha hizo Shilingi 229,435,856,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi 210,926,213,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 18,509,643,000 ni kwa ajili ya mishahara. Aidha shilingi 11,633,376,000 imetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

293. **Mheshimiwa Spika,** bajeti ya matumizi mengineyo inajumuisha shilingi 1,257,428,928 kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia; shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim; shilingi 1,400,000,000 kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; shilingi 280,000,000 kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika; na shilingi 250,000,000 kwa ajili ya Kituo cha Kikanda cha Kupambana na Ugaidi cha SADC.

294. **Mheshimiwa Spika,** aidha, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizotengwa shilingi 3,835,341,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim.

295. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia fedha kiasi cha shilingi 11,633,376,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha shilingi 5,633,376,000 kwa ajili ya kugharamia ujenzi, ukarabati na ununuzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini; shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu jijini Arusha; na shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim jijini Dar es Salaam.

**296. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Wizara imepanga pia kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo yenye makisio ya thamani ya shilingi 343,100,000,000 kutoka vyanzo mbadala ikiwemo ubia na mikopo ya karadha. Fedha hizo zinajumuisha shilingi 127,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na kitega uchumi Nairobi, Kenya; shilingi 66,100,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, makazi ya Balozi na vitega uchumi Lusaka, Zambia na shilingi 150,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, makazi ya balozi na kitega uchumi Kinshasa, DRC.

## 8.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi Zilizo Chini ya Wizara Kwa Mwaka 2024/2025

### 8.2.1 Kituo Cha Kimataifa Cha Mikutano Arusha (AICC)

**297. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Kituo kimepanga kukusanya mapato ya shilingi 29,523,318,000 kutokana na vyanzo vya ndani. Mapato yatatumika kugharamia uendeshaji wa Kituo, mishahara na miradi ya maendeleo ya upanuzi na ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya AICC pamoja na vifaa vya TEHAMA na samani za vyumba vya mikutano.

### 8.2.2 Kituo Cha Uhusiano wa Kimataifa Cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS - CFR)

**298. Mheshimiwa Spika,** Kituo kinakadiria kupokea na kutumia fedha kiasi cha shilingi 7,720,841,396 katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,685,500,000 zitatokana na mapato kutoka vyanzo vya ndani na shilingi 5,035,341,396 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Ruzuku kutoka Serikali kuu inajumuisha shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 3,835,341,396 kwa ajili ya mishahara.

### 8.2.3 Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini Katika Masuala ya Utawala Bora na Demokrasia

**299. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, APRM Tanzania imepanga kutumia kiasi cha shilingi 1,257,428,928, ambazo ni fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi 626,731,369 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 630,697,559 ni kwa ajili ya mishahara.

# Hitimisho

09

**300. Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 241,069,232,000 Kati ya fedha hizo shilingi 229,435,856,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 11,633,376,000 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**301. Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyoendesha vikao vya Bunge kwa uzalendo na umahiri wa hali ya juu. Vilevile kwa niaba ya Wizara napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mchango mkubwa walioutoa kwa Wizara yangu.

**302. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Viongozi mbalimbali, wadau wa Nishati pamoja na Washiriki wengine wa Mkutano huo uliofanyika Makao Makuu ya UNESCO Jijini Paris, Ufaransa mwezi Mei, 2024.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Mji wa Serikali, Mtumba

40466, Dodoma, Tanzania

S. L. P. 2933, Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 26 2323201 - 7

foreign.go.tz